

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Tano – Tarehe 14 Februari, 2011**

*(Mkutano uilanza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 52

**Idadi Kubwa ya Wananchi Kutopiga Kura**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM** aliuliza:-

Katika uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba, 2010 ilibainika kwamba zaidi ya Watanzania milioni kumi na moja hawakupiga kura kati ya wananchi milioni ishirini waliojiandikisha kupiga kura:-

Je, ni sababu zipi za msingi zilizopelekea idadi hiyo kupungua sana?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu ni haki ya kila raia mwenye sifa kama ilivyoainishwa kwenye Ibara 5(1) na (2) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Ingawa katika Sheria za nchi hii, upigaji wa kura ni hiyari, hakuna Sheria inayolazimisha mtu kupiga kura.

Katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 31 Oktoba, 2010, Watanzania waliojiandikisha walikuwa 20,137,303 na waliojitokeza kupiga kura ni 8,626,283 sawa na asilimia 42.83.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya sababu zilizochangia kwa Wapiga kura kujitokeza kupiga kura siku ya Uchaguzi ni kama ifuatavyo:-

- (i) Elimu ya Uraia pamoja na Elimu ya mpiga kura kutotolewa kwa kiwango na muda wa kutosha.
- (ii) Baadhi ya vituo vyatupiga kura kuwa mbali na maeneo ya makazi ya watu hasa Vijijini.
- (iii) Kuhama kwa kupiga kura kutoka kwenye Majimbo na Kata walizojiandikisha kuwa Wapiga kura kutokana na sababu mbali mbali.
- (iv) Baadhi ya wananchi kutopiga kura kutokana na majina yao kutoonekana katika orodha ya wapiga kura kwenye vituo vyatupiga kura kutokana na kasoro mbalimbali.
- (v) Dharura mbalimbali ikiwemo hali ya mvua katika baadhi ya maeneo ziliwafanya wananchi kutojitokeza kwenda kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inakamilisha taarifa kamili ambayo itabainisha mafanikio na kasoro zote zilizojitokeza. Taarifa hiyo itakapokamilika, itatolewa kwa umma na wadau wote. (*Makofi*)

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa sensa ya idadi ya watu ya mwaka 2002 ilibainisha wazi kwamba asilimia 44.2 ya Watanzania wako katika umri kuanzia siku moja hadi miaka kumi na nne na asilimia 51.8 ya Watanzania ambao wako katika umri wa miaka kumi na tano hadi miaka sitini na nne. Ndani ya kundi hilo miaka 15-17 hawana sifa za kujiandikisha kupiga kura na asilimia 3.9 ya Watanzania wako katika umri wa miaka 65 na zaidi, taswira au picha kamili inavyoonekana kwamba siku zote watu walioko chini ya umri wa miaka 18 ni wengi zaidi kuliko wale wa umri wa miaka 18 na kuendelea.

Je, sasa kilichotokea Tanzania ambapo mwaka huu asilimia 50 ya wapiga kura. Asilimia 50 ya watu wa Tanzania yote yani milioni 20 wameweza kujiandikisha kupiga kura. Je, kuna nchi nyingine yeyote ambayo ufanisi huu umepatikana?

(ii) Mmesema hapa Mheshimiwa Waziri kwamba taarifa kamili itatolewa na kwa kuwa vyama vyatupiga kura na mlivishirikisha kikamilifu au ripoti ilikuwa ni upande mmoja tu kwa Tume ya Uchaguzi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU- SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa kwamba takwimu za Wapiga Kura ukilinganisha na idadi ya watu waliopiga kura, zimeendelea kupungua mwaka hadi mwaka, tulivyoanza mfumo wa

vyama vingi mwaka 1995, asilimia 76.7 kati ya watu waliojiandikisha walipiga kura. Mwaka 2000 asilimia 84.4 kati ya watu waliojiandikisha kupiga kura. Naomba radhi takwimu ni ndefu siwezi kuzisoma, lakini ukipenda naweza nikakupa baadaye.

Mwaka 2005 asilimia 72 walipiga kura, mwaka huu asilimia 42.83. kama nilivyosema sababu ni nyingi, lakini wenzetu waliopewa kazi hii kisheria Tume, wanafanya utafiti hivi sasa za kujua sababu. Hizi nilizosema ni baadhi tu ambazo wengine tumezunga kwa macho. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira hiyo taarifa nataka kuwaahidi wote mtapata, itachapishwa, tutaiteta na tutraigawa kwa wadau wote. Najua sababu ziko nyingi nikizieleza hapa nyingine zinaweza kuwa za kubuni na kila mmoja hapa pengine anaweza kuwa na sababu nyingi. Kwa hiyo, naomba tuvute subira.

Lakini ni ukweli ulio wazi ni kwamba yapo Mataifa mengine ambayo pengine takwimu kama hizi wameweza kujitokeza kwa uchache kama ilivyojitokeza Tanzania. Lakini naomba radhi kwa leo sina mlolongo wa takwimu ya nchi hizo. Lakini naweza nikazitafuta nikazipata. Muhimu ni kwamba suala hili halikusababishwa na chama chochote, suala hili halikusababishwa na Serikali, halikusababishwa na Chama cha Mapinduzi (CCM).

Kama nilivyokuwa najibu swalı langu la Jumatatu iliyopita, suala hili linahitaji ushirikiano wa pamoja. Vyama vyote vyta siasa ni wadau katika zoezi hili. Sisi wote tulihimiza wanachama wetu wajandikishe, tulipaswa wote kuwahimiza wananchi hawa wapige kura. Wote tuna *interest* au tuna nia moja, kila mmoja alitaka hawa wapiga kura ili tupate kura, hatujui hizi kura zilizopotea zingekuwa za nani. Kwa hiyo, bado vyovyote itakavyokuwa kwa mfumo wowote hata ndani ya Katiba mpya, mabadiliko yote lazima wananchi waelimishwe kupitia Vyama vyta Siasa na Taasisi nyingine zote ili watekeleze wajibu wao.

Na. 53

### **Kijiji cha Kibakwe kuwa na Mamlaka ya Mji Mdogo**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:-

Kijiji cha Kibakwe sasa kimekuwa kutokana na kuwepo kwa umeme, shughuli za uchimbaji Madini ya Vito na Shaba, hali iliyosababbisha wananchi kujenga nyumba bora, idadi ya watu kuongezeka na utoaji wa huduma za kijamii kama maji, masuala ya usafi na afya kwa ujumla kushindikana kusimamiwa na Serikali ya Kijiji:-

Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya kikitangaza Kijiji cha Kibakwe kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vigezo muhimu vya kuanzisha Mamlaka ya Mji Mdogo kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Mji Na. 8 ya mwaka 2007 (*The Urban Planning Act. No. 8 of 2007*) ni vifuatavyo:-

- (i) Eneo liwe na idadi ya watu wasiopungua 10,000;
- (ii) Kuwepo na huduma za jamii zifuatazo:- Kituo cha Afya, shule ya sekondari, soko na maduka 20 ya reja reja yenye leseni na Mahakama ya Mwanzo; na
- (iii) Eneo liwe na Makao Makuu ya Kata au Tarafa.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kibakwe kipo katika Kata ya Kibakwe, Tarafa ya Kibakwe. Sensa ya watu ya mwaka 2002, inaonesha kuwa Kijiji hiki kilikuwa na idadi ya watu 6,298. Kwa mwaka 2010 Kijiji hiki kilikadiriwa kuwa na idadi ya watu wapatao 8,312 (ongezeko la asilimia 2.1 kwa mwaka). Huduma za jamii zilizopo ni pamoja na Kituo cha Afya (1), Shule ya Sekondari (1). Maduka ya reja reja (16) na Soko(1). Katika Kijiji cha Kibakwe ndipo yalipo Makao Makuu ya Kata na Tarafa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia vigezo hivyo na taarifa tulizo nazo kutoka Halmashauri, pamoja na nia nzuri ya Mheshimiwa Mbunge wa Kibakwe ya kutaka Kijiji hiki kipande hadhi kutokana na maendeleo yaliyotokana na madini ya vito na shaba, Kijiji cha Kibakwe bado hakijakidhi vigezo vya kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kibakwe kitakapokuwa kimekidhi vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria na utaratibu za maombi kuzingatia, Serikali itapokea maombi hayo na kuyashughulikia.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwanza niseme tu kwamba kwa vigezo ambavyo amevitaka Mheshimiwa Waziri, ni kwamba ni kama, katika vitatu, ni kama viwili tunakidhi, kinachokosekana hapa ni hiki cha idadi ya watu ambapo hapa niseme kimsingi kabisa natofautiana kitakwimu na nadhani ni vizuri tukakaa pamoja, lakini tatizo langu ni kwamba kwa kuwa vigezo vingi tunakidhi na sikubaliani na takwimu zilizotolewa hapa za idadi ya watu.

Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari mimi na yeye tukae na kuangalia namna ya kupata takwimu sahihi ili aweze kunipa jibu hili upya?

Mheshimiwa Spika, swalı langu ni kwamba, kuna baadhi ya miji ambayo ilikwisha tangazwa, miji midogo imetangazwa na hajjaweza kuanza na ni muda mrefu sasa umepita na uzoefu unaonesha miji ambayo inatangazwa ikiwa kwenye Makao Makuu ya Wilaya inachelewa kuanza kuliko ambayo iko pembedi na Makao Makuu ya Wilaya, kwa sababu wale wana shauku ya kuendeleza sehemu waliopo kutoka kwenye Kijiji kuwa Mji Mdogo.

Je, Serikali haiyoni kuna haja ya kuangalia *separate* kwa mfano kama Kibaigwa ilivyo na Kongwa, kwamba Kibaigwa imeweza ku-*take off* kiharaka zaidi kuliko hata Kondoa, kuliko hata Mpwapwa. Je, Waziri anasemaje juu ya hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja hili la takwimu Mheshimiwa SimbaChawene, mimi sina tatizo. Takwimu nilizozitoa hapa ni takwimu ambazo sisi tumezifanyia kazi. Lakini kama Mbunge anafikiri kwamba takwimu kwa sababu yeye ndiyo anakaa na watu kule kama anawahesabu, mimi sina tatizo kabisa.

Kuhusu vigezo nitakavyotumia ni hivihivi ambavyo navisemea hapa, labda aseme sasa kwamba tubadilishe vigezo hivi ndiyo utapata matokeo tofauti na haya yanayozungumzwa hapa. Mheshimiwa Simbachawene ni rafiki yangu, niko tayari kukaa naye tuzungumze, tuangalie kwamba vigezo hivi vikoje na ile idadi.

Mheshimiwa Spika, la pili analozungumzia hapa ni la msingi sana. Sisi hatusemi kwamba pale tu palipo Makao Makuu ya Tarafa au Kata au Wilaya ndipo paanzishwe na anataja Kibaigwa kwa maana kwamba amekuwa *concrete*. Kibaigwa pale *development* yake unavyoingalia inavyokwenda pale, ukiisha hivyo hivyo maana yake ni kwamba siku ukija kuamua kuufanya uwe Mji pale patakuwa pamevurugika.

Anachosema Mheshimiwa Simbachawene ni kwamba kule Kibakwe kuna *development* kama hiyo kwa maana ya madini yanayopatikana pale, ni *problem*. Halmashauri ya Mpwapwa ikikaa, ikaona kwamba kuna haja ya kuwa na Kibakwe amba ni Mji mdogo, sisi tutapokea.

Mheshimiwa Spika, tumesema hapa msisahau kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa imeshapitisha Azimio kwamba Mji wa Mpwapwa uwe ni Mji Mdogo wa Mpwapwa.

Sasa kama Mpwapwa wanafikiri kwamba wanaweza wakawa na yote miwili, Kibakwe na Mpwapwa, sisi tutawasikiliza wao, kwa sababu wao ndiyo wanaoleta pendekexo, mimi sina tatizo na hilo. (*Makofii*)

**SPIKA:** Punguzeni majibu marefu inasabisha muda usitoshe. Tunaenda Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Mariam Kasembe.

Na. 54

### **Uchimbaji wa Bwawa Katika Mto Miesi - Masasi**

**MHE. MARIAM R. KASEMBE** aliuliza:-

Serikali imeandaa mpango wa kukarabati Bwawa la Mcchema na kuchimba Bwawa lingine katika mto Miesi Wilayani Masasi:-

Je, kazi hii itaanza lini na itatumia gharama kiasi gani kukamilisha mpango huo?

### **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, nijibu swali la Mheshimiwa Kasembe, kama ifuatavyo:-

Bwawa la Mcchema linahitaji ukarabati wa tuta, kuziba eneo lililopasuka pamoja na utoro wa maji. Ili kufanya kazi hii upembusi yakinifu, usanifu na uandaaji wa michoro kwa ajili ya ujenzi, pamoja na uandaaji wa zabuni ya ujenzi imekamilika. Zabuni zimetangazwa katika gazeti la *Daily News* la tarehe 7/1/2011.

Kazi ya ujenzi wa bwawa inatarajiwa kuanza pindi taratibu za manunuzi za kumpata Mkandarasi zitakapokamilika.Kwa vile zabuni imetangazwa gharama zitajulikana baada ya kufungua tenda ya ujenzi. Ujenzi utachukuwa muda wa wiki 18.Ujenzi wa bwawa jipya katika Mto Mesi,umewekwa kwenye mipango ya muda wa kati.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa katika majibu yake ya msingi Mheshimiwa Waziri amesema uchimbaji wa Bwawa jipya la Mto Mesi litawekwa katika mpango wa kati.

(i) Je, haoni ni vyema akatueleza kwamba mpango huu wa kati ni lini ili wananchi wangu wa Jimbo la Masasi wawe na matumaini na kuelewa ni lini Bwawa hili litaanza kuchimbwa?

(ii) Kwa kuwa tatizo la maji katika Mji wetu wa Masasi na Vijiji vyake sasa hivi ni kubwa sana kiasi kinachopelekea wananchi kununua maji ndoo ya lita 20 kwa shilingi elfu moja.

Mheshimiwa Waziri uko tayari kuja na wataalam wako kuja kuangalia chanzo cha maji cha Mto Ndanda na Mto Mesi pamoja na mabwawa ambayo yapo katika Kijiji cha Chingulungulu, Chiwale, Lukuledi, Mihima na Mtakuja kwa sababu inaonyesha wataalamu tulionao wameshashindwa kazi na wananchi wanaendelea kuteseka.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu kwa niaba ya Waziri wa Maji, maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Nilivyosema katika jibu la msingi, kwamba tumeweka mipango ya muda wa kati, lakini tatizo kubwa ni kwamba tunataka wananchi wa Masasi wapate maji. Mpango uliopo sasa hivi tuna mradi mkubwa wa maji, katika chanzo cha Mbwinji ambacho tayari mkandarasi yupo na ameshaanza kazi na tunategemea baada ya miezi 15 mradi huo utakuwa umekamilika na wananchi watapata maji kwa asilimia mia moja.

Kuhusu kwenda Masasi, nitajipanga pamoja wataalamu wangu twende tukaangalie hivyo vyanzo ambavyo Mheshimiwa Mbunge amependekeza.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa mazingira ya Vijiji vya Jimbo la Masasi ya kuwa na tatizo la maji yanafanana au yanakaribia kufanana na tatizo la maji ya Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro *Orkestement* ambapo Serikali iliahidi na kuitisha Bajeti ya dharura kwa ajili ya kunusuru mazingira hayo magumu na hadi sasa Hazina haijatoa hata senti tano kati ya shilingi bilioni 1.8 ambayo iliridhiwa na Bunge hili.

Serikali inatoa ahadi gani kwa wananchi wa Simanjiro kwa ahadi hiyo ya dharura ambayo mpaka sasa ni karibu mwaka mzima unakaribia kwisha wakati wananchi wanaendelea kuteseka?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka kama ifuatavyo:-

Ni kweli kunaweza kuwepo hizo ahadi ambazo Serikali imetoa na tumetoa ahadi hizo sehemu nyingi na sisi dhamira yetu ya Serikali ni kwamba tuhakikishe kwamba wananchi wetu wanapata maji safi na salama kwa asilimia takribani 60 katika Vijiji na takribani 90 katika Miji yote.

Kwa hiyo, naomba atupe muda tufuutilie ahadi hiyo na tuone namna gani tutakavyoitekeleza.

## **Mchakato wa Ajira za Askari Polisi**

**MHE. OMARY AHMAD BADWEL** aliuliza:-

Mchakato wa ajira za askari polisi huchukua muda mrefu kiasi cha kufikia miezi kumi na miwili (12) ndipo wanathibitishwa kazini:-

- (a) Je, Serikali haioni kuwa, utaratibu huo ni wa uonevu mkubwa kwa polisi?
- (b) Je, Serikali ina mipango gani ya kufanya marekebisho ya Sheria na taratibu mbalimbali zinazohusiana na ajira za polisi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mhesihmiwa Omary Ahmad Badwel, Mbunge wa Bahi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mchakato wa ajira katika jeshi la polisi hauchukui miezi kumi na mbili (12) kama alivyoleza Mheshimiwa Mbunge. Ajira ya askari polisi huanza mara tu anaposajiliwa (*enlistment*) kama *recruit constable* katika Chuo cha Polisi, hii ni kwa mujibu wa kifungu D.1 (2) (a) cha Kanuni za Utumishi za Jeshi la Polisi (*Police Force Service Regulations*) za mwaka 1995. Hata hivyo, mara tu anaposajiliwa hutakiwa kufanya kazi kwa mkataba wa miaka mitatu mitatu hadi anapotimiza miaka kumi na mbili (12) ambapo hupewa uhuru wa kuchagua kuendelea kufanya kazi kwa mkataba (*gratuity*) au malipo ya izeeni (*pensionable*).

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu B.12 (4) cha Kanuni hizo askari anapochagua kufanya kazi kwa masharti ya malipo ya izeeni ndipo huthibitishwa kazini. Hata hivyo askari akifikia cheo cha Mkaguzi Msaidizi (*Assistant Inspector*) huingia kwenye malipo ya izeeni hata kama hajatimiza umri wa miaka 12 kazini.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huu nilioueleza hapa juu hamna uonevu wowote. Hata hivyo nitamke kwamba Serikali inaendelea kufanya marekebisho ya Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali zinazohusiana na ajira na utendaji wa polisi kuitia mpango wa maboresho wa Jeshi la Polisi (*Tanzania Police Force Reform Programme*).

**MHE. OMARY AHMAD BADWEL:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza na ninashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Swali langu la msingi lilionyesha kwamba askari hawa wanapata kuajiriwa kwa muda mrefu sana na huu ni uonevu. Lakini katika mchakato wa jibu la Mheshimiwa Waziri ameonyesha ni namna gani askari wanapata ajira kamili baada ya miezi 12 kwa kuchagua kwenda katika mkataba au malipo ya izeeni. Swali langu linarudi pale pale kiasi cha miaka 12 tofauti na watumishi wengine wote katika nchi hii?

Mheshimiwa Waziri haioni kwamba huo ni uonevu kwa askari polisi na hasa wa cheo cha chini. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kurekebisha sheria hii kwa ajili ya polisi nao wapate haki ya kuajiriwa katika muda mfupi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, hakika niseme kwamba hizi *concerns* alizonazo na sisi tunazo. Ndiyo maana nimesema kwamba tunao mchakato wa maboresho ambayo tutabdalishwa hizi Sheria. Hizi Sheria zimekuwepo kwa muda mrefu sana na ninaweza nikalitamkia Bunge kwamba *they are completely outdated*, lazima tupate utaratibu mpya. Kusema kwamba ni uonevu bado nasema hapana, ni utaratibu ambaou umekuwepo. Lakini baada ya kutazambua kwa muda mrefu tumeona hautufai na kweli tuko katika mchakato wa kuubadilisha. Nadhani nitakuwa nimejibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Ahsante, swali lingine la nyongeza Mheshimiwa Abdallah Haji Ali. Umekaa sivyo. Kila mtu akae kwenye kiti tulichomwekeea.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, naitwa Mussa Haji Kombo, kutoka Chake Chake. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Namwomba Mheshimiwa Waziri anisaide kupata utaratibu wa askari, anaajiriwa mtu wa aina gani hasa akiangalia chombo hiki ni cha Muungano. Mheshimiwa ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, utaratibu uko wazi na uko bayana. Ni utaratibu ambaou unaanzia chini, unaanzia Wilayani, nafasi zinatangazwa na utaratibu wa jinsi watu ambaou wanaweza wakaomba ajira katika Jeshi la Polisi ukawekwa bayana. Kwa hiyo, Kamati za Ulinzi na Usalama za nchi yetu zinakaa katika ngazi mbalimbali, kuanzia ngazi ya Wilaya, wakiwemo viongozi wa polisi, inakuja katika ngazi ya mkoa, mpaka inakuja katika ngazi ya Taifa.

Lakini niseme kwamba ni ajira ambazo zinatangazwa na zinakuwa kwenye magazeti na watu wanazona, wananchi wote wanazona na wanafuata taratibu hizo mpaka inafikia ngazi ya juu ambapo maamuzi yanafanyika ya kuona nani anafaa kuajiriwa katika Jeshi la Polisi.

Lakini nikujibu, nikizingatia maagizo ya Mheshimiwa Spika, kwamba lazima tuwe na majibu mafupi katika majibu yetu. Ni kwamba tunakuwa na utaratibu wa uangaliaizi zaidi. Kwa sababu hiki ni chombo ambacho kinataka umakini sana wa kuwapata watu ambaou kwa kweli watalitumikia jeshi letu bila kuliweka doa na ndio maana kunakuwa na kipindi cha muda mrefu cha kuweza kuwatazama na kuweza kuwachuja kuona ni watu gani ambaou wanafaa.

Lakini hata hivyo katika utaratibu wa maboresho tuliokuwa nao sasa hivi tunajaribu kutazama ni njia zipi zinaweza kuwa bora ambazo zinaweza zikahamasisha na kuhusisha wananchi wote kwa ujumla bila kuonekana kwamba kuna upendeleo katika wale ambaou wanaajiriwa katika Jeshi la Polisi.

### **Zana Bora za Uvuvi**

**MHE. SAID MOHAMED MTANDA** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiwahamasisha wavuvi kuchoma nyavu zao na kuwaahidi kuwatafutia vifaa bora vya uvuvi ili waondokane na uvuvi haramu:-

Je, Serikali imetekeleza kwa kiwango gani ahadi hiyo, kwa kuwapatia nyavu pamoja na boti wavuvi waishio katika kijiji cha Mchinga Kijiweni?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Mtanda, Mbunge wa Mchinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, inahamasisha wavuvi kutumia zana bora za uvuvi ili kuboresha uvuvi kujiongezea kipato na kutunza mazingira katika maeneo ya uvuvi.

Kwa upande wa Mikoa ya Pwani, Serikali kupitia mradi wa usimamizi wa mazingira ya Pwani na Bahari (*MACEMP*), inaendelea kuwasaidia wavuvi kutekeleza azma hiyo kwa kupitia miradi midogo midogo. Hamasa na miradi hii imekuwa ikitekelezwa sambamba na sera ya Taifa ya Uvuvi (1997) inayolenga kuendeleza na kudumisha rasilimali za uvuvi kwa faida ya kizazi hiki na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, katika jimbo la Mchinga miradi mitano (5) ya uvuvi yenye thamani ya shilingi 98,661,475.00 imeanzhishwa na kutekelezwa na imewanufaisha jumla ya wavuvi 110 ikiwa ni wanaume 98 na anawake 12 kuanzia mwaka 2009 mpaka mwaka 2010.

Serikali kupitia mradi huu imetoa zana bora za uvuvi ambazo ni pamoja na boti 5, injini za boti za kupandikiza aina ya YAMAHA TANO (5) zenye nguvu ya farasi (*Horse Power*) 40 kwa kila moja, na nyavu za jarife 50, kwa vijiji vya Kijiweni, Mvuleni A, Mchinga A, Maloo na Mchinga B.

Mheshimiwa Spika, kijiji cha Mchinga Kijiweni pekee kimenufaika kwa kupatiwa mradi wa uvuvi wa nyavu zenye macho zaidi ya inchu tatu, na mradi wenywewe una jumla ya thamani ya shilingi 19,916,160/=.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mhesihmiwa Said Mtanda. Hata kama unaitwa lazima usimame, *so that the Speaker catches your eye.*

**MHE. SAID MOHAMED MTANDA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa kikundi cha Mambo Hadharani *fair play*, Wawili Dawa, Tatu Bila, Tupendane, Mgumia, Radi Tupeleke, *Zola Zola B, B and U* ni mionganoni mwa vikundi ambavyo viliamua kwa hiari yao kusalimisha nyavu haramu kwa Serikali na kwa kuwa maisha ya watu hawa inategemea sana uvuvi na hadi sasa watu hawa wanapata shida kutokana na kutokuwa na shughuli mbadala.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha hawa waweze kurejea katika maisha yao ya kawaida kupitia Bajeti ya Serikali ya mwaka huu na kupitia utekelezaji wa mradi wa *MACEMP* awamu ya pili?

Pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi aliahidi kuwapatia wavuvi hawa baadhi ya vikundi hivi vyta uvuvi mradi wa ng'ombe na mbuzi wa kisasa kutoka Naliendele. Je, ni kwa kiwango gani Serikali imetekeleza ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, moja ya vikundi vilivyowezeshwa katika Jimbo la Mchinga viliwezeshe wa kupitia mradi wa *MACEMP* ambao kwa sasa awamu yake ya kwanza inakamilika mwaka huu na tayari majadiliano yameanza na Benki ya Dunia ili kwenda katika awamu ya pili. Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kadri raslimali zitakavyopatikana katika mradi huu wa *MACEMP* awamu ya pili, vikundi vyote alivyovitaja vitawezeshwa kama hivi vyta kwanza vilivyowezeshwa ili waweze kupata maisha mbadala na jinsi ya kujipatia maisha.

Pili, ahadi iliyotolewa na Serikali ya kuwapatia hawa wapiga kura wa Mheshimiwa Mbunge, ng'ombe na mbuzi wa maziwa. Niseme pia kwamba ahadi hiyo itabaki pale pale. Mheshimiwa Mbunge namwomba aniruhusu nirudi niweze kufuatilia kwamba ahadi yenyewe ilikuwa na sura gani. Lakini pili kuweza kutafuta rasilimali na kuhakikisha kwamba vikundi hivyo pia vinapatiwa mifugo hiyo iliyoahidiwa. (*Makofii*)

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa operesheni hii ya kuchomewa nyavu wavuvi imeshatumika kwa muda mrefu, na kwa kuwa wavuvi hawa huwa hawatengenezi wao nyavu, Serikali haioni umuhimu wa kudhibiti nyavu zinakotengenezwa na zinakouzwa badala ya kuendelea kuwachomea hawa wavuvi nyavu zao? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, katika agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu alilolitoa tarehe 12 Januari, 2010 Wakuu wa Mikoa wote wa Tanzania waliagizwa kwamba wasimamie udhibiti wa nyavu haramu na hili lilielekezwa zaidi kwamba udhibiti huo uwabane waagizaji wa nyavu, watengenezaji wa nyavu, wasambazaji wa nyavu, na watumiaji.

Kwa hiyo, naomba tu nisisitize kwamba agizo na maelekezo yamekuwa wazi kwamba yanawabana wote, watengenezaji pamoja na wasafirishaji na watumiaji wa nyavu hizo.

**Kutunga Sheria ya Uzalishaji wa  
Vyakula Kumlinda Mtumiaji**

**MHE. PINDI H. CHANA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutunga sheria inayomtaka mzalishaji hususan wa vyakula na bidhaa nyingine kumlinda mlaji au mtumiaji wa bidhaa yake?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kuweza kusimama hapa kwanza, nimshukuru sana Mungu kwa baraka zake nyingi. Niwashukuru sana wananchi wapiga kura wa Singida Kaskazini kwa kura nyingi za kishindo kwa Chama Cha Mapinduzi na kwangu, nimshukuru sana kipekee Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wake. Nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa tena. Nikupongeze Mheshimiwa Spika, kwa kuchaguliwa.

Niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wa vyama vyote kwa kuchaguliwa na niwaombe tushirikiane kuisogeza nchi isonge mbele pamoja. Kwa kuwa leo ni siku ya wapendao duniani, kwa mke wangu Faraja na watoto niwatakie sikukuu njema na wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kujibu swalii la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ningependa nimjulishe Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa Sheria ya Ushindani Na. 8 ya mwaka 2003 ilitungwa kwa lengo la kukuza na kulinda ushindani katika biashara na kumlinda mlaji au mtumiaji wa huduma dhidi ya mienendo isiyo halali katika soko.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushindani Na. 8 ya mwaka 2003 inamtaka mzalishaji wa bidhaa (wakiwemo wazalishaji wa vyakula) kuzalisha bidhaa zilizo salama ili kumlinda mlaji.

Vile vile, Sheria hiyo inamtaka kuwa mzalishaji anapokiuka wajibu wake anatenda kosa na mlaji anaweza kudai fidia kama atakuwa amepata madhara kutokana na matumizi ya bidhaa iliyozalishwa na mzalishaji bila kuzingatia masharti ya usalama wa bidhaa husika.

Mwisho, nimpongeze sana Mheshimiwa Pindi Chana, kwa swalii hili na niwapongeze wana Njombe wote kwa Mkoa Mpya waliopata. Ahsanteni sana.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Lakini kama jinsi ulivyotuambia Sheria hii ni ya ushindani ila kipengele cha kumlinda mlaji na kwa tatizo hili la bidhaa ambazo hazikidhi viwango nchini Tanzania ni kubwa ukizingatia madawa ya Kichina, watu wakitungia wanatumia wanapata athari, vyakula vilivyo *expire* Waziri atakubaliana na ombi langu la kuja na Sheria ambayo mchakato wake uanze sasa ambapo kichwa cha Sheria hiyo ni “Kumlinda mtumiaji”. Ahsante. (*Makofî*)

**SPIKA:** Swalii sasa. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Pindi Chana kwamba tatizo la bidhaa ambazo hazina ubora ikiwa ni pamoja na vyakula limekuwepo na kwa wakati tofauti limeweza kuwadhuwalaji. Naomba nisisitize kwamba Sheria ya Ushindani Na. 8 inakidhi matakwa ya aina mbili, kwanza inamlinda mlaji na kutoa nafasi kama mlaji atakuwa amepata kudhuriwa na chakula au bidhaa ya aina fulani aliyoitumia ana haki ya kupata fidia chini ya Sheria hii.

Lakini la pili inamlinda mlaji dhidi ya wafanya biashara ambaao wanaingiza na kuleta bidhaa ambazo hazina ubora ambazo haina kiwango ambacho kinatakiwa chini ya Sheria hii na naomba kusema kwamba Serikali itaendelea kuiangalia kwa makini Sheria hii na kuangalia uwezekano wa kuifanyia marekebisho pale ambapo itaonekana inafaa. (*Makofî*)

Na. 58

### **Ujenzi wa Daraja la Sibiti**

**MHE. SALOME D. MWAMBU** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa kwenye Kampeni za uchaguzi, aliahidi ujenzi wa daraja la Sibiti ambalo linaunganisha Wilaya ya Iramba na Shinyanga mapema iwezekanavyo.

Je, Serikali imefikia hatua gani ya utekelezaji wa ahadi hiyo ya Rais?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga daraja la Sibiti linalounganisha Wilaya ya Iramba na Mkoa wa Shinyanga umeshaanza. Serikali katika Bajeti ya mwaka huu wa fedha 2010/2011, imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.304 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hili.

Tayari usanifu na uandaaji wa nyaraka za Zabuni kwa ajili ya ujenzi umekamilika. Zabuni za ujenzi wa daraja zitatangazwa katika mwaka wa fedha wa 2010/2011. Ni matarajio ya Wizara kuwa Mkandarasi atapatikana na kuanza kazi kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha 2010/2011.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Taarifa za nyuma zinaonekana zabuni ilishatangazwa tangu Agosti mwaka 2009. Je, ni kitu gani kilisababisha utekelezaji wake ukwame?

(ii) Je, Serikali itawaahidi nini Wananchi wa Iramba Mashariki kwa kuwa ile ahadi ya kwanza haikutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni kweli kabisa kwamba, Serikali ilitangaza zabuni ya kwanza ya ujenzi wa Daraja la Sibiti, mwezi Agosti 2009, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge alivyosema. Ninaomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba, zabuni hiyo ya mwaka 2009, haikuitikiwa vizuri na makandarasi wetu nchini; ni kampuni mbili tu zilizo jitokeza na kampuni hizo mbili ndizo zilizorejesha hata makabrasha ya zabuni, lakini yakashindwa kuwa na vigezo vilivyonakiwa katika utekelezaji wa Mradi huu; hivyo, ikaamuliwa mchakato mzima uanze upya. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, mchakato mpya wa zabuni hiyo umeshaanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Iramba Mashariki kuwa, mchakato wa utekelezaji wa Ahadi ya Mheshimiwa Rais, umeshaanza kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi. Wizara yangu itahakikisha kwamba, inashirikiana kwa karibu na Mheshimiwa Mbunge, kufuatilia kwa karibu mchakato mzima. Vilevile nimalizie kwa kumhakikishia zaidi Mheshimiwa Mbunge kuwa, utekelezaji wa Mradi huu safari hii utakuwa bora zaidi kwa sababu utahusisha uboreshaji wa kipande cha barabara chenye urefu wa kilomita 25 kutoka Chemchemi hadi Sibiti, kwa kunyanyua tuta na vilevile kwa kuweka makalavati makubwa.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala hili linafanana kabisa na mazingira ya Wilaya ya Kilombero na Ulanga; na kwa kuwa katika Ahadi za Mheshimiwa Rais mwaka 2005 aliahidi kujenga daraja linalounganisha Wilaya ya Kilombero na Ulanga; napenda sasa kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba; je, Serikali katika ahadi hizo zilizotolewa na Mheshimiwa Rais; ina mpango gani au inaweza ikawathibitishia vipi Wananchi wa Kilombero na Ulanga kwamba daraja hilo litajengwa katika kipindi hiki na ni lini litaanza?

**SPIKA:** Hayafanani kabisa, kule kuna mafuriko. Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu swali hilo na ninadhani unafahamu. Mheshimiwa Naibu Waziri; ni Waziri eeh! Mheshimiwa Waziri, tafadhalii.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, hilo daraja liliahidiwa na Mheshimiwa Rais na kwa bahati nzuri katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2010, kuanzia ukurasa wa 72 – 83, unazungumzia pia kuhusu hilo daraja; na kwamba Daraja la Kilombero *designs* zimeshamalizika na kwa sasa tupo kwenye utaratibu wa kuzitangaza hizo *tender* kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hilo. (*Makofi*)

Na. 59

### **Ujenzi wa Barabara ya Likuyufisi – Mkenda kuelekea Msumbiji**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Ujenzi wa kiwango cha lami wa Barabara ya Likuyufisi – Mkenda kuelekea Msumbiji ni agizo la Rais na upembuzi yakinifu pamoja na upimaji wa barabara hiyo unakaribia kukamilika ikizingatiwa wenzetu upande wa Msumbiji, wamepiga hatua kubwa ya uboreshaji wa barabara hiyo.

Je, Serikali iko tayari kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami kwa awamu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza azma yake ya kujenga kwa kiwango cha lami, Barabara ya Likuyufisi – Mkenda kuelekea Msumbiji, yenye urefu wa kilometra 124, kulingana na agizo la Mheshimiwa Rais. Hivi sasa, Mhandisi Mshauri, *M/S Crowntech Consult Ltd.*, anaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa barabara kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo. Mara kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu itakapokamilika, hatua nytingine ya kutangaza na kuijenga barabara hii kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha utafuata. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuifanya matengenezo ili Barabara ya Likuyufisi – Mkenda iweze kupitika wakati wote.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, niishukuru Serikali, kwa ahadi hiyo.

(i) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Magufuli anafahamu kabisa umuhimu wa agizo la Rais la utengenezaji wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami na ni agizo la muda mrefu; na kwa kuwa masuala ya upembuzi yakinifu na usanifu yamekuwa na tabia ya kuchukua hata miaka 100 wakati mwengine; je, Serikali sasa iko tayari kuniambia huo upembuzi yakinifu, usanifu na upatikanaji wa fedha ni lini vitakuwa vimeshaambatana sambamba kwa mpango kazi na kutuarifu Wananchi wa Jimbo la Peramiho ili tuweze kujua agizo hilo la Rais linatekelezeka?

(ii) Kwa kuwa barabara hii ni kiungo kikubwa sana cha mahusiano kati ya Watanzania na Wananchi wa Msumbiji katika urafiki wetu na maendeleo ya Mkoa wa Ruvuma na Jimbo la Peramiho. Je, Serikali inafahamu kwamba hata sasa bado yapo maeneo korofi ambayo hayapitiki na ipo tayari kuendelea kushirikiana na Wakala wa Barabara wa Mkoa kuhakikisha hilo lililotolewa hapa mbele kama ahadi ya kupitika mwaka wote linaweza kutekelezeka na kweli ikapitika mwaka wote?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wizara yangu imetoa kipaumbele cha juu kabisa kwa Mradi huu kutokana na agizo hilo la Mheshimiwa Rais. Kwa kawaida, Mradi kama huu wa Barabara ungeanza na upembvuzi yakinifu ukikamilika ndiyo tuingie kwenye usanifu ambao ni *detail design*. Kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, kazi zote mbili tumemkabidhi Mhandisi Mshauri, *Crowntech*, lengo ni kuharakisha mchakato huu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kuwa, ujenzi wa barabara za lami unahitaji maandalizi ya muda mrefu na ya kina na masuala ya kitaalamu. Kwa kweli kama nilivyosema, Serikali itaendelea kuifanyia matengenezo Barabara ya Likuyusifu – Mkunda kwenda Msumbiji ili ipitike. Kwa taarifa tu ni kwamba, katika mwaka huu wa fedha, Serikali imetenga shilingi 665,863,000 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo.

Na. 60

**Kuboresha Miundombinu ya Mifereji kwa ajili ya  
Kilimo cha Tangawizi – Same**

**MHE. ANNE K. MALECEL A** liuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Same Mashariki wamejitalidi kwa nguvu zao kujenga kiwanda cha kusindika tangawizi; hatua hiyo ya kuongeza thamani ya tangawizi kwa wakulima itachochea na kupanua kilimo cha tangawizi ambacho huhitaji matumizi ya maji kwa wingi:-

Je, Serikali itachukua hatua gani madhubuti ili kupanua na kuboresha miundombinu ya mifereji ili kukidhi mahitaji yatokanayo na upanuzi wa kilimo hicho?

### **NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua juhudzi za Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Wananchi wa Same Mashariki, kuendeleza Zao la Tangawizi. Katika kufuatilia juhudzi za Wananchi hao, tarehe 31 Januari, 2011, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, alifanya ziara ya kukagua maendeleo ya kilimo katika Wilaya ya Same, ambayo ilijumuisha ukaguzi wa mashamba ya tangawizi, kiwanda cha kusindika tangawizi na Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji wa Ndungu. Kwa kutambua juhudzi za wakulima, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

(a) Wizara yangu imemwagiza Mhandisi wa Umwagiliaji wa Kanda ya Kilimanjaro kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Same, kuangalia uwezekano wa kupata vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na kujenga mabwawa madogo maarufu kama "Ndiva" kule Upareni, ujenzi wa bwawa la Kambani kwenye Mto Yongoma litakalokidhi mahitaji ya kilimo cha umwagiliaji katika Vijiji vya Lugulu, Kanza na Vumba na Vijiji vya Kitugwa, Kambeni, Goha, Nyamba, Sambweni na Kilongwe katika Kata ya Mpini na Myamba.

(b) Katika mwaka 2010/2011, Serikali imetenga shilingi milioni 56 katika Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya ya Same (*DADPS*), kwa ajili ya ukarabati wa mifereji katika Kijiji cha Sambweni. Serikali itaendelea kutenga fedha za kuboresha mifereji ya umwagiliaji kupitia *DADPS* ili kukidhi mahitaji ya kilimo cha tangawizi.

Mheshimiwa Spika, kipekee, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Wananchi wa Jimbo la Same Mashariki, kwa uibuaji wa Mradi wa Kusindika Tangawizi, kwa sababu usindikaji huo utaongeza ubora wa Zao la Tangawizi na kuwaongezea wakulima uhakika wa soko na kipato.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kushukuru halafu niulize maswali mawili ya nyongeza. Kabla sijaauliza swali, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri mno, ambayo sikuwa nimeyategemea kusema kweli. Pia nimshukuru kwa roho yake nzuri ya upendo aliyoionesha mara baada ya kuteuliwa, akaamua kutembelea kule Milimani Same Mashariki na kuona kama kweli tumejenga Kiwanda cha Tangawizi na siyo kibanda cha kuku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa Same Mashariki kuna Kata kumi za Milimani ambazo zote zina uwezo wa kulima tangawizi kwa wingi sana lakini tatizo kubwa ni kwamba kuna matatizo ya barabara na vijibarabara ambavyo vitawawezesha Wananchi kutoa tangawizi kutoka mashambani kufikisha kwenye kile kiwanda. Je, Serikali haioni kuna uharaka kwa sababu kiwanda sasa hivi karibu kinaanza kazi na kuna umuhimu wa kuboresha barabara na vijibarabara ili Wananchi waweze kupeleka kwa urahisi tangawizi pale kwenye kiwanda kuliko ambavyo sasa wanabeba kwa vichwa vyao?

(ii) Kwa kuwa nina Kata mbili za Tambarare; Kata ya Ndungu na Kata ya Kalemau, ambazo nazo zina eneo kubwa sana linaloweza kulimwa tangawizi; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, alikuja akaona Mradi wangu wa Umwagiliaji wa Ndungu kwamba sasa hivi hauna hali nzuri; na kwa kuwa sasa ni muhimu watujengee Bwawa la Ndungu ili tuweze kulima tangawizi katika hizi Kata mbili: Je, Mheshimiwa Waziri anasema nini kuhusu Mradi wangu wa Umwagiliaji wa Kata ya Ndungu?

**SPIKA:** Suala ni barabara na bwawa tu. Hebu naomba ujibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nilipoutembelea Mradi ule, niligundua kwamba, wamefanya kazi kubwa. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, tangawizi ni nzito na hivyo Wananchi hawawezi kubeba kichwani mazao yale kutoka shambani kwenda sokoni. Kwa hiyo, sambamba na kuagiza wataalamu kuandaa Mradi kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji; kwanza ya kusafisha tangawizi na pili ya kumwagilia tangawizi; nimewaagiza pia kuweka makadirio ya kujenga barabara za kutoa mazao mashambani kwenda sokoni (*farm to market roads*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa Bwawa hili analolisema la Ndungu, ni mkubwa sana. Tuli-design tangu mwaka 1984 kwa dola milioni 14 wakati ule dola ilipokuwa ni shilingi 12 tu. Kwa hiyo, sasa hivi tunavyozidi kuchelewa, naona tunazidi kuingiza gharama kubwa. Litakapo jengwa Bwawa hili, litakuwa na uwezo wa kuongeza hekta zingine 1,000 zaidi ya zinazolimwa sasa hivi. Kwa kweli, naona umuhimu na nitawaagiza wataalamu waangalie na waliweke katika mpango wa maendeleo. (*Makofi*)

Na. 61

**Kufufua Kituo Kidogo cha Utafiti wa Mbegu Suluti – Uyole**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya pembejeo za kilimo zikiwemo na mbegu bora, lakini Wakulima wa Mkoa wa Ruvuma hususan wa Wilaya ya Namtumbo, wamekuwa wakitilia shaka mbegu wanazopata kwa sababu haziendani na hali ya hewa ya Mkoa wa Ruvuma na hivyo kupata mavuno hafifu:-

Je, Serikali haioni ni vema kukifufua kile kituo kidogo cha utafiti wa mbegu kilichopo kwenye Kijiji cha Suluti kilichojudikana kama Kituo Kidogo Uyole ili kiweze kupanda Mahindi ya Mbegu kwa ajili ya Mkoa huo kikisaidiana na Shamba la JKT Mlale?

#### **NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo na Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo Kidogo cha Suluti bado ni mojawapo ya vituo vidogo vilivyo chini ya Taasisi ya Utafiti Kilimo Uyole. Uyole ni Makao Makuu ya Utafiti, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini. Moja ya majukumu ya utafiti katika Kanda hiyo ni kufanya utafiti na kugundua aina mpya za mbegu za mazao zeny ukinzani dhidi ya wadudu, magonjwa, zinazozaa sana na zinazokidhi mahitaji ya walaji na soko. Kituo Kidogo cha Suluti kinatumika kwa shughuli za utafiti kwa mazao ya maharagwe, soya, alizeti, mahindi na mihogo kwa ajili ya kuzalisha mbegu zitakazofaa kwa hali ya hewa ya Mkoa wa Ruvuma na sehemu ya Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Spika, baada ya vituo vya utafiti kugundua mbegu bora, vinawajibika kuzalisha mbegu mama na kuipatia Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA), ambayo ina jukumu la kuizalisha mbegu hiyo na kupata mbegu za msingi na zilizothibitishwa kwa ajili ya kuzipatia kampuni za mbegu na kuwauzia wakulima. Pamoja na kukitumia Kituo Kidogo cha Utafiti cha Suluti katika kufanya utafiti, Wizara yangu imeandaa mpango wa kujitosheleza kwa mbegu bora hapa nchini. Katika mkakati huo, makubaliano yamefikiwa kati ya ASA na ARI Uyole, kutumia mashamba ya kituo cha Suluti kuzalisha mbegu mama kwa ajili ya kusambazwa kwa wazalishaji mbegu bora (*Certified Seed*) kwa matumizi ya wakulima. Hatua hii itasaidia sana katika kufikia azma ya Taifa ya kujitosheleza kwa mbegu bora.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa wakulima katika Wilaya ya Namtumbo hawatumii mbegu ambazo haziendani na hali ya hewa ya wilaya hiyo; ni vema Halmashauri ya Wilaya kuititia mipango yake, ikatenga maeneo ya mashamba makubwa kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora kwa matumizi ya Wilaya, Mkoa na eneo la Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kutumia fursa hii tena, kumpongeza Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, kwa juhudu kubwa anazoendelea kufanya kuboresha kilimo katika Jimbo lake la Namtumbo.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na ya ufasaha.

(i) Kwa kuwa katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika amesema makubaliano yamefikiwa kati ya ASA na ARI Uyole kutumia mashamba ya Kituo cha Suluti kuzalisha mbegu mama lakini kituo kile kinahitaji kukarabatiwa miundombinu yake pamoja na kutengenezwa pia miundombinu ya umwagiliaji. Je, Wizara inaweza kukiweka kituo kile katika bajeti yake mwaka huu wa 2011/2012?

(ii) Kwa kuwa kituo kile ni muhimu sana katika Kanda ile na pia katika kutekeleza kipaumbele cha nne cha Rais cha Kilimo na Mifugo. Je, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana anaweza kuja kukitembelea Kituo kile na kuona uhalisia wake ili akipe kipaumbele katika Bajeti hii ya 2011/2012?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa kwamba, mkakati wetu katika Wizara ya Kilimo ni kuhakikisha kwamba, tunaongeza uzalishaji wa mbegu hapa ndani ili kupunguza utegemezi wa mbegu kutoka nje. Na katika mikakati, baadhi ya mikakati tuliyonayo ni mingi; mambo ambayo tutayafanya ni kuboresha majengo katika vituo vyetu vyote ikiwa ni pamoja na Suluti. Kuvipa vituo zana za kilimo kama matrekta na inapowezekana hata *combine harvesters* na kuweka miundombinu ya umwagiliaji kuhakikisha kwamba, mbegu haikauki wakati inaoteshwa. Tunataka pia kuhamasisha sekta binafsi kutusaidia kuongeza uzalishaji wa mbegu maana mpaka sasa hivi uzalishaji bado upo chini sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kukitembelea kituo hicho, ninataka nimhakikishie kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, atafanya ziara katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, atakapokuwa kule amenihakikishia kwamba atapita Kituo cha Suluti kuona jinsi kinavyoendelea.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na kwamba katika kutekeleza azma ya Kilimo Kwanza mbegu zinahitajika sana lakini pia pembejeo; sasa kwa vile Wakulima wa Mkoa wa Ruvuma wamepata mahangaiko makubwa ya kupata pembejeo; je, hali hiyo imesababishwa na kitu gani na Serikali itafanya nini ili kukomesha hali hii na ili Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma waliozoea kulima waweze kulima na ku-supply chakula katika nchi nzima kama kawaida yao?

**SPIKA:** Kwa pembejeo unamaanisha mbolea?

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Ushirika, napenda nijibu swali la Mheshimiwa Devota M. Likokola, kwa kifupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake ni pana sana lakini nadhani kama nimemwelewa na kwa uzoefu wangu, baada ya kuzungukia nchi hii nadhani anataka kujikita kwenye usambazaji wa mbolea na kwenye matumizi ya *voucher* kama nimemwelewa maana yake yapo mambo mengi; lakini nataka nimhakikishie kwamba, upo upungufu ambao umejitokeza kwenye utaratibu huu wa *voucher* tumeuona; wapo mawakala ambao siyo waaminifu; na wapo hata wafanyakazi ambao hawakuwa waaminifu. Tunachosisitiza tu ni kwamba, upungufu wote ambao umejitokeza, tunaendelea kuufanya kazi na hivi tunavyozungumza, wataalam wako nje wanafanya kazi ili tuhakikishe kwamba, utaratibu wa usambazaji wa mbolea hizi zenyetruku hasa unaofuata tuweze kuuboreshe na kuondoa matatizo waliyoyapata Wananchi wa Ruvuma na si Ruvuma, tunadhani ni mikoa mingi ambayo imekumbwa na tatizo hili. Mimi nasema poleni sana, lakini tutajitahidi kuondoa hivi vikwazo katika msimu ujao.

Na. 62

#### **Kuhamisha Jenereta Mbili kutoka Ikwiriri kwenda Liwale**

**MHE. FAITH M. MITAMBO** aliuliza:-

Ni muda mrefu Serikali iliahidi kuupatia Mji wa Liwale umeme wa uhakika na Serikali ilishaainisha kupeleka jenereta mbili zenyetruku hasa ukubwa wa KW 800 kutoka Ikwiriri kwenda Liwale:-

Je, ni lini mpango huo wa kuhamisha jenereta utakamilika?

#### **WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faith M. Mitambo, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, Serikali iliahidi kuupatia Mji wa Liwale umeme wa uhakika kwa kufunga jenereta mbili kutoka Ikwiriri, zenyetruku hasa ukubwa wa KW 800 kutoka Ikwiriri. Kufuatia kukamilika zoezi la uwekaji waya wa umeme kupita Daraja la Mkapa, Mji wa Ikwiriri ulitarajiwa kuanza kupata umeme kutoka katika Kituo cha Kufua Umeme cha Somanga Fungu mwishoni mwa mwezi huu wa Februari, 2011.

Kwa juhudini kubwa zilizofanywa na wataalam wetu kupitia Shirika la TANESCO, ninayo furaha kuwaarifu Wananchi wa Liwale kwamba, tayari mashine hizo au Kituo cha Ikwiriri kinapata umeme unaotokana na gesi ya asili kutoka Somanga Fungu. Mashine za

Ikwiriri zilizokuwa zinatumia diseli zimezimwa hivi sasa na sasa wataalam wetu wapo Liwale wakiangalia eneo ambapo mashine hizo zitafungwa.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kuhamisha jenereta hizo utaanza mara moja baada ya wataalam wetu kukamilisha zoezi la kubaini wapi zinastahili kufungwa katika Mji wa Makao Makuu ya Wilaya ya Liwale.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, ningeomba kuuliza swali la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa mpango wa kuhamisha jenereta hizo ulikuwa ufanyike mara baada ya uwashaji wa mashine zilizoko katika Kituo cha SONGAS cha Somanga kukamilika; na kwa kuwa mashine hizo zimekwishawashwa sasa na Mji wa Ikwiriri na Vitongoji vyake vinatumia SONGAS; je, Mheshimiwa Waziri wa Nishati unaweza kusema ni lini jenereta hizo zitafikishwa Mjini Liwale?

(b) Kwa kuwa tatizo la umeme wa uhakika kwa Mji wa Liwale limekuwa ni la muda mrefu; na kwa kuwa Wilaya ya Liwale iko karibu na Wilaya ya Nachingwea ambayo tayari imekwishaunganishwa kwenye Mradi wa Mnazi Bay; ni kwa nini Serikali isiiunganishe Wilaya hii katika Mradi wa Mnazi Bay kutokea Nachingwea ili Wilaya hii sasa iweze kupata umeme wa uhakika?

**SPIKA:** Humu ndani (a) na (b) ni maswali mawili.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Faith Mitambo, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Ushauri tulioopata kwa wataalam ni kwamba, zoezi la kuhamisha mashine zile mbili zilizokuwa Ikwiriri ambazo zimezimwa, limeweza kuchukua takriban miezi mitatu, kwa sababu wanahitaji kuzifungua zote kuziweka katika vipande vipande ili ziweze kusafirishwa kwa urahisi bila kuathirika. Kwa hiyo, tunatarajia baada ya miezi mitatu ama minne, zoezi hilo litakuwa limekamilika, lakini namuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuko pamoja hapa, tutakuwa tukimpa taarifa za maendeleo ya utekelezaji wa Mradi huu kama tulivyokusudia.

La pili, kuhusu kuipatia Wilaya ya Liwale umeme wa uhakika unaotokana na gesi asilia, inayozalishwa eneo la Msimbati Mnazi Bay kule Mtwara, hiyo ndiyo dhamira ya Serikali kama ilivyo katika maeneo mengine ya nchi hii, lakini pia tunazingatia tofauti na uhalisia wa jiografia katika maeneo husika. Jiografia ya Wilaya ya Liwale, sote tunaifahamu na Mheshimiwa Faith Mitambo atakubaliana na mimi kwamba, umbali ulioko kutoka Wilaya ya Nachingwea na hata Masasi kwa ujumla kuufikisha pale utachukua muda mrefu. Dhamira yetu ni kuhakikisha kwamba, hatimaye Mji wa Liwale nao kwa sababu ndiyo Wilaya pekee iliyobaki katika Mkoa wa Lindi, ambayo haipati umeme wa uhakika wa kutumia gesi ya asili kwa sababu Kilwa wanatumia gesi ya asili

ya Songo Songo; kwa hiyo, mipango tunayo na tunahakikisha kwamba, kadiri muda unavyokwenda, tutazidi kuwaarifu Watanzania kuwafikishia huduma hiyo ya uhakika.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini mchakato wa majenereta ya Mji wa Kibondo na Mji wa Kasulu utakamilika na Watu wa Kasulu na Kibondo kupata umeme?

**SPIKA:** Umemsikia, haya naomba ujibu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Zitto, kama ifuatavyo:-

Habari njema zilizopo ni kwamba, ufungaji wa jenereta hizo umeshakamilika na sasa hivi tunakamilisha kufunga miundombinu kwa ajili ya kusambaza umeme, lakini majenereta tayari yameshafungwa na Mheshimiwa Zitto anafahamu vizuri sana na Mkoa wa Kigoma wanatambua hilo na *Ishallah* wiki ijayo ama mwanzoni kabisa mwa mwezi wa tatu, Wananchi wataanza kupata huduma kama ilivyokusudiwa.

**SPIKA:** Haya basi, habari hii ni njema inafurahiwa na sisi wote.

Na. 63

### **Miradi ya Umeme Kutoka Mgodi wa Kahama Kwenda Nyang'hwale**

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR** aliuliza:-

Moja ya ahadi alizozitoa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Jimboni Nyang'hwale, tarehe 26 Oktoba, 2010 wakati wa ziara ya kampeni ni kuleta umeme Jimboni Nyang'hwale kutoka Mgodi wa Kahama:-

- (a) Je, Mradi huo utaanza lini?
- (b) Je, ni Kata ngapi zitakazofaidika na Mradi huo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Jimbo la Nyang'hwale ni miongoni mwa maeneo yatakayofaidika na Mradi unaofadhiliwa na Mfuko wa *Millenium Challenge Account* kuititia Mradi unaojulika kama *Millennium Challenge Cooperation* kutoka Marekani. Utekelezaji wa Mradi huu tayari umeshaanza, zoezi la uthamini wa mali za Wananchi watakaoathirika na Mradi huu hasa kupisha ujenzi wa miundombinu ya kupeleka umeme katika maeneo husika tayari umeshafanyika na taratibu za malipo ya fidia zinaendelea na

zinatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2011, kama ambavyo tumekuwa tukitoa taarifa kupidia Bunge lako Tukufu. Vilevile mkandarasi wa Ujenzi wa Mradi huo ameshapatikana, ambaye ni *Symbion Power LLC* na kwa sasa anaendelea na zoezi la upimaji wa njia za umeme (*Detailed Survey*).

(b) Mheshimiwa Spika, Kata zitakazofaidika na Mradi huo katika Jimbo la Nyang'hwale ni Kata ya Karumwa katika Kijiji cha Msalala, Kata ya Nyijundu kwenye Kijiji cha Nyarubere na Kata ya Nyang'hwale katika Kijiji cha Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, naendelea kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais ya kupeleka umeme Jimboni Nyang'hwale kama alivyoahidi katika maeneo mengine, itaendelea kutekelezwa kama ilivyokusudiwa.

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri; nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa ahadi hii ya Serikali imekuwa ni ya kujirudia rudia mnamo mwaka 2007 yalifanyika maandamano ya kudai umeme na maji katika Jimbo la Nyang'hwale, kwa sababu umeme huo umepita ndani ya Mji wa Kalumwa kuelekea mgodini na pia umeme huo umepita tena njia nyingine kwenda Ziwa la Viktoria, Wananchi waliandamana kudai umeme; Naibu Waziri alikuja mwaka 2008 na kuwatuliza Wananchi na kuahidi kwamba 2009 umeme utawashwa; je, kwa kauli hii ya leo unawahakikishia vipi ama Serikali inawahakikishia vipi Wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale kwamba kauli hii ni ya uhakika na ni sahihi ili Wananchi waweze kuwa na imani na Serikali yao?

(ii) kipindi kile cha 2009 yalionekana malori ya TANESCO yakiranda randa kwa kuwahadaa Wananchi; je, Wananchi safari hii watakuwa na imani ipi kwa ahadi hii ya Mheshimiwa Waziri? Ahsante.

**SPIKA:** Ulijuaje kama yanarandaranda.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunachokisema hapa ndicho tunachokitekeleza, tumekuwa tukitoa taarifa kupidia Bunge lako Tufuku, utekelezaji wa miradi ya namna hiyo unachukua muda mrefu, una hatua za kuanzia kwenye makaratasi kwa wakati huo unakuwa unasema utekelezaji umeanza. Ninafahamu kiu ya Wananchi ni kuona ni wakati gani sasa hasa mitambo ama miundombinu katika maeneo husika; nimekuwa nikisema na ninarudia kusema kwamba, utekelezaji wa Miradi hiyo unaendelea na kauli hii ninayoisema ni kwa niaba ya mikoa yote sita, ambayo itafaidika na Miradi ya MCC wakiwemo Wananchi wa Jimbo na Wilaya ya Sengerema, pamoja na kwingineko katika ile mikoa sita.

Kuhusu malori aliyojasema mimi nipo jirani na Mheshimiwa Amar, majimbo yetu yanapakana na ni rafiki yangu wa karibu, sikuwahi kusikia habari hizo hata mara moja za kuona malori yanaranda randa lakini yawezekana kama yalikuwa ni magari ya TANESCO, basi yalikuwa yanashirikiana na wafadhili wa Mradi katika kufanya tathmini ya njia ambako umeme utapita, lakini hatuna sababu nyingine ya kuamini kwamba, urandarandaji wa malori hayo ulikuwa na dhamira nyingine zaidi ya utekelezaji ya Mradi huo.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Jimbo la Mbozi Magharibi lina Kata kumi nne, lakini ni Kata moja tu kati ya Kata hizo kumi nne ambayo ni Tarafa ama Halmashauri ya Mji wa Tunduma ndiyo yenye umeme; je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Kata nyingine kumi na tatu zilizobakia zinasambaziwa umeme?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Silinde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika na Watanzania kwa ujumla, sote tunafahamu nchi yetu ina mahitaji mengi, utekelezaji wa Miradi yetu tunaufanya kupitia vipaumbele ambavyo tunakuwa tumekubaliana na hasa kupitia bajeti zetu za Wizara za Fedha, ambazo zinawekwa katika Wizara husika. Kwa vipaumbele ambavyo tumejiwekea kama Taifa, tunatekeleza Miradi kwanza. Awali tulikubaliana tuanze na kuwaunganisha Makao Makuu ya Mikoa yote kupata huduma za umeme na hatimaye tutafika katika Makao Makuu ya Wilaya. Maeneo ya Kata ni bahati kwamba, wapo wanaofuatisila kutohakana na uasili wa njia za kupitisha umeme, unaopelekwa katika Makao Makuu ya Wilaya. Kwa hakika, dhamira yetu kwa sasa ni kumaliza kwanza Makao Makuu ya Wilaya zote, zoezi ambalo litakamilika kwenye mwaka huu wa fedha, kwa sababu wilaya zote pamoja na hizi mpya ambazo zimetangazwa hivi karibuni, tunaziingiza kwenye bajeti ijayo.

Kwa wilaya ambazo mpaka kufikia mwaka jana tulikuwa tunazitambua, zoezi la kuzifikishia umeme Makao Makuu ya hizo wilaya, linakamilika katika bajeti ya fedha hii ambayo inaishia tarehe 30 Juni, 2011. Kwa hiyo, Mheshimiwa Silendi na Waheshimiwa Wabunge wengine katika maeneo ya Kata, ninaendelea kuwashakikishia kwamba, tukishakamilisha zoezi hilo, vipaumbele vinavyofuata ni maeneo ambayo yana shughuli nyingi za kiuchumi na zina matokeo makubwa katika uchumi wetu na hasa taasisi maalum kama shule, makanisa, misikiti pamoja na shughuli zingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa Kata, tutaendelea kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge, kwa kadiri mahitaji ya kila Jimbo yanavyokuwa na uwezo wa rasilimali fedha unaopatikana ndani ya Serikali.

Na. 64

#### **Ada kwa Shule za Msingi na Sekondari**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Kwa muda sasa Serikali imekuwa ikiwatangazia Watanzania kwamba Elimu ya Msingi itatolewa bure, hali kadhalika Elimu ya Sekondari kwa mtoto anayefaulu kwenda shule za Serikali kwa shule za kutwa ada itakuwa ni shilingi 20,000 na shule za bweni ni shilingi 70,000:-

Je, Serikali inasema nini juu ya kauli hii?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, ada kwa Shule za Sekondari ni shilingi 20,000 kwa shule za kutwa na shilingi 70,000 kwa shule za bweni. Viwango hivi vimewekwa kwa mujibu wa Waraka Na. 11 wa Mwaka 2004 ili kuwapunguzia Wananchi mzigo wa kulipa ada.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya Msingi, elimu hiyo itaendelea kutolewa bure hadi mwanafunzi atakapomaliza darasa la saba ambalo ni kikomo cha elimu ya msingi ambayo ni ya lazima. Hata hivyo, baadhi ya shule nchini zimekuwa zikitoza michango mbalimbali ya kuendeleza shule husika baada ya kupata ridhaa ya Kamati za Shule kwa Shule za Msingi na Bodi za Shule kwa Shule za Sekondari.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikijinasibu kwamba elimu ya msingi ni bure, lakini ukweli umedhihirika kwamba sio bure kwa sababu wazazi wanapokwenda kuandikisha watoto wao na hili pia limetokea katika Jimbo langu la Kawe, hawaruhuswi kuandikishwa mpaka wawe na kiasi fulani cha fedha:-

(i) Je, Serikali haiioni kwamba huu ni wakati muafaka wa kuwaambia Watanzania ukweli ili wazazi wajiandae kifedha kulipia watoto wakati wanapoandikishwa?

(ii) Kwa kuwa sasa imethibitika elimu ya msingi siyo bure kama inavyosemekana na siyo shilingi 20,000 na shilingi 70,000 kama ambavyo inasemekana; je, Serikali iko tayari sasa kuwaambia Wazazi na Watanzania kwa ujumla ni kiasi ambacho kinatakiwa kitozwe katika shule za msingi na kiasi gani ambacho kinatakiwa kitozwe katika shule za sekondari za kutwa na bweni ili Kamati za Shule zisitumie wigo huo kupata fedha bila utaratibu? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa majibu mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wa Jimbo la Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, labda mimi niseme hivi; kwa Wabunge wenzangu na Wananchi wote kwa ujumla kwamba, kuna utofauti wa michango na kuna utofauti wa aina za shule. Kwa hiyo, Ofisi ya Kamishna huwa inatoa kibali, inaziruhusu zile Kamati za shule husika kuanza kuwatoza wazazi michango kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya shule husika. Kama ambavyo tumesema kwamba, shule za Wananchi ni shule zetu, lazima vilevile na wazazi wachangie kwa kuendeleza maendeleo ya shule.

Vilevile kuna mfumo maalum ambao unatumika, tayari kwa mfano kama upande wa shule za sekondari, kuna kitu kinaitwa *captation grands* ambayo ni shilingi 25,000; shilingi 12,500 inatumika kwa ajili ya vifaa vya kujifunzia na kufundishia na shilingi 15,000 nyingine inayobaki kwa ajili ya uendeshaji wa shule kwa matengenezo ya magari, ukarabati mdogo mdogo; semina, safari, utawala na dharura. Kwa hiyo; Kamati hizi za shule zina mamlaka kabisa kwa ajili ya kuwatangazia wazazi ili watoto waweze kuchangia michango mingine ya ziada.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ningependa kuuliza swali. Kwa kuwa katika Jimbo hili hili la Kawe kuna Shule kadhaa za Kata zenyenye wanafunzi wengi sana na bahati mbaya pamoja na uchache wa Walimu na madarasa pia ni machache na tunaishukuru Serikali kwa kutoa elimu ambayo kusema kweli ni karibu na bure kabisa. (*Makofi*)

Je, Serikali itakuwa tayari kuchangia kidogo tu kwa shule za binafsi na mimi ni mmojawapo nikiwa mdau ili waweze kuwachukua hao watoto wenyewe vipaji maalum kutoka Shule za Kata na kuwaleta katika shule hizi za binafsi ili waweze kuboresha au kukuza elimu yao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mlaki, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuna baadhi ya shule za binafsi ambazo Serikali huwa inazipa ruzuku, lakini mpaka ziwe zimefuata vigezo ambavyo vimewekwa na Serikali hasa katika utozaji wa ada, kwa sababu kuna utozaji wa ada holela, lakini kama wakifuata masharti, kwa mfano, kama ni shule za kutwa ni shilingi 250,000; wakishafuata masharti hayo, sisi Wizara ya Elimu hatuna matatizo kwa ajili ya kuzipa grants.

Na. 65

### **Sifa za Walimu Wanaofundisha Elimu ya Msingi Hapa Nchini**

**MHE. RACHEL M. ROBERT** aliuliza:-

Inasemekana kuwa asilimia 50.3 ya Walimu wa Shule za Msingi hapa nchini hawana sifa kwa sababu elimu yao ni chini ya Daraja A hali inayochangia kushuka kwa kiwango cha elimu hasa kwenye masomo ya Hisabati na Sayansi; na wakati huo huo Serikali imeweka mpango wa kuwapatia mafunzo Walimu 29,292 wenyewe Daraja B na C ili wafikie Daraja LA III A:-

(a) Je, kwa nini Serikali isiwasaki Walimu wa Daraja la III A kuongeza elimu yao kufikia Diploma au Stashahada ili wawe na uwezo mkubwa wa kufundisha?

(b) Kwa nini Serikali isiongeze idadi ya wale wanaoomba kujiunga na vyuo ili kuondoa kabisa Daraja la III A kwa kuzingatia karne hii ya kuongezeka kwa sayansi na teknolojia kunakohitaji mbinu mpya za kufundisha na matumizi ya teknolojia ya kisasa?

(c) Je, Serikali inasema nini juu ya vijana waliohitimu Shahada na Vyeti takriban 16,000 walioripotiwa kuwa wapo mtaani hadi Desemba, 2010 kwa kutoajiriwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b), na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikail imeweka utaratibu wa Walimu kuomba kujiunga na Vyuo vya Ualimu kwa ngazi ya Stashahada kila mwaka. Hata hivyo, nafasi za Vyuo vya Stashahada huwa hazijai kutokana na kukosa wanafunzi wenyе sifa, mfano, wanafunzi wengi wanaomaliza Kidato cha Sita hudahiliwa katika Vyuo Vikuu na Vyuo vingine. Aidha, ili MWalimu aweze kusoma Stashahada ya Ualimu, lazima awe amefaulu Mtihani wa Kidato cha Sita.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2010/2011, kati ya wahitimu 17,684 waliofaulu masomo yao, wahitimu 8,857 walitoka kazini, yaani *in service*; jumla ya wahitimu 9,226 ndiyo walioajiriwa na Serikali wakiwemo wahitimu 4,920 wenyе shahada na wahitimu 4,306 wenyе stashahada.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Elimu, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ya Naibu Waziri yazingatie maswali yangu.

(i) Kwa kuwa wapo Walimu wengi waliomaliza miaka ya nyuma na Serikali inatambua kuwa sasa hivi kuna uhaba wa Walimu: Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ajira nyingi kwa Walimu hao hasa katika Mkoa wa Shinyanga ambao umekuwa nyuma sana kielimu?

(ii) Kwa kuwa Serikali imekuwa na utaratibu wa kuwaajiri Walimu waliofeli masomo yao ya ziada na kuwaelekeza wakarudie hayo masomo wakiwa chuoni. Je, Serikali inasema nini sasa kuhusu wanachuo ambao wako sasa hivi chuoni?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya dada yangu, Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwanza, napenda tu nimhakikishie kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, iko makini sana; Walimu wote waliohitimu mwaka huu wa fedha 2010/2011 na wamefaulu, ninataka kumhakikishia kwamba, wote walajiriwa. Ila sasa kwa swali hilo lingine kwamba, kuna vijana ambao bado wako mitaani na walihitimu miaka ya nyuma; mimi nataka tu kutoa rai kwa Wabunge wenzangu na Wananchi wote kwa ujumla kwamba, kama kuna mWalimu yuko mitaani na hajaajiriwa na anaomba sasa kuja kuajiriwa, tunawakaribisha kwa sababu Serikali inahitaji sana Walimu kwa ajili ya kukidhi haja ya Walimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna hawa Walimu ambao miaka ya nyuma walikuwa wakiajiriwa lakini wanakuwa na *supplementary* kwenye vyuo; sasa ilikuwa wakienda huko walikuwa hawarudi ku-*clear* masomo yao wanakaa mpaka miaka saba au hata kumi, mwaka huu tukaona hapana, kwa sababu kiwango cha Elimu chenyewe kama mnavyoona matokeo ya Kidato cha Nne; tumeona tuweke *stop*, waende Walimu waliofaulu lakini hawa ambao tayari wana *supplementary* tumesema, watarudia mitihani yao. Ninataka niwatangazie Walimu popote wanaponisikia kwamba, tarehe 4 Aprili waende kwenye vyuo vyao kwa ajili ya ku-*clear* masomo yao ili wakisha-*clear*, tuwajumuushe pamoja na Walimu ambao tutawaajiri mwaka huu kwa ajili ya kuwaajiri wote kwa pamoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri, lakini nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imetua tamko kwamba Walimu wanaotakiwa kurudia masomo ya Stashahada wanatakiwa kwenda kufanya hivyo tarehe 4 Aprili; na kwa kuwa tangazo hili limetoka kipindi ambacho walishatoka kwenye maeneo yao ya vyuo; na kwa kuwa Waraka uliokuwa unealekeza kubadili huu utaratibu haukufika mapema vyuoni; na kwa kuwa wanatakiwa kulipia ada za hayo masomo wanayotakiwa kujiandaa; je, Serikali iko tayari vilevile kutoa muda mwingine wa ziada Walimu hao waweze kurudia masomo yao kutokana na uhaba wa Walimu ambo tuko nao sasa hivi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la mdogo wangu, Mheshimiwa John J. Mnyika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, hao Walimu kwanza wanafahamu na tayari tulishapeleka matangazo baada tu ya kuwatangazia zile ajira. Ninataka niseme tu kwamba, ikiwa kuna MWalimu anaona hajajiandaa kufanya hii mitihani, yeye anaweza akawasubiria tu mwaka mwingine, lakini Walimu kwa sababu najua wamejiandaa na yale masomo wanakwenda kufanya kama *supplementary*, tunawaomba waje wafanye mitihani ili waweze kuajiriwa kipindi hiki, maana wasipokuja kufanya mitihani hawataajiriwa tena mpaka mwaka mwingine na mambo mengine yanaweza yakabadilika kwa sababu sasa hivi au hata mwaka kesho Walimu watahitimu wengi sana. Tumepandisha hadhi vyuo vingine viwe vinafundisha *Faculty of Education* kama Dodoma wanafunzi ni wengi, MUSE Mkwawa na pale Chuo cha Chang'ombe (*DUCE*), kwa hiyo, tuna hakika mwaka

kesho tutapata Walimu wengi sana; kwa hiyo, wakizembea wasipofanya mitihani mwaka huu, watakuja tena kuachwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Na. 66

### **Wakaguzi wa Shule Nchini**

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA** aliuliza:-

Sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 imeweka uhalali wa kisheria kuwepo kwa Wakaguzi wa Shule ambako kumetoa fursa ya shule kukaguliwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa shule zinaendeshwa kwa kuzingatia taratibu na kanuni zinazotawala Sheria ya Elimu iliyotajwa. Je, Serikali inasema nini juu ya Wakaguzi wa Shule kukaa ofisini bila kazi kwa kukosa fedha za uendeshaji, vifaa vya ofisi na majengo ya kufanyia kazi, magari na kadhalika huku elimu ikiendelea kushuka kila mwaka hasa katika Mkoa wa Shinyanga ambaa umekuwa wa mwisho kwenye matokeo ya Mtihani wa Darasa la Saba katika Mwaka 2010?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ukaguzi wa Shule inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Hata hivyo, Serikali imeendelea na jithada za kuhakikisha kuwa, Wakaguzi wa Shule wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Katika kipindi cha mwaka 2006 hadi 2010, Serikali ilifanya mambo yafuatavyo: Magari 89 kwa ajili ya Ofisi za Ukaguzi wa Shule yalinunuliwa; Ofisi 50 za Ukaguzi wa Shule za Wilaya na Kanda zilikarabatiwa; Kompyuta 100 na vifaa vingine vya ofisi vilinunuliwa; na Bajeti ya Ukaguzi wa Shule imeongezeka. Aidha, Mkoa wa Shinyanga wenye mahitaji ya magari manane una magari matano; hivyo, Wizara yangu itaendelea na zoezi la ununuzi wa magari ili kuhakikisha kuwa, Ofisi za Ukaguzi wa Shule katika Kanda na Halmashauri zote zinapata magari.

Mheshimiwa Spika, katika kuleta ufanisi wa ukaguzi wa shule, Idara imeanzisha utaratibu wa ukaguzi wa shule kwa kuzingatia makundi ya ubora ambapo shule zilizo chini ya kiwango zitakaguliwa mara nyingi zaidi ili kuinua kiwango cha ubora. Vilevile Wizara katika utaratibu wake wa kuimarisha ukaguzi wa shule, imeandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Shule kwa lengo la kuwawezesha Walimu Wakuu na Waratibu Elimu Kata kama Wakaguzi wa Ndani na wa karibu wa shule, kusimamia shule ili ziweze kujilettea maendeleo kwa kuzipatia msaada endelevu wa kaitaalumu na kitaaluma.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako mazuri.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema katika majibu yake Serikali itaendelea kutoa magari kwenye Kanda na kwenye Halmashauri kwa ajili ya kuweza kuinua kiwango cha ukaguzi na kuboresha ukaguzi wa shule katika Mkoa wa Shinyanga; na kwa kuwa Wilaya ya Meatu katika Mkoa wa Shinyanga imeweza kuwa ya mwisho katika matokeo ya Mtihani wa Darasa la Saba; Waziri atakubaliana na mimi kuwa kati ya haya magari ambayo Serikali imesema inayatoa katika Halmashauri zetu, Wilaya ya Meatu ipewe kipaumbele cha kupata gari hilo ili kazi ya ukaguzi iweze kufanyika kwa ufanisi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba, Mpango wa Wizara ya Elimu katika mwaka huu wa fedha ni kununua magari 19 ambayo katika kuyasambaza, tutaangalia mgawo kwa sehemu ambazo zina mazingira magumu. Sasa kama Wilaya ya Meatu tutaiangalia kama ni mionganini mwa Wilaya ambazo zina mazingira magumu, Mheshimiwa Opulukwa, nadhani utapata gari hilo.

Vilevile suala la Mkoa wa Shinyanga kuwa ni Mkoa wa mwisho kitaaluma; na mimi nataka niungane na wewe kwamba, katika takwimu zetu pale Wizarani, inaonekana Mkoa wa Shinyanga karibu takriban miaka mitatu mfululizo, umekuwa ni Mkoa wa mwisho kitaaluma. Mimi nadhani *DEOs* na *REOs* wangeshirikiana ili waweze kutafuta mbinu mbadala kujua kwa nini Mikoa mingine wanaweza kufanya vizuri na Mkoa wa Shinyanga usiweze kufanya vizuri. Hata hivyo, miaka ya nyuma, Mkoa wa Rukwa nao ulikuwa na matatizo kama Mkoa wa Shinyanga; ni vizuri Wabunge wa Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Rukwa mkaangalia mbinu mbadala kwa kuweka zile *good entertainments* kwa *teachers*, ambazo wenzeni waliweza kuziweka mpaka Walimu wanakwenda Rukwa na wanakaa kule. Kwa hiyo, hata Mkoa wa Shinyanga kwa sababu tatizo kubwa ni Walimu, basi ni vizuri mkashirikiana mtafute mazingira mazuri ya kuweza kuwatunza hao Walimu ili waweze kukaa katika Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana na muda wa maswali umekwisha na leo nina kazi kubwa zaidi ...

## **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu gani na tumemaliza maswali?

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Spika, tumemaliza ndiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhusu utaratibu katika masuala mawili kwa kutumia Kanuni ya 68. La kwanza, linahusiana na lugha ambayo Wabunge tunaizungumza au Mawaziri wanapojobu maswali imekuwa sasa ni utamaduni Mawaziri au Naibu Mawaziri kusema dada yangu au mdogo wangu na kadhalika; na Kanuni zinatamka kwamba, tuwatambulisse Wabunge ama kwa vyeo vyao au kwa majina yao kamili.

Mheshimiwa Spika, naomba hili Wabunge ama Mawaziri tunapokuwa tunazungumza, tuweze kuyazingatia kwa sababu siyo Lugha ya Kibunge.

La pili, nadhani ni Kanuni ya 61, ambayo inazungumzia kuhusu kuzungumzia jambo lenye maslahi ambapo, kwa mfano, wakati Mheshimiwa Rita Mlaki anauliza swali lake amesema yeye ni mdau wa shule binafsi; sasa sifahamu kama anamiliki shule binafsi au hapana, lakini aliuliza swali ambalo linapelekea Serikali kusaidia shule binafsi?

Kwa hiyo, nadhani kwa mujibu wa taratibu zetu, tunapaswa kutokuzungumzia jambo lenye maslahi au kutaja maslahi yanayohusika. Vilevile wakati wa swali linalohusiana nadhani na Kiwanda cha Tangawizi kule Same, sifahamu kama Mheshimiwa Anne K. Malecela ana maslahi binafsi kwenye kiwanda, lakini ni vizuri tunapozungumza masuala kama haya ndani ya Bunge, tuweze kutangaza maslahi yetu au kusema kwamba ni namna gani ambavyo unahuksika na suala hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa haya naomba uweze kuyakazia ili shughuli zetu ziweze kwenda vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto yuko sahihi. Kwanza kabisa ile ya kuitana dada yangu, rafiki yangu na kadhalika, Mawaziri wataitwa kwa vyeo vyao na Wabunge wataitwa kwa majina yao; hiyo ni Kanuni.

Lingine, wakati wa maswali Waheshimiwa Mawaziri hamuwezi kupongeza, kusalimu na kadhalika, muda ni dakika tano tu kwa swali la msingi na la nyongeza. Kwa hiyo, naomba sana, kama tunavyosema, Bunge la Kwanza wengi ni wapya wanaendelea kujifunza. Kwa hiyo, hilo nalo tulizingatie kwa sababu mkianza kuwasalimia watu na kuwashukuru na kadhalika, basi tutashindwa kujibu maswali.

Leo hii niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, hata wale waliozoea kujibu maswali kwa kirefu kwa kuandika, leo wamekuja na nusu *page*; kwa kweli wamefanya vizuri sana na ndiyo maana tumefika pazuri, lakini kasoro iko kwenye maswali ya nyongeza mnatuhutubia badala ya kuuliza maswali ya nyongeza, matokeo yake hatutoi nafasi kwa maswali ya nyongeza zaidi kwa sababu maswali ya nyongeza ni marefu, Mawaziri wameanza kujisahihisha, wao wana matatizo wakijibu majibu ya nyongeza watazunguka sana. Nadhani tutaendelea kujifunza. (*Makofî*)

Kuhusu maslahi, nayo pia ni sahihi; Kanuni ya 61, kama mtu ana maslahi binafsi inabidi atangaze. Ninaamini Kiwanda cha Tangawizi kile siyo chake binafsi ni cha Wananchi, nina mashaka na swali la Mheshimiwa Mlaki; kwa hiyo kama ni hivyo, anapaswa mtu atangaze maslahi aliyonayo kwenye suala analolizungumza hapa. Kwa hiyo, hilo ni sahihi na ninaomba tulizingatie.

Waheshimiwa Wabunge, nimepata maoni ya Mheshimiwa Mbunge mwingine kwamba, viti vile vya nyuma hawaonekani kwenye macho ya Spika, kwa hiyo, hata wakisimama kwa maswali ya nyongeza siwaoni; ni kweli tumekubaliana kwamba, vile viti vya nyuma tulivyooangeza vitapandishwa kidogo ili viwe juu zaidi kuliko mstari wa mwisho na hivyo hivyo viti vile vya mwisho havina vipaza sauti, lakini Bunge lijalo tutakuwa navyo. Kwa hiyo, kuna maandalizi yanafanyika na kwa sasa hivi naomba mpate tabu kidogo, mtusamehe tutatengeneza.

Kama tulivyokubaliana kutangaza wageni, tukitangaza kila mtu hapa dakika 20 zitatoka na mimi leo nina matatizo ya muda, kwa hiyo, natangaza wageni wafuatao:-

Tuna Mheshimiwa Dkt. Willibrod P. Slaa, Katibu Mkuu wa CHADEMA na ninyi wote mniamfahamu, alikuwa Mbunge mwenzetu hapa. Alikuwa Mbunge makini sana na alikuwa Mbunge wa SADC kwa kipindi chote, tunaku-*miss* kule SADC sasa hivi; ahsante sana na karibu. (*Makofi*)

Pia kuna wanafunzi 50 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara Dar es Salaam; naomba wote wasimame popote walipo. Karibuni sana, ninyi ni jirani zetu na karibuni tuendelee kushirikiana. (*Makofi*)

Tuna wageni wanaongozwa na Meya wa Jiji la Mwanza ni Madiwani; wote wasimame walipo, hao ni Madiwani nafikiri ni wa CHADEMA.

Halafu Mheshimiwa Dkt. Willibrod P. Slaa, ameongozana nafikiri na Sekretarieti yake; naomba pia wasimame. (*Makofi*)

Baada ya kusema hivyo, tunaendelea na kazi za kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, leo tunategemea kufanya uchaguzi wa Tume kipindi cha jioni, yaani saa kumi na moja jioni. Uchaguzi wa Tume tutaufanya hapa ndani, kutakuwa na kuwahoji wale walioomba kugombea nafasi hiyo na kupiga kura.

Tumebadilisha saa kwenda saa 11 kwa sababu asubuhi hii nina kauli nyingi; Kambi ya Upinzani watakuwa na kauli yao halafu na Mheshimiwa Waziri wa Maji ana kauli; kwa hiyo, naona muda mwingi utakuwa umetumika kwa ajili hiyo.

Matangazo ya kazi; Mheshimiwa Peter Serukamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa,

kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo leo tarehe 14, saa saba mchana katika Ukumbi Namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mashirika ya Umma, Mheshimiwa Kabwe Zitto, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma kuwa, leo tarehe 14 kuanzia saa saba mchana watakuwa na kikao katika Jengo la Utawala, Ukumbi Namba 227.

Mwenyekiti wa Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuwa, kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo leo saa tano asubuhi katika Ukumbi Namba 219, ghorofa ya pili.

Mheshimiwa Katibu wa Caucus ya Chama cha Mapinduzi, anaomba niwatangazie Wajumbe wake wa Chama cha Mapinduzi kwamba, Kamati ya Uongozi wanakutana saa tano halafu saa saba Wabunge wa Caucus wanakutana Ukumbi wa Msekwa; hao wengine Kamati ya Uongozi wanakutana kwenye *Board Room* ya Spika, saa tano ni Kamati ya Uongozi halafu na saa saba Wanachama wote.

Baada ya kusema hivyo, naomba tuendelee na shughuli zinazofuata.

## **KAULI ZA MAWAZIRI**

### **Kauli Kuhusu Utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini**

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, Kanuni Na. 49, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu Utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza mipango mbalimbali kwa lengo la kuwapatia Wananchi huduma ya maji. Programu ya Maji Vijijini ya Miaka 20 ya 1971-1991, iliyohusu utekelezaji wa Miradi ya Maji iliyojengwa na Serikali. Serikali ilikuwa ikibuni Miradi na kuisanifu, kuitekeleza na kuiendesha.

Tathmini ya Sera ya Maji ya Mwaka 1991 ambayo ilifanyika mwaka 1997, ilibaini kuwa Miradi ya Maji ingekuwa endelevu iwapo tu Wananchi wangeshiriki katika kuibua, kujenga na kuendesha Miradi hiyo. Miongoni mwa misingi muhimu ya Sera ya Maji ya Mwaka 2002 ni pamoja na ushirikishaji wa Wananchi vijijini katika Miradi ya Maji kuititia Halmashauri zao na vyombo vyaya watumiaji maji.

Msingi mwingine muhimu wa Sera ya Maji ya 2002 ni utekelezaji wa azma ya Serikali ya kurudisha madaraka kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa Sera ya Maji, Serikali imeandaa Mpango wa Kitaifa wa Kuendeleza Sekta ya Maji. Vilevile, Serikali imeandaa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ya miaka 20 ya 2006-2025.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji imegawanywa katika awamu nne za vipindi vya miaka mitano, ambapo awamu ya kwanza ni kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 hadi mwaka 2011/2012. Programu hiyo kuu ina programu nne ambazo zinahusu: (i) usimamizi wa rasilimali za maji; (ii) huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini; (iii) huduma za maji na uondoaji wa majitaka mijini; na (iv) uimarishaji na kujenga uwezo wa taasisi zenye majukumu muhimu katika Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuandaa Programu, Serikali ilikubaliana na Washirika wa Maendeleo wa Sekta ya Maji mambo yafuatayo kuhusu Miradi ya Maji itakayotekelawa kwa fedha watakazotoa:-

- (i) Taratibu za Manunuzi za Benki ya Dunia zitumike katika manunuzi yenye gharama kubwa na ya kimataifa;
- (ii) Taratibu za manunuzi za Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004 zitumike kwa manunuzi ya kitaifa;
- (iii) Fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini zitumwe na Wizara ya Fedha moja kwa moja kwenye mafungu ya Mikoa na Halmashauri bila kupitia Wizara ya Maji; na
- (iv) Halmashauri ziwasilishe taarifa za utekelezaji na matumizi ya fedha kila robo mwaka kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, Chimbuko la Programu ya sasa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ni Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, ambao ulianza kutekelezwa mwaka 2002 kwa mkopo nafuu wa Dola za Kimarekani milioni 26 kutoka Benki ya Dunia na mchango wa Serikali na Wananchi wa Dola milioni 1.7. Utekelezaji ulianza katika Wilaya tatu za Mpwapwa, Kilosa na Rufiji kama majoribio ya utekelezaji wa Sera ya Maji ya Mwaka 2002.

Mwaka 2004, mradi uliendelezwa katika Wilaya nyingine tisa za Handeni, Igunga, Iramba, Kiteto, Kondoa, Kongwa, Manyoni, Morogoro, na Singida. Wilaya ziliongezeka kuwa 14 baada ya Wilaya za Handeni na Morogoro kugawanywa na kuanzisha Wilaya Mpya za Kilindi na Mvomero, sawia.

Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ulifikia ukomo mwezi Juni, 2008. Kuanzia mwaka 2008/2009, Miradi iliyoanzishwa chini ya Mradi huo imekamilishwa au kuendelezwa chini ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ambayo ni sehemu ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini katika Wilaya 14, hususan katika manunuzi na usimamizi unaofanywa na Halmashauri kwa wataalam washauri na wakandarasi, umetumika katika kufanikisha maandalizi na utekelezaji wa Programu ya sasa.

Tangu mwaka 2007/08, Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, imejielekeza katika kutekeleza Miradi inayoleta matokeo ya haraka, Miradi Mikubwa ya Maji Vijijini (vijiji 10 katika kila Halmashauri) na Miradi mingine inayotekelawa na wadau mbalimbali katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, majukumu ya taasisi zinazohusika ni kama ifuatavyo:-

Serikali za Mitaa: Halmashauri zinapanga na kutekeleza Miradi katika wilaya kwa kuwatumia wataalam washauri na wakandarasi, chini ya mikataba ambayo Halmashauri zenyewe zimeingia na wataalam washauri na wakandarasi.

Sekretarieti za Mkoa: Sekretarieti za Mkoa zinafutilia na kusimamia utekelezaji katika ngazi ya wilaya.

Ngazi ya Taifa: Wizara ya Maji inaandaa miongozo na kuratibu Programu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Washirika wa Maendeleo. Wizara ya Maji hufutilia upatikanaji wa fedha kutoka Hazina na Washirika wa Maendeleo na kwamba fedha zinazopatikana zinatumika kulingana na mipango ya utekelezaji ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa Wataalam Washauri kwa ajili ya Miradi ya Vijiji kumi; naomba nitoe maelezo yanayohusu taratibu za manunuzi kuhusiana na utekelezaji wa miradi ya maji kwenye vijiji kumi katika kila Halmashauri.

Juhudi za Halmashauri kuajiri wataalam washauri wa kusanifu Miradi ya Maji Vijijini zilianza mwaka 2005 kwa kutumia taratibu za manunuzi za Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004. Ilipofika mwaka 2007, washirika wetu katika kutekeleza programu waliamua kwamba taratibu za manunuzi za Benki ya Dunia zitumike. Ilibidi zoezi la kutafuta wataalam washauri lienze upya.

Mwezi Novemba 2007, Serikali ilitoa mafunzo kwa Maafisa wa Halmashauri zote nchini kuhusu taratibu za manunuzi za Benki ya Dunia. Baada ya mafunzo hayo, Halmashauri zote zilianza zoezi la kufanya tathmini za kampuni za wataalam washauri zilizoonesha nia ya kusanifu Miradi ya Maji.

Mheshimiwa Spika, wakati taratibu za kuwapata wataalam washauri zinaendelea, Serikali ilianza kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kwa kujenga na kukarabati miradi midogo yenye kuleta matokeo ya haraka (*Quick Wins*).

Halmashauri zilitekeleza Miradi hiyo Julai 2007 hadi Juni 2009. Awamu hii ya utekelezaji wa Programu ilihu pia na kuzijengea uwezo wa kiufundi na kiofisi; Halmashauri zote, Sekretariati za mikoa na Wizara ya Maji.

Hadi mwezi Desemba 2010, jumla ya Miradi ya Maji 4,134 yenyе vituo vya kuchotea maji 9,824 ilikuwa imejengwa au kufanyiwa ukarabati, ambapo watu wapatao 2,594,350 walikuwa wananaufaika na huduma ya maji. Vilevile, ofisi 54 za Idara ya Maji za Halmashauri zilikuwa zimekarabatiwa na nyingine mpya 67 kujengwa. Ofisi mbili za Sekretarieti ya Mikoa ya Shinyanga na Tabora pia zilikuwa zimekarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Miradi ya Maji katika vijiji kumi katika kila Halmashauri, hadi Januari 2011, Halmashauri 124 kati ya Halmashauri 132, tayari zimeajiri wataalam washauri. Hii ni baada ya Halmashauri hizo kukamilisha taratibu zote za manunuzi na kupata ridhaa ya Benki ya Dunia. Wataalam hao wanafanya upimaji, usanifu wa miradi, kuandaa makabrasha ya zabuni na watasimamia ujenzi wa miundombinu ya maji itakapoanza kujengwa.

Mheshimiwa Spika, idadi ya Halmashauri ambazo zimeajiri wataalam washauri kwa kila mkoa ni kama ifuatavyo: Arusha 6; Dar es Salaam 3; Dodoma 6; Iringa 8; Kagera 8; Kigoma 2; Kilimanjaro 6; Lindi 6; Manyara 4; Mara 5; Mbeya 8; Morogoro 3; Mtwara 6; Mwanza 7; Pwani 7; Rukwa 5; Ruvuma 5; Shinyanga 6; Singida 3; Tabora 6; na Tanga 9. Orodha ya Halmashauri hizi iko kwenye Jedwali Na. 1.

Kwa Halmashauri sita za Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Kibondo, Kilosa, Morogoro, Manispaa ya Morogoro na Bariadi, kampuni zilizoshinda gharama zake za kufanya kazi zilikuwa juu kuliko kiwango kinachokubalika. Halmashauri hizo zilirudia zoezi hili kwa kuandaa orodha fupi (*short list*) ya wataalam washauri. Halmashauri hizo sasa zimepata ridhaa ya Benki ya Dunia ya kufungua mapendekezo ya kifedha na kufanya majadiliano na wataalam washauri waliopata alama za juu. Kati ya hizo, Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Kibondo, Kilosa na Bariadi zimekamilisha kazi hiyo na rasimu za mikataba zimepelekwa Benki ya Dunia ili kupata ridhaa ya kusaini mikataba. Morogoro na Manispaa ya Morogoro wanaendelea na mchakato wa tathmini ya kifedha, kuandaa rasimu ya mkataba na kufanya majadiliano na mtaalam mshauri.

Manispaa ya Singida haikupata ridhaa ya Benki ya Dunia kumwajiri mtaalam mshauri kwa kuwa kampuni iliyoidhinishwa siyo kampuni ya ushauri katika kazi za kiufundi (*consultancy firm*), bali ni Shirika lisilokuwa la Kiserikali (*NGO*). Halmashauri hiyo imeandaa orodha fupi ya washauri na tayari imefanya majadiliano na aliyeshinda. Ridhaa ya Benki ya Dunia itatolewa baada ya muda mfupi.

Halmashauri ya Simanjiro nayo ilirudia kutangaza lakini hakuna wataalam washauri waliojitokeza. Orodha fupi ya wataalam washauri iliandaliwa kwa utaratibu maalum na kutumwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata ridhaa. Halmashauri imepata kibali cha Benki ya Dunia cha kufungua mapendekezo ya kifedha na kufanya majadiliano na mtaalam mshauri ambaye amepata alama za juu.

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma itatekeleza Miradi ya Vijiji vyake kupitia Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Manispaa ya Musoma, ikiwa ni pamoja na kutumia mtaalam mshauri wa Mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inafuatilia kwa karibu upatikanaji wa ridhaa kutoka Benki ya Dunia ili kuharakisha upatikanaji wa wataalam washauri kwa ajili ya Halmashauri nane zilizobaki kwa lengo la wataalam hao kupatikana kabla ya mwisho wa mwezi Machi, 2011. Jedwali Na. 1 linaonesha hatua iliyofikiwa na Halmashauri mbalimbali katika kupata wataalam washauri hadi mwisho wa Januari 2011.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ambazo zimesaini mikataba baina yake na wataalam washauri, wataalam hao wanaendelea na kazi zifuatazo: utafiti na upimaji wa vyanzo vya maji; usanifu wa Miradi ya Maji; uhamasishaji wa jamii kuhusu usafi wa mazingira; uhamasishaji kuhusu uundaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji; na uandaaji wa zabuni za uchimbaji wa visima na ujenzi wa miundombinu ya maji. Hadi kufikia tarehe 31 Januari 2011, utekelezaji ulikuwa umefikia katika hatua mbalimbali, ambaeo upo katika makundi tisa.

Kundi la kwanza ni Halmashauri kumi ambazo wataalam washauri wanaandaa taarifa za awali na kuainisha kazi zitakazofanyika (*scoping study*). Halmashauri hizi ni Manispaa ya Temeke, Jiji la Mbeya, Kiteto, Rarya, Manispaa ya Bukoba, Kasulu, Sumbawanga, Mbinga, Handeni na Jiji la Tanga.

Kundi la pili ni la Halmashauri tatu ambazo wataalam washauri wametayarisha zabuni ili zitangazwe kupata wakandarasi watakaochimba visima vya maji. Halmashauri hizo ni Manispaa ya Ilala, Mvomero na Kisarawe.

Kundi la tatu ni la Halmashauri nne ambazo zimetangaza zabuni za kupata wakandarasi watakaochimba visima vya maji. Halmashauri hizo ni Manispaa ya Kinondoni, Manispaa ya Moshi, Manispaa ya Songea na Tabora/Uyui.

Kundi la nne ni la Halmashauri saba ambazo zimetangaza zabuni za kupata wakandarasi watakaochimba visima na zimefanya tathmini ya kupata wakandarasi. Halmashauri hizo ni Kondoa, Karagwe, Ngara, Rombo, Musoma, Tarime na Mbozi.

Kundi la tano ni la Halmashauri tano ambazo zimepata kibali cha kusaini mikataba baina yao na wakandarasi wa uchimbaji wa visima lakini bado wanafanya mawasiliano na wakandarasi kwa ajili ya kusaini mikataba. Halmashauri hizo tano ni Arusha, Manispaa ya Dodoma, Misenyi, Muheza na Mji wa Korogwe.

Kundi la sita ni la Halmashauri 58 ambazo zimeajiri wakandarasi wa kuchimba visima na tayari wakandarasi wameanza kazi. Idadi ya Halmashauri hizo kwa kila mkoa ni kama ifuatavyo: Arusha 3, Dodoma 3, Iringa 3, Kagera 4, Kilimanjaro 3, Kigoma 1, Lindi 1, Mara 1, Manyara 1, Mbeya 3, Morogoro 2, Mtwara 2, Mwanza 6, Pwani 4, Rukwa 3, Ruvuma 3, Shinyanga 4, Singida 1, Tabora 5, na Tanga 5. Orodha ya Halmashauri hizi iko katika Jedwali Na. 3.

Kundi la saba ni la Halmashauri 25 ambazo zimekamilisha uchimbaji wa visima vya maji. Halmashauri hizo 25 ni Manispaa ya Arusha, Longido, Monduli, Chamwino, Kilwa, Mji wa Lindi, Liwale, Nachingwea, Ruangwa, Hanang', Mbulu, Serengeti, Kibaha, Mji wa Kibaha, Ileje, Mbeya, Masasi, Mtwara, Nanyumbu, Newala, Iramba, Singida, Bukombe, Shinyanga na Manispaa ya Shinyanga.

Kundi la nane ni la Halmashauri mbili ambazo wataalam washauri wamefanya usanifu wa Miradi ya Maji ya Mtiririko na kuandaa zabuni kwa ajili ya kutafuta wakandarasi wa kujenga miundombinu ya maji. Zabuni hizo zitatangazwa baada ya muda mfupi. Halmashauri hizo ni Hai na Babati.

Kundi la tisa ni la Halmashauri sita ambazo wataalam washauri wamefanya usanifu wa Miradi ya Maji ya Mtiririko na kuandaa taarifa za usanifu pamoja na zabuni kwa ajili ya kutafuta wakandarasi wa kujenga miundombinu ya maji. Halmashauri hizi ni Kilolo, Ludewa, Makete, Mji wa Njombe, Njombe na Mji wa Mpanda. Zabuni hizo zitatangazwa mwezi Machi 2011. Jedwali Na. 2 linaonesha hatua za utekelezaji zilizofikiwa na wataalam washauri hadi kufikia mwisho wa mwezi Januari 2011.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchimbaji wa visima vya maji; usanifu uliofanywa na wataalam washauri unaonesha kuwa Wananchi kwenye vijiji vingi katika Miradi ya Vijiji wamechagua visima kama vyanzo vya kuwapatia maji. Hii inatokana na jiolojia, haidrojiolojia na haidrolojia maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Jedwali Na. 3 linaonesha kampuni za wakandarasi zilizoajiriwa na Halmashauri kwa ajili ya uchimbaji wa visima. Jedwali Na. 4 linaonesha idadi ya visima vilivyocheinba katika Halmashauri 25. Jumla ya visima 285 vimechimbwa. Kati ya hivyo visima 214 vina maji (75%).

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata wakandarasi wa uchimbaji wa visima na kuanza kazi ya uchimbaji, ujenzi wa miundombinu ya maji unategemewa kuanza 2010/2011. Ujenzi wa miundombinu ya maji unazingatia hatua iliyofikiwa na wataalam washauri katika upimaji, usanifu wa miradi na maandalizi ya zabuni kwa ajili ya kupata wakandarasi wa ujenzi wa miradi. Ujenzi utakuwa kwa awamu kuzingatia upatikanaji wa fedha. Wizara yangu inazishauri Halmashauri kuhakikisha kuwa wakandarasi wanakamilisha kazi zilizopangwa kulingana na mikataba yao.

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza (2007/2008 – 2011/2012) ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, fedha zilizoahidiwa na Washirika wa Maendeleo pamoja na Serikali ni Dola za Kimarekani milioni 951. Kati ya hizo, kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ni Dola za Kimarekani milioni 290. Dola za Kimarekani milioni 180 ni kutoka kwenye Mfuko wa Pamoja (*Basket Fund*) na Dola za Kimarekani milioni 110 ni kwa ajili ya Miradi Maalum (*Earmarked Projects*).

Mheshimiwa Spika, kati ya Dola za Kimarekani milioni 180 za Mfuko wa Pamoja zilizoahidiwa, kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 106, sawa na shilingi bilioni 138.1, zimetumika katika kutekeleza miradi inayoleta matokeo ya haraka, kugharimia wataalam

washauri na uchimbaji wa visima na kuanza ujenzi wa miundombinu katika baadhi ya Halmashauri. Jedwali Na.5 linaonesha mgao wa fedha kwa kila Halmashauri kuanzia Juni 2007 hadi Desemba, 2010.

Kwa awamu ya kwanza mpaka 2011/2012, fedha zilizobaki katika Mfuko wa Pamoja ni Dola za Kimarekani milioni 99. Kiasi hicho kinatuwezesha kuendelea na ujenzi wa miundombinu katika baadhi ya vijiji. Tunaandaa awamu ya pili ya programu ambapo tutahitaji Dola za Marekani milioni 262 ili kukamilisha vijiji vitakavyobakia. Jedwali Na. 6 linaonesha fedha zilizobaki kama zilivytengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika kila Halmashauri. Kiasi cha fedha kilichotengwa kimezingatia kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini, idadi ya watu na teknolojia inayotumika.

Katika kuhakikisha kuwa uendeshaji na usimamiaji wa Miradi ya Maji unafanyika ipasavyo; ni lazima kuunda vyombo vya watumiaji maji na kuvisajili kwa mujibu wa sheria. Aina ya vyombo vya watumiaji maji ambavyo tayari vimeundwa na kusajiliwa na idadi yake hadi mwezi Desemba 2010 ni kama ifuatavyo: Jumuiya za Watumiaji Maji 594; Arusha (52), Iringa (20), Mbeya (7), Dodoma (59), Ruvuma (12), Kilimanjaro (17), Kagera (25), Shinyanga (34), Lindi (8), Morogoro (39), Tabora (19), Manyara (57), Mara (85), Singida (52), Kigoma (13), Dar es Salaam (53), Pwani (14), Tanga (18) na Mtwara (10); kuna Kampuni 18 za Morogoro (17) na Kilimanjaro (1); Udhamini (*Registered Trustees*) 15 za Kilimanjaro (11), Mtwara (Mbuo) (1), Dodoma (Kibaigwa) (1), Arusha (1) na Manyara (1) na Corporation Sole 1 ya Mtwara (Masasi).

Kulingana na takwimu hizo ni dhahiri kwamba, Halmashauri hazijafanya juhudzi za kutosha kuhamasisha uundaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji. Hali hii inachangia kwa kiasi kikubwa, kwa baadhi ya miradi kutofanya kazi na juhudzi zetu kutokuwa endelevu.

Kamati za Maji zilizopo ni ngazi tu ya muda ya kuelekea kwenye uundaji wa vyombo huru vya watumiaji maji vilivyosajiliwa kisheria kwenye Halmashauri. Halmashauri na Wananchi wasiishie kwenye uundaji wa Kamati za Maji za Vijiji ambazo ni sehemu ya Serikali za Vijiji.

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto zilizopo kwenye utoaji wa huduma ya maji vijijini ni uwezo mdogo katika ngazi za Halmashauri na Sekretarieti za Mkoa katika kutekeleza na kusimamia miradi ya maji.

Katika kuziwezesha Halmashauri na Sekretarieti za Mkoa kutekeleza majukumu yao, Wizara yangu iliagiza nyenzo za kufanya kazi. Hadi kufikia mwezi Desemba 2010, Halmashauri ziliwa zimepata magari 108, pikipiki 252, *printer* 124, kompyuta 111 na *scanner* 116. Taratibu zinaendelea ili kupata magari 15 yaliyoagizwa kwa ajili ya Halmashauri zilizobaki. Sekretarieti za Mkoa zimepata magari 21, *printer* 20, kompyuta 21 na *scanner* 20. Katika awamu ya pili ya Programu, Serikali itazingatia upatikanaji wa magari kwa ajili ya Halmashauri mpya na mikoa mipy.

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya Halmashauri, magari ya Programu ya Maji yanatumiwa kinyume na ilivyopangwa. TAMISEMI tayari imetoa maelezo, Halmashauri hizo zinatakiwa ziheshimu taratibu za manunuzi ya vifaa vya programu ya maji ikiwa ni pamoja na matumizi ya magari hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kuzijengea uwezo Halmashauri, mwezi Novemba 2006, Serikali iliajiri wahandisi wa maji 96 na kuwapangia vituo vya kazi kwenye Halmashauri mbalimbali na Sekretarieti za Mikoa ambazo ziliwu hazina wahandisi. Zoezi hili lilifanyika kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na Sekta ya Maji kwa ujumla. Hadi kufikia mwezi Januari 2011, kati ya wahandisi hao, 73 wanaendelea na kazi katika vituo vyao kwenye Halmashauri (62), Sekretarieti za Mkoa (8), na Miradi ya Maji ya Kitaifa (3).

Halmashauri zote bado zina uhaba wa wataalam katika fani mbalimbali. Serikali itaendelea na juhudzi za kuongeza idadi ya wahandisi wa maji na mafundi sanifu ili kukabiliana na uhaba huo. Serikali ina mpango wa kuajiri wahandisi wapya 132 ili kila Halmashauri iweze kuwa na angalau wahandisi wawili. Pia, kuna mpango wa kuhamisha mafundi sanifu 198 ambao hapo awali walikuwa kwenye ofisi za maji za mkoa na baadaye kuhamishiwa kwenye ofisi za maji za mabonde na kuwapeleka kwenye Halmashauri mbalimbali.

Mipango hiyo itatekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2011/2012. Serikali itaongeza idadi ya wataalam wa maji katika Sekretarieti za Mkoa ili kuzipa uwezo wa kufuatilia utekelezaji wa Programu kwenye Halmashauri zilizo katika mikoa yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba, Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini inaendelea kutekelezwa. Utafiti wa vyanzo na usanifu wa miradi, uchimbaji wa visima na utayarishaji wa zabuni kwa ajili ya kupata wakandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya maji uko katika hatua mbalimbali.

Serikali inafuatilia kwa karibu upimaji na usanifu na utekelezaji wa miradi katika vijiji vyote kumi ambavyo vimechaguliwa na kila Halmashauri. Halmashauri mpya zitakazoanzishwa zitawekwa katika Mpango wa Awamu ya Pili ya Programu. Halmashauri na Sekretarieti za Mkoa zinawajibika kuwasimamia kikamilifu wataalam washauri katika kazi zao ikiwa ni pamoja na kuandaa zabuni za ujenzi na vilevile usimamizi wa ujenzi wa Miradi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2010/2011, Serikali imetenga fedha za kuanza ujenzi wa miundombinu ya maji kwenye kila Halmashauri. Mgao wa fedha kwa Halmashauri umezingatia idadi ya watu ambao hawajapata huduma ya maji na aina ya teknolojia itakayotumika. Halmashauri zinatakiwa kuanza ujenzi wa miundombinu kwa awamu, kuzingatia vipaumbele vya Halmashauri na fedha walizotengewa. Serikali itaendelea kutoa fedha kadiri zitakavyopatikana hadi kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika vijiji vyote kumi kwa kila Halmashauri. Fedha zitatolewa kulingana

na jinsi taarifa za utekelezaji wa miradi na matumizi ya fedha za kila robo mwaka zitakavyowasilishwa na Halmashauri. Halmashauri zitakazochelewa kuwasilisha taarifa au kuwasilisha taarifa ambazo hazina ubora, zitachelewa kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuwasiliana na Washirika wa Maendeleo ili fedha za kutosha zinapatikane kwa ajili ya ujenzi wa Miradi katika vijiji vyote kumi kwa kila Halmashauri. Alipofungua rasmi Bunge lako Tukufu tarehe 18 Novemba, 2010, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema:

*“... Tumedhamiria kulitatua tatizo hili kwa kuongeza mgao wa fedha za bajeti kwa ajili ya huduma za maji. Nilishaagiza kwamba, tufanye kila tuwezalo ili Bajeti ya Sekta ya Maji iongezwe kwa kiasi kikubwa kuanzia mwaka ujao wa fedha.”*

Serikali inawahakikishia Wananchi na Waheshimiwa Wabunge kwamba, Miradi yote katika vijiji kumi kwa kila Halmashauri itatekelezwa hatua kwa hatua hadi itakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, Kauli hii ina majedwali sita. Kwa ukamilifu na kuweka rekodi sawa, naomba majedwali yasomeke katika *Hansard* kama sehemu ya Kauli hii.

Napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wananchi, Taasisi za Kiserikali na Zisizo za Kiserikali, Madhehebu ya Dini, Washirika wa Maendeleo na Wadau wote wa Sekta ya Maji, kwa kuungana na Serikali katika juhud zake za kuwapatia Wananchi maji safi, salama na ya uhakika. Kwa njia ya pekee, namshukuru ndugu Mustafa Jaffer Sabodo, kwa kutoa msaada utakaowezesha uchimbaji wa visima 700 nchi nzima nje ya Dar es Salaam. Nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi ya Kauli hii, kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wananchi wa Rungwe Mashariki, kwa dhamana kubwa, kunichagua bila kupingwa kwa mara ya tatu mfululizo kuwa Mbunge wao. Naahidi kuendelea kuwatumikia wao na Watanzania wote kwa bidii na unyenyekevu mkubwa. (*Makofi*)

Nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kunisikiliza. Maji ni Uhai na Usafi wa Mazingira ni Utu. Kwa heshima kubwa, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

### **Uteuzi wa Wabunge wa Kambi ya Upinzani**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 50, ningependa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani atoe kauli anayotaka kuitoa.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE - KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi katika kikao hiki kwa kutumia Kanuni ya 50, inayoruhusu Maelezo Binafsi ya Mbunge kutekeleza matakwa ya Kanuni ya Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 15(2) inayosema kama ifuatavyo, nanukuu: “Kiongozi wa Kambi Rasmi ya

Upinzani Bungeni atateua Wabunge wa Chama chake au Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambao watakuwa Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara zilizopo za Serikali.”

Mheshimiwa Spika, ni matumaini na matarajio yangu na ya Watanzania wote kuwa, Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani wataisimamia vilivyo Serikali na kutimiza kwa vitendo ibara ya 63 ya Katiba kuhusiana na majukumu ya Bunge. Ileweke wazi kuwa, Wasemaji Wakuu wa Upinzani ni Mawaziri wanaosubiri na hivyo watafanya ama kuonesha yale ambayo Serikali haikuyaona au imeshindwa kuyatekeleza. Lengo la kuwa na Serikali ni kuonesha mtazamo wa pili na pale patakapohitajika tutatoa ushauri. Baraza Kivuli litashauri vilivyo na hatutasita kukosoa kwa lengo la kujenga pale inapobidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na idadi ya Mawaziri na Manaibu Mawaziri wa Serikali kuwa 50, uteuzi wangu wa leo umeteua Wasemaji Wakuu na Manaibu wao wasiozidi 29. Ili kuishi kivitendo, kilio chetu cha muda mrefu cha kuwa na Baraza dogo la Mawaziri na natambua uwezo mzuri sana wa Waheshimiwa Wabunge wetu, lakini ni vema kutenda yale tunayoyahubiri. Ninatoa rai kwa Serikali kwamba, watendaji wote wapewe ushirikiano kwa wasemaji hawa ili waweze kutekeleza majukumu yao na kuimarisha demokrasia yetu. Ikumbukwe kwamba, Watendaji wa Serikali au *Civil Servant* hawastahili kuwa na chama chochote na wanahudumia Serikali iliyopo na kuwa tayari kuhudumia Serikali bila ya kujali itaundwa na chama gani cha siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonesha kuwa, Wasemaji wa Upinzani wamekuwa wakionekana wanoko au pengine vizabizabina na wasio na uzalendo, pindi wanapohoji au kuikosoa Serikali. Ni rai yetu kuwa, muono huu sasa uondoke kwani lengo letu sote ni kujenga nchi yetu iwe na uchumi imara na demokrasia ya kweli kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu wote. Kwa kuwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ndicho kilichotimiza masharti yatokanayo na Kanuni ya 14(4) ya kuchagua Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni; hivyo basi, mimi nikiwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, nimeamua kwa sasa kuunda Baraza la Waziri Kivuli kutoka CHADEMA peke yake. Natambua kuwa, Kanuni za Bunge zimebadilishwa na sasa Wabunge wote wa Upinzani wapo chini ya uongozi wangu. Hata hivyo, kwa kuwa bado mawasiliano hayajakamilika na kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na Baraza hili, nimeonelea niteue kama nilivyo eleza awali kutoka CHADEMA pekee.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa, hapo siku za usoni na baada ya kuelewana na kuridhiana na wenzetu, nitaweza kuunda Baraza litakaloweza kushirikisha vyama vingine kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani kwa wakati muafaka. Napenda kuchukua fursa hii, kuwapongeza Wabunge wote wa Upinzani waliochaguliwa kuongoza Kamati za Bunge za Udhhibit wa Fedha za Umma, kwa maana *PAC*, *LAAC* na *POAC*. Ninawahakikishia ushirikiano wangu wa dhati kama Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni sambamba na Baraza zima la Wasemaji Wakuu wa Upinzani katika kuisimamia Serikali kwenye majukumu ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo basi, naomba kuwataja Waheshimiwa Wabunge kutoka Kambi ya Upinzani ambao watakuwa ndiyo Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani kulingana na idadi ya Wizara za Serikali zilizopo. Naanza na Ofisi ya Waziri Mkuu; atakayekuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni mimi mwenyewe Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbobe, nikiwa vile vile Kiongozi wa Kambi hiyo hapa Bungeni na hata nje ya Bunge, nitasaidiwa kwa karibu na Mheshimiwa Silinde David Ernest, Mbunge ambaye yechee atashughulika na masuala ya TAMISEMI (Utawala). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), itasimamiwa na Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis.

**SPIKA:** Kama wapo tunaomba wasimame.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI:** Nitaanza na Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbobe, nipo hapa; Naibu wangu Kivuli atakuwa Mheshimiwa Silinde David Ernest, atakuwa msaidizi wangu wa karibu sana; Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis; Uwekezaji na Uwezeshaji, Mheshimiwa Esther N. Matiko; na Naibu Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu mwingine ambaye tutasaidiana katika kuratibu Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye kwa kweli ana majukumu mengi ni Mheshimiwa Vicent Kiboko Nyerere. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, atakayekuwa anashughulika kama Msemaji Mkuu kwenye Ofisi ya Rais, Utawala Bora ni Mheshimiwa Said Amour Arfi, ambaye kwa bahati mbaya yupo kwenye matibabu; atakayekuwa Msemaji Mkuu wa Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) ni Mheshimiwa Mchungaji Israel Y. Natse; Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) ni Mheshimiwa Susan A. Lyimo; Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) ni Mheshimiwa Pauline P. Gekul; na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ni Mheshimiwa Leticia Nyerere. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, ambaye ni Naibu Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Kwa uzito wa Wizara hii atasaidiwa na Naibu Waziri Kivuli, ambaye atakuwa Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Godless Lema; Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Tundu Lissu, ambaye vile vile ni Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Ezekia D. Wenje; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Joseph Selasini; na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvubi, Mheshimiwa Silvester M. Kasulumbayi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ni Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni Mheshimiwa Halima James Mdee; Wizara ya Maliasili na Utalii ni Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa; Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa John John Myika; Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Eng. Salvatory Machemuli; Wizara ya

Uchukuzi, Mheshimiwa Mhonga Saidi Ruhwanya; Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Lucy F. Owenya; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, Mheshimiwa Christowaja Mtinda; na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Dkt. Gervas Mbasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kazi na Ajira, Mheshimiwa Regia Mtema; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Naomi A. Kaihula; Wizara ya Habari, Vijana na Michezo, Mheshimiwa Joseph O. Mbilinyi; Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Mustapha Akunaay; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Meshack Opulukwa na wa mwisho ni Msemaji Mkuu kwenye Wizara ya Maji, Mheshimiwa Highness S. Kiwia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, Wabunge wetu wote wana sifa ya kuwa Wasemaji Wakuu hususan Mawaziri, lakini ukweli ni kwamba, tumeona tuishi kivitendo, kauli yetu umuhimu ya kuwa na Baraza dogo Kivuli ambalo litafanya kazi kwa kadiri iwezavyo kuweza kuisadia Serikali kwa kuikosoa na tunawaomba watuelewe na watupe ushirikiano nasi tutashirikiana nao kwa kadiri itakavyowezekana. Nawatachia kazi njema. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mbona hamshangilii Mawaziri jamani? (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, alichokifanya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ni kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu cha 14(4), anao uwezo wa kuchagua Baraza lake kutokana na chama chake au na chama kingine.

Mimi napenda niliweke wazi Bunge letu; tutafanya mambo ndani ya Bunge, siyo mambo ya magazeti kutufundisha sisi namna ya kufanya kazi; haitusaidii na wala haiwasaidii wao. Kinachofanyika ni kuwadanganya Wananchi na Wananchi kuamini kwamba, magazeti ndiyo yanasema kweli.

Anachokifanya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kipo katika mujibu wa Kanuni zetu. Bado Kiongozi alichosema ni kwamba, ataangalia baadae wenzake wengine atakapofanya mabadiliko na hiyo pia anaendelea kuifanyia kazi.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 16(4), inabidi wakae wote wakubaliane utaratibu watakaoendesha Kambi yao kwa mujibu wa taratibu za Kanuni. Hiyo ni Kanuni ya 16(4). Kambi itabidi itengeneze Kanuni ya namna ya kuijendesha yenye.

Sasa kwa kuanzia, ameona aanzishe watu wake kusudi waweze kukusanya mawazo, kwa utaratibu wao watakubaliana ni namna gani watakavyoendesha Kambi ya Upinzani Bungeni. Sasa wanasema Mheshimiwa Spika, amepindisha kanuni; vipi?

Tulichokifanya siku ile ni kutafsiri hata wenyewe wameshaelewa kwamba ni utaratibu ulio sahihi na wa Kimataifa, hatuwezi kuwa na Kambi tatu humu ndani; Kambi ni mbili tu.

Hawa jamaa wanaıtwa Waziri Kivuli kwamba, wao wanataka kuikosoa Serikali ili Serikali iliyoko huku iondoke waingie wao. Hawa wanatakiwa wa-*maintain* Serikali walijonayo kusudi wasiondolewe. Ni makambi mawili tu basi. Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa Tanzania ni Mheshimiwa Mbewe. Akienda nchi yoyote anatambulika na anapewa *status* zote za Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

Akiwa Kiongozi wa Kambi ya CHADEMA hawezi kupewa; na sasa kwa sababu CHADEMA wana asilimia 12.5 ndiyo maana amechagua Mawaziri katika Kambi yake; hii ndiyo tofauti. Uongo ulioelezwa na Gazeti la Mwananchi jana, hauna maana wala mantiki.

Naomba kazi zetu zifanyike humu ndani siyo kufanyia nje. Sisi hatuwatambui wale wote wanaofanya kazi nje. Kwa hiyo, wananchi mkisoma magazeti someni kama barua nyingine zozote, lakini Bunge ni hili hapa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri Vivuli wote waliochaguliwa. Kama alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kazi yenu ni kuikosoa Serikali na kuonesha sera mbadala mnazofikiria ninyi ndizo zitakazoweka Serikali vizuri. Huo ni wajibu wenu kabisa. Kwa hiyo, mfanye hiyo kazi yenu ila ninachokisema, ndani ya Bunge letu tujenge heshima ya Bunge la Tanzania. Tunakosoana, lakini tunakuwa marafiki wakati wote. Hilo ndilo nawaombeni tulifanye vizuri.

Sasa tunaendelea na shughuli za leo. Kama mtakavyoona, leo hii tutapunguza tena idadi ya wachangiaji kwa sababu tumetumia muda huu halafu na jioni tutakuwa na uchaguzi. Kwa hiyo, wengi hawatapata nafasi. Kesho tunakusudia asubuhi tuweze kuendelea na mijadala lakini jioni tuache upande wa pili waweze kutoa ufanuzi wa mambo mbalimbali mliyosema. Kwa hiyo, utakuta pia idadi yetu inapungua.

Kwa hiyo, ninaomba niwaite Mheshimiwa Januari Makamba kama yupo atafuatiwa na Mheshimiwa Christowaja Mtinda. Halafu Mawaziri aliowachagua Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, mimi niliunda Kamati zangu kabla yeye hajaunda hili Baraza, kwa hiyo, zitakuwa na mabadiliko ya hao waliochaguliwa. Kama hayuko kwenye Kamati ambayo *portfolio* yake inayoangukia, tutamhamishia kwenye Kamati ambayo ana-*portfolio* yake. Haya ni makubaliano tuliyofanya na makubaliano na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Mheshimiwa Januari Makamba.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 68(7) na Kanuni ya 63(6), nikinukuu Kanuni ya 63(6) inasema: “*Mbunge aliyetakiwa kuthibitisha ukweli wa kauli au usemi au wa maelezo yake aliyyoyatoa Mbungeni atawajibika kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge papo hapo au katika muda utakaopewa na Spika kwa ajili ya kufanya hivyo.*”

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba katika Kikao cha tarehe 10, mwezi huu wa Februari Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini aliomba kupata ufanuzi kwamba Mbunge anaweza akachukua hatua gani kama anaona Kiongozi mwenye nafasi kubwa katika nchi kama Waziri Mkuu analidanganya Taifa na kulidanganya Bunge.

Mheshimiwa Spika, ukatoa ufanuzi katika maeneo kadhaa, lakini mwisho wa ufanuzi wako ukalielekeza Bunge kwamba, na naomba nikunukuu, kwa mujibu wa kumbukumbu za Kikao cha Bunge cha siku hiyo ulisema kwamba: “*Kwa hiyo, tarehe 14 kipindi cha asubuhi atoe maelezo ya kwamba Waziri Mkuu amesema uongo. Maana yake alichosema ni kwamba Waziri Mkuu amesema uongo, sasa anataka tumpe mwongozo wa namna ya kufanya na akasema aandike. Sasa kifungu hiki cha 64 kinamda elete maelezo hayo mpaka tarehe 14.*”

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako. Kwa kuwa kwa mujibu wa maelekezo uliyoyatoa na maelezo ya Mheshimiwa Godbless Lema, alipaswa atoe maelezo hayo leo wakati huu wa asubuhi kwenye Bunge lako Tukufu. Naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Ndivyo nilivyosema na ataleta kwa Spika kwa maandishi. Spika atatumia namna yake ya kuendesha Kikao cha Bunge anavyoona inafaa. Kwa hiyo, utaleta kwa maandishi. (*Makofî*)

**MHE. JANUARI Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukupongeza kwa uongozi wako mahiri wa Bunge letu, hukutetereka hata pale ambapo umejaribiwa na umedhihirisha na kuthibitisha kwamba Chama chetu hakikufanya makosa kukuteua wewe, lakini hata Bunge letu kwa ujumla na lenyewe halikufanya makosa kukuchagua kuongoza Taasisi yetu hii muhimu. Nanong’onezwa hapa kwamba wanawake wanaweza na naamini kweli wanaweza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Bumbuli kwa kuniamini na kunichagua kuwa mwakilishi wao kwenye Bunge letu Tukufu, nawaahidi kwamba zile changamoto za Jimbo letu, maji, barabara, umeme zahanati, elimu, mikopo, Walimu, Madaktari, Wauguzi tutawashughulikia zote kwa maarifa mapya na kwa nguvu mpya na kwa kasi mpya na safari yetu ya maendeleo tutafika salama.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ipo kwenye tatizo la uhaba wa umeme na tayari Bunge letu linayo Kamati ya Nishati na Madini ambayo mimi ni Mwenyekiti.

Nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti na imani ambayo wameionesha kwangu. Sasa tuliomba kibali kwako kwamba kutokana na hali ya sasa ya umeme, basi Kamati yetu ianze kazi mara moja ili Bunge letu na lenyewe lishiriki kwenye kutafuta suluhu ya tatizo hili. Nafurahi na ninashukuru kwamba ulitukubalia na kazi hiyo tumeianza.

Mheshimiwa Spika, jana tulikwenda kwenye kituo cha kuzalisha umeme Mtera, tumeona hali halisi na tumeamua kwamba Bunge litakapoahirishwa tarehe 18, basi wakati Waheshimiwa Wabunge wanakwenda Majimboni, Kamati yetu sisi itakuwa Dar es Salaam, tutahamia pale wiki nzima kuzungumza na watu wa Wizara, watu wa *TANESCO*, wadau wote wa kwenye sekta ya umeme kusaidia Bunge letu na lenyewe litoe mchango kwenye kumaliza hili tatizo. Naomba niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba safari hii Kamati yenu itatumia maarifa yote, jitihada zote kuhakikisha kwamba Bunge letu linatoa mchango kwenye kumaliza tatizo hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tutaisimamia na kuishauri Serikali pale inapobidi, tutaisinikiza ili ifanye maamuzi sahihi na ya haraka kumaliza tatizo la umeme. Watu wanachotaka sasa ni umeme na sio orodha ya miradi ya kuzalisha umeme. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nilivyoomba nafasi ya Ubunge na nikaipata, nilikuja kwenye Mkutano wa Kwanza mwezi wa Novemba, nikaingia Bungeni nikaogopa. Kwanza nikiamini kwamba Ubunge ni nafasi kubwa, nafasi ya heshima, lakini hata jengo lenyewe mazingira yenewe yanaogopesha. Kwa hiyo, nilikaa kimya kikao cha kwanza ili nione na nijifunze. Nakumbuka Rais wa zamani wa Marekani John F. Kennedy kabla ya kuwa Rais alikuwa *Senator*, na kabla ya kuwa *Senator* alikuwa Mbunge na kule wenzetu Bunge ni miaka miwili. Mwaka mzima wa kwanza hakuzungumza Bungeni, mwaka wa pili mpaka katikati alikuwa hajazungumza. Alivyoulizwa kwanini, akasema ule mwaka wa kwanza niliutumia kushangaa, nimeingiaje Bungeni? Baada ya kuwasikiliza watu wanavyozungumza na yanayotokea Bungeni, nikautumia mwaka wa pili kushangaa na wao waliingiaje Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Kwanza niliutumia kushangaa nimefikafikaje hapa? Lakini baada ya kuona baadhi ya mambo yaliyojiri kwenye Mkutano wetu wa kwanza, vioja na vituko vilivyofanywa na baadhi ya wenzetu, nikaanza kushangaa wamefikafikaje Bungeni? Lakini hofu hiyo iliondoka juzi baada ya kusikia mchango wa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni - Mheshimiwa Freeman Mboge ambaulielekeza kwamba mwenendo walioanza nao wameona haulipi na kwamba sasa hivi wanabadilisha uelekeo wa namna ya kushiriki kwenye mijadala ya hapa Bungeni na kwa msingi huo, tunategemea mabadiliko ya namna ambavyo wenzetu watashiriki kwenye Bunge letu hili. Maana yake ni kwamba, mahafidhina wenye Chama kile hawana nafasi tena na kwamba sasa kama walivyodhamiria sasa ni Bunge moja. Sisi tunawaahidi kwamba kwa mwenendo huo tutafanya kazi kwa pamoja na tutashirikiana ili Bunge letu hasa liwe moja na wote tutoe mchango kwa maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hotuba ya Rais, imechangwa vizuri, bahati mbaya ukichangia mwisho unakuwa umefilisiwa sana, maneno mazuri yamekwishazunguzwa. Labda nichangie jambo tu dogo.

Mheshimiwa Mbunge wa Ubungo wakati anachangia alisema kwamba kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais pale alipokemea migawanyiko kwenye nchi yetu, hasa udini, mwenzetu aliitafsiri kwamba ni kueneza huo udini kwa kuukemea. Naomba nitofautiane na hilo na ni dhana potofu. Utakumbuka sisi wote ni wanafunzi wa Mwalimu Nyerere na siku zote alikuwa anazungumzia nyufa zilizokuwa zinaanza kujitokeza. Moja, ya ufa alioutaja ni uduni na alikuwa anaimba sana kuhusu umoja wa nchi yetu. Sasa ni wajibu wa kiongozi kwanza hata kama hakuna dalili zozote za hizo nyufa, ni wajibu wa kuzizungumzia ili zisitokee na pale alipokuwa ameziona ni wajibu wake kuzizungumzia ili zisiendelee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, binafsi ningeshangaa kama hotuba ya Rais isingekuwa na Ujumbe wa Umoja wa Kitaifa. Sasa wakati Mwalimu Nyerere anatuhimiza tuzibe nyufa ikiwemo nyufa ya udini, hatukuona tatizo, lakini Rais wa Nne anapofanya hivyo, tunaona ni tatizo. Sasa hapa tatizo sio *principle*, tatizo labda ni Rais mwenyewe. Sasa mimi naomba kumhimiza Mheshimiwa Rais aendelee, nasi Wabunge sote tuendelee kuhimiza umoja wa kitaifa, nchi yetu ni moja, iendelee kuwa moja na pale tunapoona dalili za migawanyiko tuzungumze bila uwoga wala kificho.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumze mambo ya Jimboni kwangu, Bumbuli. Nitazungumza kwa kifupi. Yameulizwa maswali mengi sana hapa toka tuenze kuhusu mgawanyo wa Wilaya. Sisi watu wa Bumbuli kwa muda mrefu sana tumekuwa tunaomba Wilaya, lakini tunaambiwa vigezo bado. Ni kweli viko vigezo saba au nane vya kuwa Wilaya, ambavyo ni eneo, idadi ya watu, mazingira maalum, Kata, Tarafa, uwezo wa Serikali na utayari wa wananchi wenyewe kuchangia Wilaya. Sasa ukivichukulia vigezo vyote kwa pamoja, hakuna eneo linaloweza kuwa Wilaya nchini. Hata Wilaya ya Siha wenyewe ukivichukua vigezo vyote haiwezi kuwa Wilaya. Maana yake ni kwamba tunapoamua baadhi ya vigezo tunavipa uzito kuliko vingine kwa mazingira maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuna kigezo kinasema, lazima tuwe na watu 250,000 ili kuwa Wilaya. Lakini Wilaya ya Pangani ina watu 42,000. Hatusemi Serikali ilikosea, hapana. Bali iliamua kuvipa uzito vigezo vingine kuliko hiki cha idadi ya watu. Sasa sisi watu wa Bumbuli tuna watu 167,000, kwa hiyo, huwezi kusema hatujafikia idadi ya watu inayotaka Wilaya. Tarafa tunazo za kutosha, Kata tunazo za kutosha, kwa hiyo nadhani Serikali ingekuwa *fair* kidogo ili hivi vigezo visiwe vinaamuliwa kulingana na utashi au *pressure* ya kisiasa ya Mbunge au wananchi wenyewe. Wote tunajua kwamba tuna tatizo la raslimali za maendeleo na unapoisogeza huduma karibu na wananchi, basi unakuwa umelipunguza hilo tatizo.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile napenda kupendekeza kwamba Serikali iangalie uwezekano na iwe bunifu kidogo pale kwenye kutafuta raslimali za maendeleo. Kwa mfano, inawezekana kabisa hizi Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji

zikaweza kutoa *bond*, kwa Kiswahili sina hakika, ni dhamana. Kwa sababu Halmashauri inakusanya mapato, ina uhakika wa mapato kutoka Serikalini, iruhusiwe kukopa pesa nyngi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika mahali hapa. Pia naomba nichukue nafasi hii ya kipekee kabisa kukupongeza wewe kuwa mwanamke wa kwanza kuwa Spika katika nchi za Afrika ya Mashariki na kama mwanamke, sina budi kukupa pongezi za dhati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niende moja kwa moja katika kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Nimesoma kwa makini kabisa Hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa katika ufunguzi wa Bunge. Nami napenda nichangie katika vipengele vichache kutokana na muda.

Mheshimiwa Spika, nianze na kipengele cha elimu. Sote tunafahamu kwamba elimu ni mkombozi, na bila elimu hakuna ambacho kinaweza kufanyika katika maendeleo ya nchi na maendeleo ya mtu binafsi. Watu ni mashahidi kabisa na matokeo ya elimu bora inayotolewa katika shule zetu kuanzia za awali mpaka vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nijikite katika elimu ya sekondari na ikiwezekana katika elimu ya juu. Tunafahamu nia nzuri ya Serikali kuanzisha Sekondari za Kata kwa wananchi wetu. Nia ilikuwa ni njema, kuwasogezesa wananchi shule ambazo watoto wanaweza kusoma ili kupunguza umbali wa kutembea, na ili wanafunzi wetu au watoto wetu waweze kupata elimu. Lakini kama ilivyoonekana ni kwamba, aidha, wazo hili lilitolewa bila kuangalia uwiano kati ya wingi na ubora au lilitolewa kwa haraka. Nasema hivyo nikizingatia kabisa maana ya shule. Shule lazima iwe na vigezo vifuatavyo na hasa shule ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, shule ya sekondari ni lazima iwe na madarasa ya kutosha, ni lazima iwe na maabara pamoja na vifaa vya maabara, ni lazima iwe na mabweni ya watoto wa kike na wakiume, ni lazima iwe na viwanja vya michezo, ni lazima iwe na mabwalo ya kulia chakula na majiko ya kupikia chakula.

Mheshimiwa Spika, shule ya sekondari zaidi ya yote ni lazima iwe na walimu waliofundisha walimu. Maana yake ni kwamba, kwa mwalimu wa shule ya sekondari ni lazima asome au baada ya kumaliza kidato cha sita afaulu kwa kiwango cha daraja la kwanza, la pili na la tatu na aende chuo kuchukua stashahada au diploma kwa miaka miwili. Katika stashahada anayochukua, ndani ya mwezi mmoja aweze kufanya mafunzo kwa vitendo ili arudi kufundisha shule ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, shule zetu za sekondari za Kata zimekuwa na matatizo ya ualimu. Sio uwingi wa walimu tu, bali hata ubora wa walimu. Walimu waliopelekwa katika sekondari za Kata wamekuwa ni wale walimu ambao wamepitia katika *crash*

*programme* ya wiki tatu au miezi tisa au miezi sita. Walimu hao badala ya kupewa vyeti wanapewa kitu kinaitwa leseni.

Mheshimiwa Spika, mbali ya hiyo, walimu hao ni wale ambao hawakufanya vizuri katika mitihani yao ya kidato cha sita. Wanachukuliwa wale ambao wamepata alama au wamepata Daraja la Nne tena *point* 29 mpaka 30. Matokeo yake hawafundishwi kikamilifu jinsi ya kwenda kuwafundisha wanafunzi. Wao wameshindwa mitihani na pia wanakwenda kufundisha wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake tumeyaona katika matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka jana. Shule za Sekondari za Kata badala ya kung'ara kwa kufaulisha, zimeng'ara kwa kutoa sifuri. Tumesikia asilimia 12 ndio waliofaulu, lakini asilimia iliyobakia ndio waliofeli.

Mheshimiwa Spika, hili ni janga la Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, mimi kama mdau wa elimu ningependa kushauri yafuatayo:- Serikali irudishe ule mfumo wake au kuuboresha, wa kuwafundisha walimu miaka miwili Chuo cha Ualimu kwa Diploma. Pia ikiwezekana, wanafunzi waliofaulu kidato cha sita kwa daraja la kwanza, la pili na la tatu walazimishwe kwenda kusomea ualimu ili warudi kufundisha wanafunzi wa shule zetu hasa sekondari za Kata ambazo zina upungufu mkubwa wa walimu.

Mheshimiwa Spika, kingine, wanafunzi waliomaliza mtihani wa Kidato cha Nne mwaka jana ni matokeo ya kufutwa kwa mchujo wa mtihani wa kidato cha pili mwaka 2008. Mtihani wa mchujo ulikuwa ni mtihani wa muhimu sana ili kuweza kumfanya mtoto aweze kumudu au aweze kupata ile *knowledge* ambayo anatakiwa kuifahamu.

Mheshimiwa Spika, nashauri mitihani yote ambayo ilikuwa ni ya mchujo kuanzia Shule ya Msingi ya darasa la nne irudishwe. Pamoja na kwamba ipo, lakini sasa mchujo urudishwe na kidato cha pili mchujo urudishwe.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie pia kwenye elimu ya juu. Tunafahamu kwamba katika miaka ya 1980 mwishoni na miaka ya 1990, sera ya ubinafsishaji ilianza nchini kwetu kufuatia zile programu za SAP (*Structural Adjustment Programmes*) na Tanzania haikuwa nyuma.

Mheshimiwa Spika, mipango hiyo imekuwa na madhara makubwa sana katika elimu ya juu. Sasa, mimi napenda kushauri kifuatacho:-

Kwa sababu kumekuwa na idadi kubwa sana ya wanafunzi...

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE – WAZIRI WA KILIMO,  
CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu!

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu!

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE – WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Ndiyo! *Section* ya 63, kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Spika, msemaji aliyejikuwa anaongea hivi punde, alieleza kama Shule za Sekondari hazina walimu, zina walimu wa cheti.

Mheshimiwa Spika, walimu wa cheti katika Shule za Sekondari walichukuliwa wote wakapelekwa kwenye Vyuo Vikuu. Katika shule zetu za sekondari tunao walimu wenye Diploma katika elimu na walimu wenye shahada. Mwaka huu, 2010/2011 zaidi ya walimu 19,120 waligawanywa katika shule zote za sekondari hapa nchini na kila shule ilipata zaidi ya walimu watano ambao ama wana shahada ama wana Diploma. Kwa hiyo, sio kweli kwamba shule zetu zimejaa walimu wa leseni.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Huo siyo utaratibu, hiyo ni taarifa. Endelea Mheshimiwa.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru msemaji aliyejipa. Nami napenda kusema kwamba nimetembea Jimbo la iliyokuwa Singida Kusini na sasa ni Singida Magharibi na Singida Mashariki, Jimbo zima, Kijiji kwa Kijiji, Kata kwa Kata, nimetembea na nimejionea shule ambazo zipo.

Mheshimiwa Spika, napenda nikwambie kwamba naomba Waziri anayehusika na Wizara hiyo afanye pia ziara akaangalie na afanye sensa ya walimu waliopo ili aweze kujiridhisha ninachosema kwamba ni kweli. Walimu wa leseni ndio wanaofundisha shule zetu. Mfano mzuri, kuna shule moja inaitwa Wembele iko Kijiji cha Mgungila. Shule ile ina majengo mazuri, lakini imefungwa kutokana na kutokuwa na mwalimu hata mmoja, amebaki mwalimu mmoja tu Mkuu ndiye anayelinda majengo ambayo yanakaliwa na popo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba niendelee kuhusu elimu ya juu. Elimu yetu ya juu imekuwa na matatizo makubwa sana. Nimesema kwamba kutokana na uwingi wa wanafunzi au mahitaji ya wanafunzi wanaotaka kujiunga na Vyuo Vikuu, Majengo yaliyojengwa au yanayoendelea kujengwa hayatoshelezi *to accommodate* ile namba ya wanafunzi ambao wanatakiwa kuingia Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake ni kwamba wanafunzi wengi wanakaa madirishani au nje kusikiliza *lecturer*. Mimi nimekuwa *lecturer* wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam sehemu ya Mkwawa, hili nalisema kwa uwazi kabisa na kwa ukweli.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wetu wamekuwa kama watu ambaeo hawana kwa. Wanafunzi hao wana matatizo makubwa sana. Tatizo lingine ambalo linasababisha, licha ya uchache wa vyumba vyaya kujifunzia, ni hii Bodi ya Mikopo. Bodi ya Mikopo imekuwa ni tatizo. Sijui ni utendaji au...

(*Hapa Kengele Ilipigwa*)

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, ni ya kwanza?

**SPIKA:** Ni ya pili. Tulilipa ule muda uliochukuliwa na huyu Mheshimiwa. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Said Mtanda na Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe ajiandae.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Lakini pia, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia mimi kuwa ndani ya Bunge lako hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kutumia nafasi hii siku hii ya Wapendanao kuwashukuru sana wapigakura wangu wa Jimbo la Mchinga kwa kunichagua, kwa kuniamini na kunifikisha hapa ndani ya Bunge lako Tukufu. Ninawaahidi kwamba sitawaangusha, nitafanya kazi kubwa ya kuwakilisha maslahi yao na maslahi ya jamii ndani ya Bunge letu hili.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii pia namshukuru sana Katibu Mkuu wa CCM ambaye kwa kiasi kikubwa amefanikisha mimi kufika hapa baada ya kufanya kazi Ofisi ya Katibu Mkuu kwa kipindi cha miaka minne, ninamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaingia katika mjadala huu wa hotuba ya Mheshimiwa Rais, nitumie fursa hii pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mchinga na wananchi wa Mkoa wa Lindi kwa ujumla kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuwateua Waheshimiwa Wabunge kutoka Mkoa wa Lindi akiwemo Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Majaliwa na Mheshimiwa Chikawe kuwa Mawaziri katika Baraza lake la Mawaziri. Sisi wana-Lindi tumefurahi sana na tuna hakika tutawasaidia wenzetu hawa waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, binafsi nampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa hotuba yake makini. Ametoa vipaumbele 13, nami nitajielekeza katika maeneo makubwa matatu. Eneo la kwanza ni eneo la elimu. Tumesoma hapa kipaumbele cha elimu, Mheshimiwa Rais ameahidi kwamba katika awamu hii ya uongozi ataendelea kuhakikisha elimu yetu inaboreshwu. Waswahili wanasema: “Ukijua kulaumu, ujue na kusifu.” Niipongeze sana Serikali yetu kwa kazi kubwa iliyoifanya kwa kushirikiana na wananchi kujenga shule hizi za Kata.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Uchaguzi la Mchinga, wananchi wa Mchinga wamefanya kazi kubwa sana kujenga *secondary schools* hizi za Kata. Tunatambua na tunaiomba Serikali kubaini matatizo makubwa yaliyomo katika sekta hii ya elimu ikiwemo upungufu mkubwa wa walimu. Shule ya Sekondari Mipingo ina mwalimu mmoja, tunategemea shule hii iweze kufanya vizuri, kwa staili gani? Kwa namna gani

shule hii ambayo haina mabweni inaweza kuwafaulisha watoto hawa katika kiwango kile tunachotarajia?

Mheshimiwa Spika, lakini suala la pili, katika elimu ni suala la mpango wetu wa kujenga *High School* kila Tarafa. Mimi nadhani ipo haja ya kutafakari sana na kwa umakini hoja hii au suala hili, kwa sababu tukijenga *High School* kila Tarafa wakati hatujaimarisha miundombinu katika shule hizi za *Ordinary Level*, kuna hatari kubwa ya baadaye kujenga *High School* hizi ambazo hazitakuwa na vijana wanaosoma katika maeneo haya.

Kwa hiyo, rai yangu kwa Serikali, kabla mpango huu haujaanza kutekelezwa, ni vyema tukafanya tafakari, ni vyema tukajikita katika ujenzi wa *High School* katika maeneo machache, lakini *High School* ambazo zitakuwa na walimu wa kutosha, zitakuwa *Boarding High School* ili vijana kutoka maeneo jirani na Tarafa hiyo ambayo *High School* hiyo itakuwepo, wapate fursa ya kukaa katika mazingira mazuri yenyе utulivu ili waweze kujipatia elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo nimeona kuna umuhimu wa kuchangia ni eneo la elimu ya juu. Sasa hivi Serikali na wadau mbalimbali wa elimu wanapozungumzia elimu, wanazungumzia sana kupanua Vyuo Vikuu na kutoa shahada (*degree*), lakini tunasahau maeneo mengine ambayo yangeweza kuzalisha watalaan wa daraja la kati. Kwa mfano, *technical schools* zetu mbalimbali sasa zimefikia pahala zimepandishwa hadhi na kutoa *Degree*. Lakini, hawa watalaan wa daraja la kati, inakuwa sio rahisi sana kuwapata.

Kwa hiyo, ninatoa wito kwamba wakati tunaendelea kufikiria namna ya kupanua vyuo vingi vitoe shahada (*degree*), lakini pia iko haja ya kuhakikisha *technical schools* zetu zinapewa nafasi kubwa ili vijana waweze kupata taaluma na baadaye waweze kujiajiri kuitia *skills* hizo wanazoweza kupata katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, tunalo suala lingine la ajira na uwezeshaji vijana kiuchumi. Hotuba ya Mheshimiwa Rais haijagusa kabisa eneo hili la ajira na uwezeshaji vijana kiuchumi. Ninatoa wito kwa Serikali kuona umuhimu sasa wa kurudisha yale Makambi ya JKT na kuimarisha vyuo vyetu vya ufundi. Tunashukuru pale Lindi tunajengewa chuo kikubwa cha *VETA*, ninaamini kabisa hata wapigakura wangu vijana wa Jimbo la Mchinga watapata fursa ya kupata ujuzi na maarifa kutoka chuo kile cha *VETA*.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ni maji, na Mheshimiwa Prof. Mwандосуа ametuambia hapa asubuhi kwamba maji ni uhai. Lakini, katika Jimbo la Mchinga tatizo kubwa la msingi ni maji. Ukienda Kiji cha Namkongo, Kilolambwani, Lihimilo, Ruhoma, wananchi wa maeneo haya hutumia takriban saa tano kwa siku kutafuta maji.

Tunapozungumza kwamba wananchi washiriki katika shughuli za kujiletea maendeleo yao, unamtakaje mwananchi huyu wa Namkongo, wa Lihimilo, wa Mnyangara anayetumia saa tano kwa siku kutafuta maji aweze kushiriki shughuli nyingine ya uzalishaji mali! Kwa hiyo, hata kufeli kwa wanafunzi wetu katika shule ile

ya sekondari ya Mipingo, mionganoni mwa sababu ni hizi, vijana wetu sasa wametumia muda mwingi pia kutafuta maji na kuacha masomo.

Kwa hiyo, ninatoa wito kwa Serikali kutekeleza miradi ya maji katika maeneo mbalimbali. Tunawashukuru wenzetu wa *World Bank* wameweza kutuletea miradi mitatu ya maji pale Mchingga, ambayo ni Mradi wa Maji wa Kilolambwani unaofadhiliwa na *World Bank*, Mradi wa Maji wa Namkongo, lakini pia Mradi wa Maji wa Likwaya.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ni kwamba kwa takriban miaka miwili sasa, miradi hiyo ya maji haijaweza kutoa maji na kuwanufaisha wananchi. Tunaiomba Serikali sasa ione haja ya kuchukua hatua kwa sababu maji ni kipaumbele kikubwa kinachoweza pia kuchangia kuinua maendeleo ya wananchi wale wa Vijijini. Ni asilimia 33 tu ya wakazi wa Wilaya ya Lindi Vijijini wanaoweza kupata maji safi na ambayo pia usalama wake ni mdogo. Ukilinganisha na wenzetu wa Kilimanjaro ambao wamefika sasa asilimia 70 na 80, sasa tunajiuliza, sisi watu wa Kusini hususan Mkoa wa Lindi tuna tatizo gani na Serikali yetu?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi tuna imani kubwa na Serikali hii, tunaomba suala la maji lipewe nafasi kubwa kwa sababu katika Ripoti ya Serikali ya *Poverty and Human Development* ya mwaka 2009 inasema ni asilimia 27 tu ya wakazi wa Vijijini wanaweza kupata maji safi na salama, ingawa sina hakika zaidi na usafi na usalama huo, kwa mwendo wa nusu saa. Lakini, ilitarajiwu kila baada ya mita 400 mwananchi wa Kijijini aweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hotuba ya Rais - Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete.

Awali ya yote, napenda kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutuwezesha tena siku ya leo kuendelea na kikao chetu cha Bunge. Lakini, pili napenda kuwashukuru wananchi na wapigakura wangu wa Mkoa wa Katavi (zamani Rukwa) kwa kuweza kuniamini na kuweza kufika hapa ili tuone namna gani tunaweza tukashirikiana nao katika kuangalia matatizo na changamoto zinazoweza kuwakabili wananchi wa Rukwa na kushirikiana kwa pamoja kuweza kuzitattua.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba hii katika eneo la elimu. Mengi yamekwishatamkwa, lakini naomba nichangie hotuba hii kwa ujumla wake. Katika suala la elimu, imeonekana hii sekta inasemwa sana. Kwa kweli tukirudi katika ukweli, mwalimu ni mtu ambaye kwa ujumla wake anapenda kutambulika katika jamii, na jamii inamtambua kwa umuhimu wake. Kutokana na Ilani yetu ya Chama, mimi ningependa Serikali ielekeze nguvu yake katika kuboresha makazi na maslahi ya mwalimu. Kwa mfano, Serikali inaweza ikashirikiana na Mamlaka ya Elimu Tanzania pamoja na Chama cha Walimu kuweza kusaidia namna gani inaweza ikaboresha makazi ya mwalimu hasa yule aliyeo Kijijini; sio tu makazi peke yake, lakini pia kupitia Chama cha Walimu.

Nakumbuka Mama Sitta akiwa Rais wa Chama cha Walimu aliweza kuelekeza Chama cha Walimu kikajenga jengo pale Ilala ambalo hilo jengo lingeweza angalau kukopa mikopo Benki na huo mkopo ukasaidia kujenga nyumba za walimu amba o walimu wangekuwa na maisha mazuri kabisa na wala sidhani kama wangekuwa na malalamiko yoyote kuhusu hili.

Mheshimiwa Spika, siyo nyumba tu, lakini pia kupitia Chama cha Walimu, Walimu ni wengi sana, na wanakatwa angalau asilimia mbili ya mshahara wao. Kupitia hela hizo kungekuwa na utaratibu kwa kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha kwamba vitendea kazi kwa walimu vinapatikana kwa sababu wanachangia ile pesa na ile pesa ni vyema ikaja ikafanya vitu vya maendeleo kuwasaidia kufanya kazi yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia pia kuhusu suala zima la utunzaji wa mazingira. Imeelezwa katika ilani na imekwishaelekezwa na baadhi ya maeneo yameanza kutendewa kazi, lakini pia ningependa kuiomba Serikali iangalie namna itakavyoweza kufanya kazi kwa ukaribu na Halmashauri zetu ili kuweza kulinda mazingira hasa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, ninaliongea hili kwa mfano halisi uliopo Mkoani kwangu Katavi. Mfano, Mto Stalike, tuna viboko wazuri sana pale, lakini kutokana na uharibifu wa mazingira, wale viboko mvua zinapokwisha kwa kweli utawaonea huruma. Nafikiri tuna viboko wazuri sana kuliko eneo lingine lolote. Kwa hiyo, naomba Wizara husika iweze kuliangalia suala hili kwa undani hasa kulinda vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchangia japokuwa Waziri wa Kilimo ameliongelea asubuhi, lakini napenda kuchangia kwa namna tofauti kidogo. Naomba Serikali kwa namna moja au nyingine ichukue juhudzi za haraka kabla msimu wa kilimo haujaanza, ione ni namna gani ambavyo inaweza kuangalia mfumo mpya wa utoaji wa pembejeo za kilimo.

Kwa mfano, mkulima wa Mkoa wa Rukwa au Katavi inapofika msimu wa kilimo anaweza kupewa pembejeo labda vocha tatu, yaani vocha ya mbolea, vocha ya mbegu na mbolea ya kukuzia, lakini aidha kwa uwezo wake mdogo kiuchumi, au kwa sababu nyingine zozote zinazoweza kuwa zinamkabili mkulima yule akashindwa kutumia vocha hizo tatu, akajikuta labda anatumia vocha aidha ya mbegu tu ama ya mbolea ya kupandia, hizi vocha nyingine labda alishaelekezwa azichukue zile tatu, lakini hizi mbili anashindwa kuzitumia, sasa hizi mbili sijui kama Serikali au Wizara husika imeweza kuangalia ni namna gani hizo vocha zinarudishwa, ama hiyo hela inaweza ikaelekezwa katika shughuli nyingine za maendeleo badala ya kuendelea kuagiza vocha kama hizo wakati mkulima hazitumii. Ina maana hiyo hela inapotea bure. Ni vyema mfumo huo ukarudiwa upya kuangaliwa: Je, mkulima wa ekari ngapi ana uwezo wa kutumia vocha kiasi gani? Hela inayobaki ikaelekezwa kwenye sekta nyingine za elimu ama za afya.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuongelea suala la uanzishwaji wa zahanati katika kila Kata. Uzoefu unaonesha kwamba kutokana na namna tulivyoanzisha shule

zetu za Kata, zimekuwa na matatizo mengi hususan vitendea kazi pamoja na watumishi. Naomba Serikali iangalie, kabla ya kuanzisha hizi zahanati kila Kata ni vyema sasa badala ya kuweka zahanati kila Kata, labda tuweke katika Tarafa nzima zahanati mmoja kulingana na ile *labour force* tulioi-produce kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, mengi kama nilivyoeleza yamekwishaelezwa na wachangiaji waliopita, sioni sababu ya kuendelea kurudia maneno, wananchi wameelewa na wanajua vilio vyao, mimi ninaunga mkono hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, nami nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya Rais. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuongea basi nitumie fursa hii...

**SPIKA:** Mheshimiwa, simama hapo hapo kwanza, halafu jiangalie wewe na mimi na yule anayezungumza utakuta umekata kati ya Spika na Msemaji. Endelea.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kwa heshima kubwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mvomero kwa kunipa heshima hii kubwa ya kunichagua kuwa Mbunge wao, nami nawaahidi tu kwamba kazi waliyonipa kwa miaka mitano sitawaangusha, nitawatumikia kwa moyo wangu wote.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, naomba nimpongeze Rais Kikwete kwa ushindi mkubwa alioupata katika uchaguzi tuliofanya Oktoba 30, 2010. Lakini pia nimpongeze kwa hotuba nzuri ambayo mimi naiona ni kwamba ameeleza mambo ya msingi kabisa, tulikotoka, tulipo na wapi tunakokwenda. Kwa hiyo, hotuba hii mimi naipongeza sana, ni dira kwetu katika miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee mambo yanayohusu Jimbo al Mvomero na niseme kwamba asilimia tisini ya wananchi wa Jimbo la Mvomero ni wakulima, kwa hiyo, mimi nitajikita katika suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kupitia kauli mbiu ya Kilimo Kwanza itekeleze kwa vitendo kwa maana ya kupeleka watalaam wa kilimo vijijini huko tuliko. Tusiwe na watalaam wa kilimo amba wanakaa maofisini badala ya kukaa na wakulima kuwasaidia katika mambo ya ushauri. Lakini lingine ni kwamba, upatikanaji wa pembejeo, tunaomba sana Serikali itekeleze kauli mbiu hiyo na wakulima wapatiwe pembejeo kwa wakati na kwa bei inayostahili.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala zima la uwezesajhi Serikali katika kutekeleza kauli mbiu hiyo ya Kilimo Kwanza, iwaangalie wakulima kuwawezesha vikundi vyta wakulima wadogo wadogo kimitaji. Sina taarifa za kutosha juu ya suala zima la mabilioni ya JK kama wakazi wa Mvomero nao waliwahi kufaidika. Kama fedha hizi zipo,

ziwafikie wakulima na wananchi wa kawaida ili waweze kujikwamua kiuchumi kwa maana ya kuwekeza katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika kusaidia kilimo ni lazima kuwepo na miundombinu ambayo inawasaidia wakulima. Jimbo letu la Mvomero tuna historia kwamba soko kubwa la Kariakoo bidhaa nyingi kama vile mpunga, matunda yanatoka Jimbo la Mvomero. Kwa hiyo, Serikali ifanye jitihada za kutengeneza barabara za vijijini kuona kwamba wananchi wanaotoka Tarafa ambazo kunapatikana mboga mboga nyingi na matunda, basi kuwepo na uhakika wa kupitika kwa barabara hizo na maeneo mengine kama Kibati, Maskati, Mzia na Kanga kuona kwamba barabara hizi zinapitika muda wote na wananchi kupeleka mazao yao katika masoko kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niliongelea suala zima la kiwanda chetu cha sukari cha Mtibwa. Mimi sioni sababu ya Serikali kuwa na upungufu wakati mwingine wa sukari wakati tunavyo viwanda vikubwa kama *Kagera sugar*, Kilombero na Mtibwa. Lakini juzi niliuliza swalii na nikapata majibu ambayo hayakutosha sana, lakini nataka niseme kwamba sioni sababu ya Tanzania kuendelea kuwa na upungufu wa sukari wakati viwanda hivi vikubwa kabisa vina uwezo mkubwa wa kuzalisha sukari.

Kwa mfano, kiwanda cha Mtibwa wakati mwingine wananchi na wakulima wanaanza kukata tamaa kwa sababu ya matatizo ya kiwanda kilichopo sasa. Kwa hiyo, wananchi kama nilivyosema, bei ya miwa imekuwa ni ndogo ikilinganishwa na wenzao wa Kilombero. Hii inawakatisha tamaa na sio ajabu wananchi baadaye huko mbele wakaamua kubadilisha, wakaanza kulima mpunga badala ya kulima miwa.

Mheshimiwa Spika, hii inawakatisha tamaa kwa sababu mnunuzi ni mmoja na wao wamekuwa kama mateka kwamba wapende wasipende watauza miwa yao hapa, lakini uvumilivu huu una muda. Ipo siku wananchi wataamua kubadili aina ya zao na hatimaye kiwanda kile kinaweza kikafungwa hivi hivi.

Kwa hiyo, ninaomba Serikali ifanye jitihada za kuona kwamba matatizo tunayoyaeleza ya Mtibwa kwa maana ya wakulima kulipwa bei ndogo, mafao ya watumishi kucheleshwa, mishahara midogo, lakini pia bei ndogo ya miwa, Serikali iingilie kati ili kuwe na sukari ya kutosha na wananchi wako tayari kulima miwa ya kutosha na kukipatia kiwanda cha Mtibwa hatimaye tuwe na sukari ya kutosha katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba Wilaya yetu bado ni mpya, tunaomba suala la mawasiliano na Waziri anayehusika aangalie uwezo wa kuliunganisha Jimbo la Mvomero na Wilaya ya Mvomero kwa mawasiliano kwa maana ya kujenga minara mbingi ya simu. Yapo maeneo katika Tarafa ya Mgeta sehemu ya Maskati, Kanga, Kibati japo tayari Kibati wameanza jitihada hizo, tuliunganishe Jimbo la Mvomero kuwa na mawasiliano ya kutosha na kama nilivyosema wakulima wetu wanalima mazao mengi ya biashara, basi mkulima huyu awe na uhakika zaidi wa mawasiliano na kutafuta masoko kwa haraka zaidi kupitia simu ya mkononi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala zima la umeme. Jimbo la Mvomero lina tatizo kubwa la umeme na hasa Tarafa ya Mgeta. Hivi ninavyoongea ni kwamba Tarafa ya Mgeta kuna nguzo za umeme zilijengwa miaka 13 iliyopita imeishia eneo linaitwa Pekomisegese. Miaka 13! Namshukuru Marehemu Mainda alifanya jitihada za kutosha kupeleka nguzo mpaka pale, lakini mpaka sasa ninavyoongea Tarafa ya Mgeta sioni sababu kwanini wanakosa umeme.

Kwa kuwa swali hilo lipo, litajibowi, lakini nilitaka nitoe kama utangulizi, Serikali ifanye jitihada za haraka sana kuona kwamba mradi wa umeme unapelekwa Mgeta na maeneo mengine ya Kibati, Kanga, Maskati na maeneo mengine ambayo bado umeme haujafika kama Doma na Meleta.

Mheshimiwa Spika Nishati ya umeme ni jambo la muhimu sana ambalo ni kichocheo kikubwa cha uchumi. Ninaomba Serikali ichukue hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni maji. Ninaomba sana tutimize ile azma yetu ya kuona kwamba maji yanapatikana vijiji kwa asilimia 60, lakini kwa Jimbo la Mvomero bado kabisa.

Leo nashukuru kwamba Waziri wa Maji ametoa taarifa ya miradi inayoendelea katika Vijiji kumi, lakini kwa Mvomero taarifa nilizonazo ni kwamba maandalizi yaliyofanyika na yaliyoanza sasa ni kwa vijiji vitatu tu ambavyo ni Mvomero, Kichangani na Madizini. Lakini aeewe kwamba Jimbo letu lina Tarafa nne, miradi hii ya Benki ya Dunia itakapoanza, basi wafikirie kwamba miradi hiyo ilenge katika Tarafa nyininge kwa maana tunayo Tarafa ya Mgeta, Mlali, Mvomero na Turiani. Kwa sasa wameanza na Tarafa ya Mvomero na Turiani, lakini iendelee kwa Tarafa nyininge.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema kuhusu afya na elimu. Wilaya yetu ni mpya, ninaomba Wizara ya Afya ione jitihada za kujenga hospitali ya Wilaya ya Mvomero. Sisi hatuna hospitali ya Wilaya, lakini pia jitihada ziendelee kujenga zahanati kwa kila kijiji katika vijiji vya Jimbo la Mvomero.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni suala la elimu. Matokeo ya Kidato cha Nne, kila mmojawetu ni lazima asikitike. Lakini nasema, kila palipo na mafanikio ni lazima pawepo na changamoto. Kwa hiyo, tunaanzia na hilo kwamba tulithubutu na Serikali ilitekeleza vizuri ilani hiyo ya mwaka 2005/2010 kwa ujenzi wa sekondari kila Kata. Tusingejenga, wapinzani wetu wangesema hakuna Sekondari.

Kwa hiyo, kwa kuwa tumejenga, tatizo leo ni kufeli kwa wanafunzi Kidato cha Nne. Kwa hiyo, tunaanzia hapo kwamba mafanikio yoyote yana changamoto zake na lazima sasa tuangalie ni namna gani tunaweza kukabiliana na changamoto hizo, ikiwepo suala la uhaba wa walimu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. DR. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia kwa mara ya kwanza katika Bunge lako Tukufu.

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi na uhai, nawashukuru sana wazazi wangu Bwana na Bibi Ndugulile kwa kuwa mimi ndiyo uzao wao wa kwanza, mke wangu Magdalena na watoto wangu Melvin na Martha ambao wakati wa kampeni, baba hakuwa nyumbani akihangaini kwa ajili ya nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wanakigamboni kwa kuwa na imani na mimi kwa kunichagua kwa kura nyingi sana kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili Tukufu. Lakini vile vile napenda kuwatachia wanakigamboni wote na Wabunge wote *happy Valentine*.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Rais kwa hotuba nzuri ambayo inaonesha dira ya sehemu ya pili ya Awamu ya Nne ya Urais wa Dr. Jakaya Kikwete. Hotuba ya Rais imegusia vipaumbele 13, lakini ningependa kuishauri Serikali katika vipaumbele vyote 13 ijaribu kukaa na kuvipanga kwa uwiano.

Mhehsimiwa Spika, katika hili, kwa mtazamo wangu ningependa kwa umuhimu tujaribu kuangalia mambo matano. Moja, suala la elimu ambalo nitaligusia kwa kirefu, suala la utawala bora, afya, kilimo, masuala ya miundombinu ambayo yatakuwa yanagusia masuala ya umeme, barabara na mfumo wa mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwa undani kidogo nigusie kipaumbele Na. 4 ambacho ni suala la elimu. Wachangiaji waliopita wameongelea kwa kirefu na kwa kina sana kuhusiana na changamoto zilizopo katika elimu. Mimi sitakwenda tena kule ila nilikuwa natoa tu pongezi kwa Serikali, kwa sababu tumetoka miaka ya nyuma ambapo tulikuwa Shule za Sekondari chini ya sekondari 1,000, lakini ndani ya miaka mitano tumeshafikisha sekondari karibia 4,000. Nadhani Serikali inahitaji pongezi.

Mheshimiwa Spika, changamoto ni lazima iwepo. Unapokuwa na wingi na ubora, haviendi sawa. *You can not talk about quality when your looking of quantity hali ambayo imepelekea sasa tumeanza kuona baadhi ya changamoto katika matokeo ya kidato cha nne.*

Mheshimiwa Spika, nataka nijikite zaidi katika mapendekezo na kwa bahati nzuri nipo katika Kamati ya Huduma za Jamii kama Makamu Mwenyekiti, tutakaa tushauriane na wenzetu wa Wizara ya Elimu ili basi baadhi ya mambo tutakayoyagusia tuweze kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ninayo mapendekezo yangu kadhaa, nadhani sasa kutokana na hii *rapid expansion* ambayo tumekuwanayo, ni muda muafaka sasa tuanze kuangalia ubora (*the quality of education*) ambayo tunataka kuitoa katika shule zetu. Vile vile kuna umuhimu wa kuipa elimu kipaumbele na kutengewa fedha za kutosha ili basi tuweze kujenga Taifa la watu ambao wameelimika.

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu la tatu, tuboreshe mitaala iendane na mazingira ya sasa. Ni vizuri kwamba katika kila *level* watoto watakapokuwa wanahitimu tujaribu kuweka mle ndani *skills* za mtu ambaye anamaliza Darasa la Saba awe na *skills* fulani, mtu ambaye anamaliza *Form Four* anatoka na *skills* fulani na mtu ambaye anamaliza *Form Six* anatoka na *skills* fulani, hata mpaka anapokuwa anafika *University* awe anatoka na *level of some skills* ili basi hawa wengine ambao wanamaliza na wanakuwa hawana uwezo wa kuendelea, basi wakitoka pale waweze kwenda kujajiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe tena rai kwa Serikali kwamba mtihani wa Kidato cha Pili ilikuwa ni kiashiria ni jinsi gani watoto wanaendelea na uelewa wao. Naomba nitoe rai kwamba mtihani huu wa Kidato cha Pili urudishwe, itakuwa ni kipimo sahihi kuangalia mwelekeo wa mafunzo ambayo wanapata shulenii.

Mheshimiwa Spika, suala la tano, Walimu ndiyo wajenzi wa Taifa. Sisi wote ambaao ni wazazi tunaona changamoto ambazo tunazipata majumbani, watoto wetu tangu wanaanza kujifunza kuandika mpaka wanaweza wakafikia *level* ambayo tulikuwa nayo. Nadhani kwa kweli inabidi tuweke mikakati ya msingi na ya makusudi ya kuwaenzi walimu wetu kwa sababu wao ndio wajenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, vilevile nataka kutoa wazo lingine kwamba katika hili naomba kuangalia ni kwa jinsi gani tunaweza kushirikisha sekta binafsi. Huko siku za nyuma *Tanzania Education Authority* kulikuwa na taratibu kwamba sekta binafsi kuna watu walikuwa wanapata *tax relief* kwa kuchangia elimu. Nilidhani hili ni wazo zuri ambalo tunatakiwa kuboresha kwamba watu ambao wapo katika sekta binafsi wakichangia katika elimu, basi ule mchango wao uweze kuwa *recognized*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho katika suala hili la elimu, ningependa kugusia kwamba jamani sasa hivi shule michango imekuwa mingi na imekuwa kero. Tuangalie utaratibu wa kuhakikisha kwamba hii michango ambayo imekuwa kero na sasa hivi mtoto asipokuwa na Sh. 200/= *tuition* haruhusiwi kwenda shule. Hii niliipata hata pale Dar es Salaam, katika Kata zangu za Mbagala nimekuwa napata malalamiko makubwa sana. Uandikishaji umekuwa wa gharama, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana hili suala la michango shulenii tuweze tukaliangalia kwa kina.

Mheshimiwa Spika, katika suala la uchumi, kipaumbele cha tatu, cha nne na cha saba. Katika hili nitajikita kidogo katika suala la umeme. Nimepata faraja sana kusikia Mheshimiwa Januari Makamba anagusia na kwamba Kamati yake imeweza kuanza kazi mara moja. Napenda kuwapongeza sana kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatutaweza kuboresha uchumi, kukuza uwekezaji wala kuleta maendeleo katika Taifa letu kama hili suala hatutakaa tukalishughulikia kikamilifu. Katika hili mimi nilikuwa naomba sana tuache siasa, tuache malumbano, tukae tujikite kuangalia jinsi gani na kitu ambacho tunaweza kukifanya. Athari za tatizo la umeme ni kubwa. Kwa hiyo, ninaomba sana tukae tujipange tuhakikishe kwamba suala hili tunaliweka vizuri na ndani ya miaka hiyo ijayo kwamba hili tatizo liwe historia. (*Makofi*)

Kwa kuwa muda umebaki mchache, naomba nijikite moja kwa moja katika masuala ambayo yako katika Jimbo langu la Kigamboni. Kigamboni (*The New City*) ni Jimbo ambalo ndani ya miaka mitano kuna mipango mingi sana ya kutaka kuliboresha. Kuna mpango wa Mji Mpya. Lakini mpango huu umekumbwa na changamoto nyingi sana.

Moja, kumekuwa hakuna habari sahihi kuhusiana na mpango huu. *Government notice* ime-expire Oktoba mwaka jana na mpaka sasa hivi hakuna tamko lolote la Serikali. Sasa imetokea hali ambapo wananchi wameanza kujenga holela.

Namwomba sana Waziri mhusika kwamba hili suala tukae tujadili kwa sababu hawa watu wana haki sasa hivi kwa sababu *notice* yenu ime-expire. Kwa hiyo, tukae tuliangalie kwa kina na upana ili tuweze kukaa na kufikia muafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pili, wananchi wa Kigamboni wana nia njema na mradi na kwa kweli wanaukaribisha kwa mikono yote. Lakini changamoto kama nilivyosema hawana habari sahihi, wangependa kujua haki zao, stahili ni zipi na hatma yao ni ipi. Kwa wale ambao tutakuja kuwashamisha ingawa watu wanasema hawatahamishwa, lakini wangependa kujua kwamba kwa wale wachache watakaohamishwa, hatima yao inakwenda vipi, na kwamba kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa ushirikishaji wananchi wa Kigamboni jambo ambalo linaweza likakwamisha maendeleo ya mradi huu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Wizara tukae kwa pamoja tuainishe maeneo ambayo yana upungufu ili basi tukitoka hapa twende kwa pamoja.

Lakini vile vile kumekuwa na suala la daraja ambalo limekuwepo katika ilani mbili za uchaguzi. Hili nilikuwa naliomba na Serikali ijaribu kuliangalia ili ujenzi wa daraja la Kigamboni uweze kuanza. Kwa sababu Mji wa Kigamboni sasa hivi unapanuka kwa haraka sana na vivuko vilivyoko kwa sasa hivi havitoshelezi, ndio suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Spika, mwisho namalizia kwa kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adhimu na mimi kwa mara ya kwanza tangu niingie katika Bunge lako Tukufu napata fursa ya kuchangia hotuba ya Rais siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, niwashukuru vijana wenzangu wa Mkoa wa Mara kwa kuona kati ya mionganini wa vijana wao ambao wanafaa kuja kuwashukuru katika Bunge hili Tukufu, lakini pia kwa heshima na taadhima, napenda kuwashukuru wajumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Vijana la Taifa, kwa kunipa ridhaa hii na Chama changu cha CCM kikaona na mimi niwe mionganini mwa makada wake waliopelekwa kwenye Tume ya Uchaguzi na hatimaye kuwa humu katika kushirikiana na Wabunge wengine tuweze kusukuma gurudumu la maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kukupongeza wewe ukiwa kama mwanamke mwenzetu kwa kupata nafasi hiyo kubwa ya kuwa Spika wa kwanza katika nchi yetu

mwanamke ambaye leo hii kwa kweli nafasi yako inafanya wanawake wote tuweze kujivunia humu ndani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda kuwapongeza Wabunge wote vijana bila kujali itikadi zao ambao wameleta mabadiliko katika Bunge lako la Kumi kuwa na vijana wengi na wengi wao wakitoka Chama cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kujikita katika suala zima la ajira. Tunajua suala zima la ajira ni tatizo kubwa katika nchi yetu. Tunajua Serikali imejitahidi katika kipindi chake cha miaka mitano, kimeweza kutengeneza ajira milioni 1.2. Katika ajira hizo milioni moja ni ajira ambazo zisizo rasmi, ajira za wafanyabiashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ziweze kutengeneza ajira laki mbili ambazo ndizo ajira rasmi. Ningependa kusema kwamba hizi ajira milioni moja kwa vijana wetu au Watanzania ni ajira ambazo hazina *future*. Hawajui *what next*. Ni ajira za wafanyabiashara ndogo ndogo. Kwa hiyo, mbali na kujitolea kupata mikopo na kuweza kuanzisha ajira hizi zisizo rasmi, ni wakati muafaka Serikali ingeweza kutoa elimu ya ujasiriamali na kuwawezesha wafanyabiashara ndogo ndogo *ku-improve*, mitaji yao iweze kukua na waweze kufaidika na hii mitaji ambayo wameianzisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia ni wakati muafaka kwa Serikali kuona kuna umuhimu wa kuwa na vyanzo vingi vya ajira ikiwepo na kufufua viwanda vyetu ili hizi ajira ambazo sizo rasmi zigeuke kuwa ajira rasmi na vijana/Watanzania wetu wawe na uhakika wa kupata kipato cha uhakika.

Mheshimiwa Spika, nikiongelea suala zima la ajira, kila mwaka vijana laki saba wanaingia katika soko la ajira. Lakini kati yao ni 50,000 ndio wanafanikiwa kupata ajira. Hii ni kwa sababu sekta binafsi hazitoi mchango wa ajira katika nchi yetu kiuhakika. Ni wakati muafaka wa Serikali kushirikiana na sekta binafsi kuona ni njia gani sahihi watakazowea kuisaidia Serikali yetu ya Tanzania na wazalendo wetu kupata ajira rasmi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ningeomba nitolee mifano michache tu, kwa nini wenzetu wa Kenya waliweza kufanikiwa? Kwa upande wa mahoteli, wenzetu nchi ya Kenya akija mgeni kufanya uwekezaji katika nchi yao, Meneja Mkuu atakuwa mgeni, lakini Meneja Msaidizi na *department* nyingine wanakuwa wazawa. Hivyo basi, yule mwekezaji anapomaliza muda wake wale wenyeji wana-take place na kuweza kuajiri wenzao zaidi. Hivyo, baada ya kuendelea kutengeneza ajira za watandika vitanda, wafagizi kwenye mahoteli, na wazawa wapate nafasi za kuweza kuajiriwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nizungumzie suala zima la vijana wenzetu wasanii ambao wameonyesha vipaji vyao na kuajiri wenye. Kumekuwa na malalamiko mengi sana ya wizi wa kazi za wasanii. Wabunge wenzetu wakiwemo Mheshimiwa Martha Mlata, waliweza kuongelea katika Bunge lililopita. Lakini tatizo hili bado ni sugu na Serikali bado haijapata njia mbadala ya kuhakikisha inatatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Uganda, nchi jirani wameweza kufanikiwa kutatua tatizo hili. Kwanza kabisa, Redio ya Serikali iko *committed* katika *ku-promote* kazi za wasanii. Vilevile katika Serikali kuwe na kitengo maalum kitakacho-deal na kazi za kusimamia kazi za wasanii pamoja na kusambaza na kuhakikisha hawaibiwi tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ili msanii aweze kuwika, anahitaji kupata *promotion* mbalimbali. Lakini pia kuna vipindi mbalimbali kwa mfano, *Border to Border, Top Ten, Top Twenty*, vile vipindi vinakuwa na matangazo mengi. Lakini msanii hanufaiki na yale matangazo zaidi ya wimbo wake kupigwa. Mimi nadhani ni wakati muafaka Serikali kushirikiana na Redio nyagine binafsi kuhakikisha wasanii hawa wanafaidika na kupigwa nyimbo zao redio na kazi zao kwa sababu kati ya vijana ambao wanaitangaza nchi yetu ni wasanii wa kizazi kipyä, wasanii wa filamu ambao tumeona wameshirikishwa wananchi mbalimbali. Juzi tu hapa Ali Kiba alipata fursa ya kuimba na mwanamuziki Mkongwe R. Kelly, lakini pia akina Kanumba tumeona wanavyoitangaza nchi yetu kwa kuweza kufanya kazi na wasanii mbalimbali wa nchi jirani kama Uganda. (*Makofi*)

Lakini pia, ningependa kuzungumzia suala la *Machinga Complex*. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuona kuna dhamira ya dhati ya kujenga majengo mengine kama vile Mkoa wa Mwanza. Lakini napenda kutoa angalizo kidogo kwamba haya majengo yanapojengwa yanamlenga Machinga hasa yule ambaye anazunguka katika Mitaa kutafuta riziki.

Lakini lazima tuweke utaratibu utakaomwezesha huyu Machinga halisi kupata nafasi katika majengo husika. Bila hivyo tutakuwa tunajenga majengo lakini walengwa hawatafaidika na majengo hayo kutokana na kutozwa kodi kubwa na matokeo watakaoweza kwenda katika yale majengo ni wafanyabiashara wakubwa na hawa wanaendelea kuranda mtaani ili waweze kupata chochote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ningependa kuongelea suala zima la umoja wa kitaifa. Kwanza kabisa, ningependa kuwashauri Wabunge wenzangu vijana ambao tumebahatika kuingia katika Bunge lako leo, kwamba tuna jukumu moja la kujenga nchi yetu bila kujali itikadi zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna *trend* ambayo inaendelea sasa hivi, baadhi ya Wabunge wenzetu wamekuwa wakichochea migomo na maandamano. Mimi nadhani kijana jasiri ni mwenye uwezo, anayeweza ku-address issues zake kwa *proper channel*. Hivyo basi, tujaribu kufuata misingi iliyoachwa na Baba wa Taifa ambaye aliweza kupigania uhuru wa nchi yetu bila kumwaga damu, ndivyo vijana wenzangu viongozi tunapaswa kufanya hivyo. Tuna jukumu la kujenga nchi yetu. Lazima tuwe na maswali ya kujibu tutakapoulizwa na vizazi vingine: Je, ninyi leo hii mmetengenezewa mazingira ya nchi ya amani, lakini hii *trend* ambayo tunakwenda nayo ya kutengeneza migomo, maandamano tutakapofanikiwa kuingia madarakani katika kizazi hiki hatutaweza kuwaambia sasa acheni tumepata nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuwashauri vijana wenzangu tufanye kile kitu ambacho Watanzania wanakihitaji tuweze kuibana Serikali, tuweze ku-*address issue* za msingi ambazo Watanzania wanahitaji. Kwa mfano, matatizo ya umeme, matatizo ya ajira kwa vijana wenzetu, matatizo mbalimbali ya maji wakiwemo na wananchi wa Bunda na Mkoa wa Mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kama tutakuwa tunatembea vyuoni kuhamasisha migomo, hatutaweza kutengeneza Tanzania imara na yenye ujuzi. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kwa kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Lakini vilevile kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kuchangia hoja rasmi za Bunge, nichukue nafasi hii pia kuwashukuru kwa dhati kabisa wananchi wa Jimbo langu la Kawe ambaao wameonyesha uaminifu wao mkubwa na imani yao kwangu ya kuniwezesha kufika hapa. Ninawashukuru wananchi wote pasipo kubagua vyama, vyama vyote vilinipigania na mimi niko hapa Bungeni. Kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri ambaao wengi ni wakazi wangu, tujisikie huru kujenga Jimbo letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikupongeze na wewe kwa dhati kama mwanamke wa kwanza kuwa Spika na ninaamini kwamba utakidhi matarajio ya wengi kwa sababu ni utamaduni kwamba anapopewa mwanamke fursa, watu wengi wanakuwa na *question mark*, wanajiuliza: huyu ataweza? Sasa mimi naamini unaweza. Nilikuamini ukiwa Naibu Spika, na naamini hiyo *negative perception* ambayo baadhi ya watu wanaweza wakawa nayo utaikidhi vinginevyo kwa kuliendesha Bunge letu katika hali ya ustaarabu wa kufuuta kanuni. (*Makofi*)

Lakini pia nampongeza Mbunge kijana mwenzangu aliyetangulia kwa ukomavu aliounyesha, ukizingatia ndio mara yake ya kwanza kuzungumza, na jirani yake pale, hakika tukienda hivi tutafika. Kwa sababu nchi hii ndio tunakuja kuichukua sisi. Hawa wazee ndio inafika alasiri. Kwa hiyo, tukienda vizuri tutakuja kuiongoza nchi yetu vizuri sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Uzee dawa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nianze na suala la elimu. Nitachangia kwa uchache kwa sababu limeshajadiliwa sana. Leo asubuhi nilikuwa nina swali kwa Wizara ya Elimu. Kumekuwa kuna tatizo la kimsingi ambalo Serikali inabidi ama ilitolee ufanuzi, bila kufanya hivyo, tutajikuta kwamba watu wetu kule chini wanakumbwa na mzigo usiokuwa na tija. Tunajua kwamba elimu ya msingi ni bure. Lakini kwa mzazi ye yeyote ambaye anapeleka kumwandikisha mtoto wake katika hizi shule zetu ambazo ziko chini ya Serikali za Vijiji/Mitaa asipokuwa na kazi ya Sh. 20,000/= mpaka Sh. 50,000/= haandikishi mtoto. Sasa Kamati za shule zimepewa mamlaka ambayo mipaka yake haifahamiki. Sasa ili kuondoa huu utata ningeomba

Serikali itoe maelekezo ili wananchi kule chini wajue wanatakiwa watoe michango kiasi gani katika kusaidia maendeleo ya shule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu katika hizi shule zetu zamani faida kubwa iliyokuwepo ni kwamba tulikuwa tunachanganyika madaraja yote katika hizi shule. Sasa hivi sisi wenye vipato vya katikati na wenye vipato vya juu tunakwenda kwenye shule za *private*, shule ambazo zina fursa chanya. Hawa huku ambao ama ni walinzi ama ni mama Ntilie ama ni wavuvi wadogo wadogo wao ndio wameishia kusoma zile shule ambazo sisi tulikuwa tunasoma zamani. Matokeo yake huyu maskini wa kawaida amerudishiwa mzigo mzito wa kuziendesha Shule za Serikali.

Sasa naomba uwepo utaratibu, kwa sababu hizi shule zimerudishwa Serikali za Mitaa, tunakumbuka miaka ya 2004/2005 Serikali ilifuta kodi za maendeleo ambazo zilikuwa ni vyanzo vya mapato ya Serikali za Mitaa. Nakubaliana na ile hatua iliyochukuliwa. Lakini ilichukuliwa kwa makubaliano kwamba Serikali itatoa ruzuku kwenye Halmashauri, kwenye Serikali zetu za Mitaa ili hizo ruzuku zishuke kule chini asilimia 20 ziwezeshe Serikali zetu za Mitaa kuijendesha, kujifanya hizi shughuli zetu za maendeleo ambazo zinajumuisha pia kuendesha hizi shule.

Ripoti za *CAG* kila mwaka zinaonyesha kwamba asilimia 20 hazirudi. Mimi natokea Jimbo la Kawe, Jimbo la Mjini pale pua na mdomo na Ikulu, asilimia 20 hairudi. Matokeo yake, Serikali zetu za Mitaa hazina fedha. Viongozi wa Serikali za Mitaa tunaowachagua kwa kuwa hakuna fedha, wananchi wanatozwa kupata huduma za msingi ambazo kimsingi ni bure. Sasa mimi nilikuwa naomba hili liangaliwe kwa umakini.

Lakini vilevile Waziri wakati ananijibu, amezungumzia suala la *capitation grants*, kwanza zinakwenda kule chini. Hii ni *theory*. Tunapokuja kwenye uhalisia kinachokwenda kule ni kiduchu na hakifiki kwa wakati. Mimi nimetembelea shule zangu ambazo ni *reflection* ya shule nyingine Tanzania, fedha ya mitihani Serikali inapeleka miezi mitatu, mitatu; shule moja iko Kunduchi Sh. 16,000/= ya mitihani kwa mwezi. Kwa miezi mitatu inakwenda kama Sh. 52,000=/. Ukija kuangalia gharama halisi za mitihani, nazungumzia kipengele kimoja hapa, sijagusa ukarabati na mambo mengine Sh. 700,000=, shule yenye watoto 800. Maana yake, salio hilo Sh. 700,000= toa Sh. 52,000= analipa mlinzi. Sasa Serikali mimi ninadhani kuna haja ya kuangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la ualimu ni tatizo kubwa. Mheshimiwa Mbunge wa Kigamboni aliyepita amezungumza shule binafsi kuchangia. Ripoti za *CAG* kila mwaka zimekuwa zikisema Serikali inatumia fedha nyingi kusomesha walimu, madhumuni yakiwa hawa walimu waende wakasaidie shule zetu za Kata za watoto masikini. Lakini matokeo yake walimu wanatosmeshwa wanakwenda kwenye shule za *private* za vigogo, hawa watoto wetu huku chini wanabaki bila walimu.

Sasa Serikali ingeanzisha utaratibu kwamba shule binafsi ambazo zinachukua walimu ambao wanatosmeshwa na kodi za Watanzania na wao kwa kiasi fulani wasaidie

kuwezesha kuisaidia Serikali kusomesha walimu wengi zaidi ili tuweze ku-*balance*. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba tuliangalie hili na linawezekana.

Mheshimiwa Spika, tuna uhaba mkubwa sana wa walimu wa sayansi. Bunge lililopita tulipitisha Itifaki ya Soko la Pamoja na moja kati ya vipengele ni kuweza kubadilishana ama kuruhusu walimu wa sayansi waweze kutoka kwenye nchi za wenzetu kuja kutusaidia kufundisha. Sasa wakati tunatoa zao la wanafunzi wanaopata *zero* na *division four* asilimia 88, tungeweza kuangalia ama tuahirishe hili zoezi wakati tunatengeneza walimu wetu ndani, walimu wakamilika wale warudi makwao, lakini hapa katikati tunakuwa tumeondoa muda wa kutengeneza watoto ambao ni mambumbumbu.

Mheshimiwa Spika, *division zero* na *division four* ndiyo wako mtaani, kwa hiyo, naiomba Serikali, hizi fursa za Afrika Mashariki tuzitumie pale inapobidi, pale ambapo haibidi tutawaacha waondoke. Hatuwezi kuruhusu watoto wetu wapate daraja la sifuri wakati tunaweza tukaazima walimu kwa kipindi fulani wakati watoto wetu wanaendelea na sisi tunasomesha watoto wengine wakakidhi zile nafasi baadaye wakaja wakaziziba. Hilo ni lingine.

Mheshimiwa Spika, lingine, hili ni tatizo la Jimbo langu, Chuo Kikuu cha *IMTU*, wanatoza fedha....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Oh, pole sana. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Stephen Ngonyani na Mheshimiwa Felister Bura ajiandae, nafikiri ndio wa mwisho.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuingia kwenye Bunge Tukufu. Pili, napenda kuwashukuru wananchi wa Korogwe Vijijini kwa kuwa na mimi na kwa kunichagua kwa kura nydingi sana. Tatu, nataka niwashukuru waganga wa tiba za jadi Tanzania nzima. (*Makofii*)

**SPIKA:** Huyo anaitwa maji marefu, maji marefu, eeh. (*Kicheko*)

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniunga mkono. Pia nataka niwashukuru Chama cha Mapinduzi, Mkao wa Tanga pamoja na Korogwe Vijijini kwa kuniona kwamba nafaa na leo hii nawakilisha wakulima wenzangu. Nitachangia katika sehemu tatu tofauti au nne hivi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza, ni sehemu ya kilimo; kwa sababu Serikali imeamua kwamba kipaumbele ni kilimo kwanza. Katika Jimbo langu kuna Bonde la Mto Mkomazi, Bonde hili la Mto Mkomazi likitengenezwa bwawa la kuhifadhi maji, tunaweza kupata chakula cha mwaka mzima na ikalisha Mkao wa Tanga, Kilimanjaro na Mkao wa Pwani. Ningombaa sana Serikali iangalie sana ili bwawa la Mto

Mkomazi kwa sababu kuna wakati lilitakiwa lianzishwe, lakini kilichotokea sijui na mpaka sasa hivi ukame umekuwa mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, katika Wilaya yangu nimezungukwa sana na mashamba ya mkonge. Haya mashamba yamewafanya wakulima wa Korogwe Vijiji ni kukosa kabisa sehemu za kulima. Ningombwa haya mashamba ya mkonge sasa hivi hayalimwi, yamekuwa ni msitu tu na ukizingatia kwamba eneo langu watu wengi ni wakulima, hawana sehemu za kulima. Naiomba Serikali ifute hati miliki ya mashamba haya na baadhi ya mashamba ni kama Shamba la Kwa Shemshi, Shamba la Magoma, Shamba la Hale, Shamba la Mbwazi, Shamba la Toronto, Shamba la Mswaha Darajani na mashamba mengine yamezuia eneo kubwa sana, wananchi wanapata shida sana na ukizingatia kwamba asilimia kubwa la wananchi wa Korogwe Vijiji wote ni wakulima.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, ni suala la maji. Utashangaa sana katika Jimbo langu kuna Makao Makuu ya Tarafa mpaka leo hii hawana maji safi. Suala la maji limeathiri kwa kiwango kikubwa sana Jimbo langu ukizingatia katika Tarafa ya Bungu kuna Vijiji zaidi ya 20 havina maji hata tone. Naomba Serikali iangalie suala la Bungu, kuna matatizo ya maji, katika Kata ya Mashewa, kuna sehemu ya Bombo Majimoto, sehemu ya Kulasi, sehemu ya Lusanga, sehemu ya Makunga na sehemu ya Vingo hawa watu wanakunywa maji yanayopita mferejeni na huko mferejini watu wanaoga, watu wanafanya kila aina ya shughuli, matokeo yake kunakuwa na magonjwa kila wakati.

Mheshimiwa Spika, vile vile nina suala la umeme. Katika Jimbo langu kuna Vijiji vingi havina umeme, lakini nguzo za umeme zimepita katika Vijiji hivyo, nashangaa wenzetu sehemu nydingine umeme unapatikana, lakini lah, katika Wilaya ya Korogwe Vijiji kuna Kata nydingi hazina umeme. Kata hizo ni Kata ya Kerenge, ukichukulia Kijiji cha Kerenge Kibaoni, Matalawanda, Alhamisi mpaka Makumba hakuna umeme. Katika Kata ya Dindila kuna Kata ya Dindila yenyewe, Mugwashi, Mhale, Mali, vijiji vyote havina umeme. Sasa nashangaa na nguzo zipo karibu kabisa, naomba Serikali iangalie suala hili hasa safari hii ukizingatia nimekuja mimi mkulima. Muwaangalie na muwape kipaumbele sana wakulima.

Mheshimiwa Spika, suala la mawasiliano, napenda kukuhakishia katika Wilaya ambayo haina mawasiliano ya simu kabisa ni Wilaya ya Korogwe Vijiji, Makao Makuu ya tarafa mpaka leo hii watu mawasiliano hawayapati na ukichunguza ndiyo kwamba ndiyo sehemu kubwa ambapo kunatoka vyakula mbalimbali ambavyo vinapelekwa katika Mikoa mbalimbali, hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam, Tanga na Kilimanjaro. Unashangaa kuona kwamba katika Tarafa ya Bungu, Makao Makuu ya Tarafa hakuna mawasiliano ya simu ya aina yoyote, lakini ukienda sehemu nydingine nydingi unakuta mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, ukienda katika Kata ya Mkalamo unakuta kule hakuna mawasiliano, wakati mifugo mingi inatoka kule na wafugaji wanaleta mifugo kwa ajili ya minada na watu leo hii Dar es Salaam wanakula nyama kutoka katika Kata hizo. Ukienda Kata ya Kizara ambako kunatoka wakulima wengi wa mpunga, mahindi pamoja na mazao mbalimbali na embe, lakini hawawi na mawasiliano ya simu na Mbunge aliyejipa

alishazungumza hili, lakini nashangaa halijafanyiwa utafiti wa aina yoyote na kupata ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana masuala kama haya wayashughulikie kwa sababu nawajali sana wakulima na safari hii nimekuja mkulima. Kwa hiyo, naomba Serikali inione vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, ukichukulia masuala ya miundombinu, katika Jimbo langu hakuna barabara ambayo inapitika wakati wote, sasa naiomba Serikali kwa sababu kule ndiyo kuna wataalamu wa kulima chai, iliki, kahawa, mahindi, mpunga na maharage. Hizi barabara zitengenezwe kwa mfano, barabara ya kutoka kwa Shemshi kwenda kwa ndugu yangu Januari haipitiki kabisa na ndiko yanakotoka maharage na majani ya chai kwa wingi. Naomba Serikali hizi sehemu iziangalie sana.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana na Bunge lako hili Tukufu, lakini nitashukuru sana kama watanisaidia kwenye masuala ya hospitali na zahanati na vituo vya afya, lakini vituo hivi vya afya havina huduma za kutosha, havina Madaktari na kama wapo ni wachache na watu wanapata shida mno na vituo hivi ni Kituo cha Mombo, Kituo cha Bungu na Kituo cha Magoma. Wako wagonjwa wengi wanaotoka katika hizi Tarafa, lakini kupata huduma inakuwa ni muda mdogo sana kufuatana na uchache wa Madaktari.

Sasa naiomba Serikali, hivi vituo vya afya waviangalie kwa makini sana ili na mimi nisiwe Mbunge wa mwaka mmoja, watakaponipelekea huduma hizi itakuwa ni vizuri zaidi na mimi nitafanikiwa sana.

Mheshimiwa Spika, nataka nimalizie kwa kuwashauri Wabunge wenzangu wanapochangia hoja zao wasituchanganye na sisi Waganga wa Jadi katika kila wanachoongea wasitufananishe na waganga, kwa sababu kila mtu na fani yake na kila mtu na imani yake. Kama imani yako haikuruhusu mambo ya uganga, lakini msituizingize kila mahali mnatudonoadonoa, tunakerwa sana na hili. Kwa sababu kila mtu ana fani yake hapa ndani, sasa na mimi fani yangu ni miti shamba. Mnapokuwa mnatufananisha tunadharaaulika kiasi fulani, naomba Waheshimiwa Wabunge na hili nanyi mlione.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya machache, ahsante sana. Napenda kuunga mkono hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Rais. (*Makofî*)

**SPIKA:** Mimi Spika sikusikia kama wanawadharau. Haya tunaendelea na Mheshimiwa Felister Bura, wiki yote tulikuwa tunakutafuta huonekani. (*Kicheko*)

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bunge lako Tukufu, lakini kwanza nimshukuru Mungu kwa kunipa nafasi ya kuwa mzima na kuwa na afya njema na pia nawashukuru wanawake wote wa Mkoa wa Dodoma walionipigia kura kwa mara nyingine na kuwa na imani kubwa kwangu kwamba tutasaidiana katika kuleta maendeleo ya wanawake wa Mkoa huu.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana kwa kupata nafasi ya kuwa Spika, sisi Wanawake wa Tanzania tunatembea kifua mbele kwamba wanawake tunaweza, tena pasipo kuwezeshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda ni mfupi, naanza kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri sana aliyoitoa siku aliyofungua Bunge hili. Alitoa vipaumbele 13 na niseme kwamba vipaumbele nya Rais havitaweza kukamilika au havitakuwa na maana kama Watanzania hatutamuunga mkono. Tunatakiwa kumuunga mkono Rais wetu, kwa yale yote aliyoyasema kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania, wafanyakazi wamuunge mkono kwa kufanya kazi kwa bidii maofisini na nadhani uwepo muda sasa wa kuweka *performance* kwa wafanyakazi. Kwa sababu kama tunapanga mipango ya nchi na wafanyakazi hawaoneshi *performance*, hatutafika mbali.

Mheshimiwa Spika, ufile wakati kila mmoja aonyeshe kazi yake anayofanya kwa mwaka ni kazi gani. Je, amefikia malengo? Kama hajafikia malengo basi achukuliwe hatua. Vinginevyo tutabaki tunaimba vipaumbele nya Rais, tunasimamia uchumi wa nchi, lakini kama hakuna juhud za makusudi zitakazofanywa kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanatimiza malengo yao hatutafika. Wafanyakazi pia nawahimiza pia kumuunga Rais mkono, wanafunzi, sisi Wabunge wanasiasa, asasi zisizo za Kiserikali, wajasiriamali kila jambo linawezekana iwapo kila mmoja atatimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la maji. Sisi Mkoa wa Dodoma ni Mkao mkame na sio kwamba tunapenda kuishi katika Mkao wa Ukame, lakini ndivyo Mwenyezi Mungu alivyoamua kuwa Mkao wa Dodoma ni Mkao kame. Tunapata mvua kwa kipindi cha wiki mbili tu, baada ya hapo hatuna mvua. Kwa hiyo, wanawake wanabaki wanahangaika mitaani, wanahangaika vijijini, wanatembea mwendo mrefu kutafuta maji na watoto migongoni, hawana shughuli zingine za kufanya kwa sababu ya kutafuta maji, wanashindwa kufanya shughuli zingine za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba suala la visima nya maji, visima vifupi na visima virefu vitazamwe kwa jicho la huruma kwa Mkao wa Dodoma. Tuna shida mno na kila mwaka tunapiga kelele juu ya visima nya maji kwa Mikoa yenye shida ya maji, Mikoa yenye ukame. Naomba hili likatazamwe.

Mheshimiwa Spika, pia Rais ameongelea sana suala la afya na mimi nampongeza kwa kumleta Tanzania Daktari wa *nerves* duniani. Jamani tumpigie makofi Rais wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania sasa tutakuwa nchi ya kwanza kwa Afrika Mashariki na Kati kuwa na Madaktari wengi wa nerves, ni zaidi ya Madaktari 60 kama tulivyoelezwa katika miezi tu michache iliyopita. Kwa hiyo, nina imani kwamba muda si mrefu tutakuwa na Madaktari wengi ambao watatusaidia katika vituo vyetu nya afya. Lakini Mheshimiwa Rais, pia amesema ataongeza Wauguzi, vifaa tiba na kadhalika. Hebu naomba Wizara ya Afya itukumbuke sisi wana Dodoma kwa sababu hospitali yetu ya Mkao imezidiwa, idadi ya wakazi imeongezeka kwa kipindi kifupi sana, hospitali ya

Mkoa haijaongezewa watumishi. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Afya itusaidie kuongeza watumishi pale Hospitali ya Mkoa na pia vitendea kazi vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, hata Wilaya yetu ya Bahi ni Wilaya Mpya haina wauguzi wa kutosha, haina Madaktari wa kutosha, haina vifaa tiba vya kutosha, naomba Wizara ikaliangalie kwa jicho la huruma. Katika Wilaya yetu ya Bahi, wanawake wanapata tabu, watoto wanapata tabu, hii itatusaidia kupunguza vifo vya watoto na akina mama wajawazito tutakapovipata vifaa vya kutosha na madawa ya kutosha. Nina imani na kwamba, Rais wetu atalitimiza alilolisema kwamba vifaa tiba tutavipata pamoja na Wauguzi na Madaktari wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala la kilimo. Tuna sera ya mwaka 2006 ya kuendeleza program ya kilimo, lakini pamoja na juhudzi za Serikali, kuna vyuo vyetu vikuu vinavyofanya utafiti huu wa mazao. Mazao haya yanayofanyiwa utafiti hayafiki kwa wakulima jamani. Utafiti huu unaishia kwenye vitabu tu haufiki kwa wakulima. Naomba utafiti huu ufile kwa wakulima jamani. Wakulima bado wanalima mazao ya miaka 1990, 1980, mazao yale ya miezi sita shambani. Kwa hiyo, tunaomba utafiti unaofanywa na vyuo vyetu vya kilimo, mazao hayo ya utafiti yawafikie wananchi ili kubadilisha mazingira na kubadilisha kilimo chetu kiwe cha kisasa zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia dirisha la kilimo, benki ya kilimo. Dirisha hili litakuwa Dar es Salaam, lakini Dar es Salaam hakuna wakulima, wakulima wako Mikoani. Hebu tuangalie namna ya kuwa na Dirisha la Kilimo katika Mikoa yetu ili wakulima wapate mikopo kwa karibu zadi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hebu fikiria mkulima ametoka Bahi, Kondo, Kagera au Ruvuma kwenda kutafuta mkopo Dar es Salaam na anapofika kule kuna masharti mengine ambayo anafika kule hayajui. Kama dirisha la kilimo litakuwa Mikoani, litawasaidia wananchi kwa karibu zaidi. Naomba Benki ya Kilimo wawe na dirisha katika Mikoa yetu. kilimo kwanza hatutakifikia kama wakulima hawataweza kukopa na kama pembejeo havitawafikia wananchi kwa wakati unaotakiwa na kama mazao yanayofanyiwa utafiti hayatawafikia wakulima. Lakini pia suala la soko la mazao lifanyiwe utafiti.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie suala la amani na utulivu nchini kwetu. Tanzania ni nchi ya mfano kwa jirani zetu, Tanzania ndiyo kimbilio la majirani zetu wanapogombana, Tanzania ndiyo kipoozeo kwa nchi ambazo ni jirani zetu. Lakini sasa hivi karibuni kumetokea mambo ya ajabu sana, Watanzania hawajui milio ya bunduki, Watanzania hawajui kuchimba handaki kama mtu hakwenda jeshini, lakini sasa Watanzania tumefikia hatua ya kuwa na wasiwasi wa kuishi, unatamani usitembee barabarani.

Mheshimiwa Spika, nawakemea wale ambao wanatafuta uongozi kwa kuwarubuni Watanzania kufanya maandamano, washindwe. Damu ya Watanzania iliyomwagika iwe juu yao, Mungu aidai juu yao, kwa sababu wale hawajui kitu, wale

waliokufa walijienda tu. Maeneo yote ambayo Watanzania wamemewaga damu kwa ajili ya mambo ya kisiasa, kwa ajili ya watu kutaka madaraka kwa nguvu kwa maandamano, damu hiyo Mungu aidai juu yenu.

Mheshimiwa Spika, niongelee sasa suala la jiografia. Tanzania ni lango la biashara kwa Afrika Mashariki na kwa Afrika ya Kati. Kuna haja ya kuimarisha Bandari zetu, maana mazao hayawezi kufika kwenye soko kama barabara hazipitiki. Kwa hiyo, tuimarishe barabara zetu, Bandari zetu na Reli (*TAZARA*, Reli ya Kati). Reli ya Kati imesuasua muda mrefu, tuone namna ya kuimarisha Reli. Pia ATC, nchi yetu haina ndege, aibu nchi kukaa bila ndege hata inayotembea ndani ya nchi yetu, jamani tunakwenda wapi? Ebu Wizara inayohusika angalieni namna ya kuimarisha ATC na namna ya kuimarisha Reli zetu ili wananchi waweze kusafiri kwa usalama.

Mheshimiwa Spika, ahsante naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa muda umekwisha na nina matangazo machache. Kwanza *party caucus* ya Chama cha Mapinduzi wanatakiwa kukutana kule kwa Pius Msekwa. Halafu kuna watu hapa wanajiita Wabunge Vijana wa CCM walio chini ya miaka 45, wanaombwa kukutana kwa muda mfupi kwenye Ukumbi wa Pis Msekwa baada ya Kikao cha Bunge jioni leo sio saa hizi, jioni. Baada ya kikao cha jioni hawa jamaa wa miaka 45 na kushuka chini wanaotoka Kambi ya CCM watakutana huko.

Leo jioni nitafikiwa na Mheshimiwa Spika, wa Bunge la Afrika Mashariki, atakuwa mgeni wangu leo jioni. Kwa hiyo, naomba Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu saa mbili jioni tushirikiane na huyu mgeni pale Dodoma *Hotel*, kadi zitakuja lakini natoa taarifa. Saa mbili jioni tushirikiane na mimi na mgeni huyo pale Dodoma *Hotel*, Spika wa Bunge la Afrika Mashariki. Now, simuoni Mheshimiwa Rage tunampongeza kwa ushindi wa Simba huko Comoro.

Baada ya kusema hivi, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja, kama nilivyosema kuna uchaguzi.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wakati nasitisha shughuli za Bunge kipindi cha asubuhi nilikuambieni leo tutakuwa na mgeni Mheshimiwa Spika wa Bunge la Afrika Mashariki ambaye amekuja kututembelea na amefika mchana huu, anaitwa Mheshimiwa Abdulrahim Abdi, Spika wa Bunge la Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, karibu sana katika Bunge hili. Nadhani ameambatana na baadhi ya Wabunge wa Bunge hilo. Namwona Mheshimiwa Mwinyi na Mheshimiwa nadhani yuko mbali, Mheshimiwa Mmari, *okay!* Lakini tutakuwa na mazungumzo nao kesho, kwa hiyo jioni walipofika wakaona nyie mnaendelea hapa, kwa nini wasishiriki na

nyinyi kuliko wakae hotelini tu. Kwa hiyo karibuni sana, nawakaribisheni sana. Ahsante.

### **UCHAGUZI WA WAJUMBE WA TUME YA UTUMISHI WA BUNGE NA MJUMBE WA APRM**

**NDG. JOHN JOEL - KATIBU MEZANI:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowatangazia siku ya Jumatano tarehe 9 Februari, mwaka 2011 na Jumapili tarehe 13 Februari, leo Jumatatu tarehe 14 kama inavyoonyesha kwenye *Order Paper* kuwa kutakuwa na uchaguzi wa Wabunge watakaoliwakilisha Bunge kwenye Tume ya Utumishi wa Bunge. Muda wa mwisho wa kurudisha fomu za kuomba uteuzi ilikuwa ni Jumapili tarehe 13 Februari, mwaka 2011 saa 10 jioni. Muda huo ulipofika Wabunge walikuwa wamejitokeza kuchukua na kurejesha fomu ni 14 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mheshimiwa; wa pili ni Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo; wa tatu ni Mheshimiwa Maua Abed Daftari; wa nne ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed; wa tano ni Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye; wa sita Mheshimiwa Salehe Hamad Pamba; wa saba ni Mheshimiwa Mhonga Said Ruhanywa; wa nane ni Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya; wa tisa Mheshimiwa Kidawa Hamad Saleh; wa kumi Mheshimiwa Abdulkarim Ismail Hassan Shah; wa kumi na moja Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo; wa kumi na mbili Mheshimiwa George Boniface Simbachawene; wa kumi na tatu Mheshimiwa Magale John Chibuda na wa kumi na nne Mheshimiwa Godfrey Zambi.

Sasa kwa mujibu wa Sheria ya Uendeshaji Bunge Na. 14 ya mwaka 2008 kifungu cha (12)(2)(e) inachanganua nafasi hizi saba ambazo zinagombaniwa ni kama ifuatavyo:-

Ni Wajumbe watano wanaochaguliwa mionganoni mwa Wabunge wa Chama Tawala na katni ya Wajumbe hao Wajumbe wawili wanapaswa kuwa wanawake. Wajumbe kundi la pili wanaochaguliwa mionganoni mwa Wabunge wa Vyama vyta Upinzani vyenye uwakilishi Bungeni amba mjambe mmoja kati yao anapaswa kuwa mwanamke. Sasa uchaguzi huu unaendeshwa kufuatana na masharti ya Kanuni ya 5(2) ya Nyongeza ya Pili ya Kanuni za Bunge Toleo la 2007 ambazo zinafafanua taratibu za uchaguzi wa Bunge wanaowakilisha Bunge katika Tume ya Utumishi wa Bunge. Kwa mujibu wa Kifungu cha 8(2)(b) cha Nyongeza ya Pili ya Kanuni ya Bunge kila mgombea atatakiwa afike mbele ya Waheshimiwa Wabunge yaani wapiga kura kujieleza kwa dakika zisizo dakika tatu na kujibu maswali yao kama yatakuwepo. Baada ya kujieleza karatasi za kupiga kura zitatolewa ili Waheshimiwa Wabunge muweze kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Kwa hiyo tutakachokifanya sasa tutawaita wagombea mmoja mmoja, nadhani wenywewe wako nje.

**WABUNGE FULANI:** Wameingia.

**SPIKA:** Wameingia. Basi wagombea wote mliotajwa, naomba mtoke nje, tutakuwa tunamwita mmoja mmoja kuja kujieleza kwa dakika tatu. Tutakwenda kwa makundi kwa maana ya Chama Tawala na vyama nya Upinzani. Tunaanza. Katibu hebu eleza vizuri.

**NDG. JOHN JOEL- KATIBU:** Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nadhani ni vizuri Katibu akatufahamisha kwamba sasa tunaanza kundi gani. Vinginevyo hao wagombea ni wengi sana, wako makundi tofauti tofauti. Angetufahamisha kwamba sasa tunaanza kundi la wanawake Bara. Tunakuja kundi linalofuata, vyovyote vile ambavyo makundi yamepangwa. Maana vinginevyo tutachanganyikiwa. Tunapigaje kura. (*Makofi*)

**SPIKA:** Katibu hebu eleza.

**NDG. JOHN JOEL - KATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ile Sheria haikusema kama tuwatofautishe kwa maana ya jinsia. Isipokuwa Sheria yenewe inasema kwamba zitapigwa, watachaguliwa Wabunge watano kati ya hao watano angalau wawili wawe wanawake. Kwa hiyo, tunapoanza tutaanza na lile kundi la Chama Tawala ambao nitaita wote wajieleze halafu baadaye nitaita kundi la Upinzani wajieleze na karatasi zitagawiwa kwa ajili ya kupiga kura.

### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika,

**SPIKA:** Ndiyo!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, tunaongozwa na Sheria, Katiba, Kanuni na Taratibu na Maamuzi ya siku za nyuma. Siku zote tunavyopiga kura kwa ajili ya Wajumbe wa Kamisheni ya Bunge tunakwenda kwa makundi. Ni kweli kwamba ni watano. Kwa hivi ili kuhakikisha kuna *representation* inayotakiwa huwa tunapiga kura. Siku zote tunafanya hivyo. Kwa mfano, kundi la wanawake kuna kundi la wanawake Bara, kuna kundi la Wanawake Zanzibar. Ndiyo tumekuwa tukifanya hivyo siku zote *unless otherwise* utaratibu ni mpya na Spika ni mpya anakuja na utaratibu mpya tutaufuata huo utaratibu mpya. Lakini taratibu za siku za nyuma zimekuwa hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hapo tumechanganya, kuna vitu nya namna hii. Hapa Sheria inasema katika Tume ile kuna Wajumbe saba. Katika Wajumbe saba watano wanatoka Chama Tawala na wale watano wa Chama Tawala angalau wawili wawe wanawake. Ndiyo maana Katibu amesema tuanze na kuwahoji wale wa Chama Tawala wote, tutakapoleta kura hapa mtakuta majina yote ya wale wa Chama Tawala na ya wanawake yapo. Kwa hiyo, wewe utakapopiga ukipenda angalau upigie wawili wanawake, wawili wanaume mmoja utachagua. Maana yake wamesema angalau wawili

wawe wanawake, siyo wawili wawe wanawake, angalau wawili wawe wanawake, tungeweza tukasema angalau wawili wawe wanaume. Kwa hiyo, hivyo ndivyo tutakavyofanya. Tutakapokuja kwenye kundi la pili, Wapinzani wote sasa katika wao tunataka wawili tu angalau mmoja kati yao awe mwanamke. Mnaona hapo. Kwa hiyo nayo itakuja kwa mtindo huo.

Haya tunaanza hiyo kazi sasa, tuko wote jamani? Maana tusiende bila kuelewana. Tumeelewana? Ndivyo inavyosema, siyo kwamba ukileta wanawake sasa unafanyaje? Unachagua nini? Kwa sababu angalau suala la Wapinzani pale, kuna kundi la Wapinzani ambao angalau mmoja atatoka Zanzibar, hiyo ndiyo inasema kabisa. Mmoja lazima atoke Zanzibar. Siyo mpinzani, yaani mmoja lazima atoke Zanzibar.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo *point* ninayoizungumza kwamba siku zote katika makundi haya tunasema ni lazima mmoja atoke Zanzibar. Kwa utaratibu wa kura ambao Katibu anatuelezea na maelezo ambayo umeyatoa hakuna hiyo *condition* ya mmoja kutoka Zanzibar. Matokeo yake tunaweza tukawa tuna athari tunakuwa na Kamisheni ambayo haina *representation* ya Zanzibar. Hii ndiyo *problem* ninayoionna na miaka yote tunapiga kura tukiweka *condition* hiyo na ndiyo maana Mheshimiwa Kidawa alikuwa Kamishna, Kamisheni iliyopita, kwa sababu tuliweka hiyo *condition*.

Sasa kama ni utaratibu mpya tunauweka kwamba hatuweki *condition at least* mmoja kutoka Zanzibar, utuambie sasa kwamba huu ndiyo utaratibu mpya ili tuweze kuufuata. Hatutaupinga, tutaufuata kwa sababu unakwenda kwenye maamuzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto tusilet *complication*. Kuna chaguzi nyingi katika utaratibu wetu. Tunapochukua *East Africa* ndiyo inakuwa na matatizo hayo. Lakini siyo hili, hili watano wanatoka Chama Tawala, lakini katika wao wawili lazima wawe wanawake.

Ya pili ni kundi la Wapinzani wawili. Katika wao, angalau mmoja awe mwanamke. Ndiyo maana sasa katika ile orodha ya wapiga kura tutaona majina hayo tutachagua, ukitaka kupigia watatu wanawake, wawili wanaume katika Chama Tawala sawa. Ukitaka kupigia wawili wanawake, watatu wanaume sawa. Kwa hiyo, umechanganya hapa, hii ni ya *East Africa*. Naomba tuendelee vizuri. Sasa kwa hiyo tunaanza na chama.....

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** *Madam Speaker*, ukiangalia wanawake wanaogombea wako zaidi ya watatu wanatoka Bara, Zanzibar wanatoka wawili. Ukitaka kwamba tunachagua wanawake wasiopungua wawili, iko hatari tunaweza tukachagua wote wawili wa Bara ama wote wawili wa Zanzibar. Bado ile *representation* yetu kwa Bunge kwamba tuangalie Muungano wetu tutakuwa hatujaifikia. Ndiyo maana *culture* yetu ya zamani ilikuwa kuna nafasi moja ya mwanamke lazima atoke Unguja, ama Zanzibar, nafasi nyingine atoke Tanzania Bara. (*Makofî*)

**SPIKA:** Mnachanganya, acha tupige kwanza kura mtaona. Hiyo mnayozungumza inahu *East Africa Parliament*. Hii ni ya Tume, tunavyosema ndivyo ilivyo. Lakini bahati nzuri wenyewe...

### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu wa kitu gani? Sasa naomba tutulie. Sasa tuwaite, tumemwita kwanza Mheshimiwa Diana Chilolo, aje ajieleze na wengine watajieleza halafu kura ile itaonekana hivyo.

### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. EZEKIEL D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu

**SPIKA:** Kama ni kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Anne Kilango kwanza. Maana wewe ulikuwa wa pili.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa. Naomba tutumie tu ubinadam kwamba wanawake hawa wawili, mmoja atoke Zanzibar, mmoja atoke Bara. (*Makofi*)

**SPIKA:** Sasa huyo anawaombeni ninyi wapiga kura, Sheria haisemi hivyo. Mheshimiwa nani alikuwepo pale.

**MHE. EZEKIEL D. WENJE:** Naitwa Mheshimiwa Wenje. Kuna kitu sijaelewa vizuri, kwa sababu kama alivyosoma Katibu anasema kwamba angalau wanawake wachaguliwe wawili kwa maana yake ni kwamba *at least* wawili lakini haina *limit*. Kwa hiyo, ina maana naruhusiwa kupigia wanawake watano?

**SPIKA:** Sawa. Itakuwa sawa. Tunaendelea jamani mna-*complicate* mambo bila sababu. Sasa namwita Mheshimiwa Chilolo.

Mheshimiwa Chilolo una dakika tatu za kujieleza na baadaye utapewa maswali matatu kama yapo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Viongozi Wakuu wote mliopo katika Ukumbi huu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu mabibi na mabwana. Niliyesimama mbele yenu naitwa Diana Mkumbo Chilolo. Nimegombea Ukarishma wa Tume ya Utumishi wa Bunge kuitia kundi la wanawake Chama Tawala.

Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa taaluma mimi ni mwalimu. Nataka niwathibitishie nimekaa Bungeni sasa ni awamu ya tatu. Nina uwezo wa kutosha kuimudu nafasi niliyoiomba. Nafahamu kazi ya Tume, nitakuwa mstari wa mbele

kuwasikiliza Wabunge wenzangu, kero zinazowasibu. Hivyo, nitatetea maslahi yenu kuhakikisha mnafanya kazi zenu vizuri pamoja na kero ya madereva inayozungumzwa kila wakati. Vile vile nitakuwa mstari wa mbele kutetea maslahi ya watumishi wa Bunge pamoja na ajira zao na kazi zote kwa kushirikiana na ushauri wa Katibu wa Bunge. Vile vile nitakuwa mstari wa mbele kushirikiana na Makamishna wenzangu watakaoshinda kuhakikisha Bunge linaendesha shughuli zake vizuri pamoja na kumshauri Rais hasa katika suala zima kwa rasilimali fedha.

Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa heshima na unyenyevu mkubwa nina uelewa wa kutosha, nina uwezo mkubwa wa kuhoji masuala mbalimbali bila hofu. Hivyo, nina imani kabisa nitawatumikia vizuri. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa nawaombeni kura zenu zote mnipe kwa roho moja mkiwa na imani kabisa nitawatumikia vyema. Ahsanteni sana. Naitwa Diana Mkumbo Chilolo.

**SPIKA:** Ahsante. Maswali.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Kwa mara ya pili, maswali.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Kwa mara ya tatu maswali.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa Diana Chilolo, chukua kiti chako.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Nashukuru sana.

**SPIKA:** Kaa kwenye kiti chako umeshamaliza kazi.

Mheshimiwa Dokta Maua Abeid Daftari, unapewa dakika tatu kujieleza na kama kuna maswali utaulizwa matatu.

**MHE. DR. MAUA ABED DAFTARI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Waziri unayeshughulika na mambo ya Bunge. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge *Assalam aleykum*.

**WABUNGE FULANI:** Waaleykum salaam.

**MHE. DR. MAUA ABED DAFTARI:** Bwana asifiwe.

**WABUNGE FULANI:** Milele, Amina.

**MHE. DR. MAUA ABED DAFTARI:** Niliyesimama mbele yenu ni Mheshimiwa Dokta Maua Abeid Daftari. Maelezo yangu tayari nimewasilisha kwenu kwa kipeperushi. Nina hakina mmepata nafasi ya kuyapitia na kujua ni kitu gani. Leo nimesimama hapa mbele yenu kuja kuomba kura, ili niwawakilishe kuwa Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge. Ni mwenzenu nimeshafanya kazi za utumishi kwa muda mrefu. Nilikuwa daktari Mkuu Pemba, nilikuwa Daktari wa Wilaya, nilikuwa Mkurugenzi wa Huduma za hospitali, nilikuwa Mkurugenzi wa Huduma za Hospitali pia nilikuwa Mbunge na Naibu Waziri kwa vipindi mbalimbali. Kwa hiyo katika kufanya kazi kwangu kazi nimepata uzoefu mkubwa katika masuala ya Utawala.

Lakini itoshe kwamba nilipata mafunzo ya utawala *IDM*, Botswana, *SEDA* Arusha, *ESAMI* Arusha, kwa hivyo ninajihisi ninayo nafasi na uwezo wa kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge na kuwatetea vilivyo katika changamoto zilizopo katika Bunge letu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Msipige makofi.

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kura yako, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa heshima na taadhima naomba kura yako, Mheshimiwa Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni na Kambi yako naomba kura zako zote, Waheshimiwa Wabunge wote ndugu zangu naomba kura zenu zote kwa Dokta Maua Abeid Daftari, ni mwenzenu aliyewatumikia kwa muda mrefu. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kanuni moja, hakuna makofi. Sasa maswali, swali mara ya kwanza?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Swali mara ya pili?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Swali mara ya tatu?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dokta Maua Abeid Daftari, naomba ukachukue nafasi yako.

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye. Tunakupa dakika tatu za kujieleza, halafu baada ya hapo utaulizwa maswali matatu kama yapo.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge Wenzangu, niliyesimama mbele yenu ninaitwa Cynthia Hilda

Ngoye. Nimesimama mbele yenu ili kuomba nafasi mnichague niwe mmoja wa Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, nimekuwepo katika Bunge lako kwa muda wa vipindi, sasa ni cha tatu. Nimeshuhudia changamoto nyingi sana na nyingi zimetatuliwa na Tume iliyopita. Naomba nafasi hii ili niweze kuanzia pale walipoishia wenzetu, kuendelea kushughulikia matatizo au changamoto mbalimbali za Bunge pamoja na utumishi mzima wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, nina uzoefu mkubwa sana katika masuala ya utumishi, ya uongozi na vile vile katika mambo ya uendeshaji kutokana na kazi mbalimbali nilizozifanya ndani ya Serikali kama Mwalimu, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa, Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Mazingira. Natazamia kabisa kutumia ujuzi wangu katika kuendeleza masuala yote na changamoto mbalimbali ambazo zipo mbele yetu. Nawaombeni sana mnisadie ili niweze kuchaguliwa, nina uwezo mkubwa wa kutafuta changamoto zote zilizopo na kuzifanya kazi. Naweza hata kufika mbele ya Rais, nikamwomba ili aweze kutusaidia Wabunge pamoja na watumishi wote ili Bunge letu liweze kuijendesha vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima nakuomba kura yako. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuomba kura yako. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kutoka Chama Tawala, pamoja na Vyama vya Upinzani, naombeni kura zenu zote na naomba mniamini. Ahsanteni sana.

**SPIKA:** Maswali, swali mara ya kwanza?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Swali mara ya pili?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Swali mara ya tatu?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hilda Ngoye kachukue nafasi yako ukae.

Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, nakupa dakika tatu za kujieleza na kama kuna maswali basi utaulizwa maswali matatu.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Spika, kama ulivyonitambulisha, jina langu naitwa Saleh Ahmed Pamba, ni Mbunge wa Jimbo la Pangani. Maelezo yangu binafsi yalitolewa asubuhi katika vipeperushi, ambayo yanaonesha uzoefu wangu katika utendaji hasa utendaji wa Serikali. Nimefanya kazi katika Serikali kwa muda mrefu, nimefikia cheo cha juu kabisa katika Serikali, Cheo cha Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kwamba nkipata nafasi hii nitachanganya uzoefu wangu nilioupata katika Serikali, kuhakikisha kwamba tunajenga Bunge la kisasa ili liweze kukabiliana na changamoto mpya ambazo zinajitokeza wakati kwa wakati. Vile vile tutataka tuifanye Tasisi hii iwe ni chombo ambacho kinawavutia wafanyakazi mbalimbali wa ngazi mbalimbali, wa uwezo mbalimbali ili waone fahari ya kuja kufanya kazi katika taasisi hii ambayo ni mhimili mkubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kura yako. Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali, naomba kura yako. Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, naomba kura yako. Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla, naomba kura zenu ili tuweze kushirikiana katika kujengwa taasisi yetu, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Maswali, mara ya kwanza?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Maswali mara ya pili?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, lipo.

**SPIKA:** Aah! Yupo, samahani Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Pamba, pamoa na maelezo yako mazuri na uzoefu mkubwa katika utendaji kazi na inaonekana una nia nzuri ya kulitumikia Bunge. Lakini ni kitu gani kimoja sisi kama Wabunge, katika miaka mitano unataka kukifanya ili utakapoondoka tukukumbuke?

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Spika, kitu kikubwa ambacho nitakifanya katika kipindi cha miaka mitano, kwanza, ni kuhakikisha kwamba tunajenga uwezo wa Wabunge ili waweze kupambana na changamoto zinazojitokeza katika taasisi hii ili kusudi waweze kukabiliana na mambo yote. Pili, ni kuhakikisha kwamba Wabunge wanapata maslahi mazuri wanapata nafasi nzuri ya kuhakikisha kwamba wanafanya kazi yao bila matatizo yoyote katika kutumikia umma. (*Makofii*)

**SPIKA:** Swali kwa mara ya tatu?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pamba ahsante, ukakae kwenye nafasi yako.

Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh. nakupa dakika tatu za kujieleza na kama kutakuwa na maswali basi yatakuwa matatu.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mwenzenu niliyesimama hapa naitwa Kidawa Hamid Saleh. Nimesimama kwa madhumuni makubwa ya kuomba kura zenu mniwezeshe niwe Mjumbe wa Tume yetu ya Utumishi wa Bunge, kama Kamishna. Ndugu zangu nina uzoefu wa kutosha katika shughuli za uongozi.

Mheshimiwa Spika, nimefanya kazi Serikalini katika kipindi cha miaka 20 kabla sijajiunga na Bunge. Hivi sasa ni Mbunge kwa kipindi hiki cha tatu. Aidha, nimefanya kazi katika sekta mbalimbali yakiwemo mashirika ambayo sio ya Kiserikali. Nimepanda ngazi Serikalini kutoka Afisa wa kawaida hadi Meneja, nimekuwa Mkurugenzi wa Mfuko wa Akinamama wa kutoa mikopo, nimekuwa Mjumbe wa *Steering Committee* wa miradi mbalimbali iliyokuwa ikipata ufadhili wa *UNDP* na *UNIFEM* na mengineyo. Mwenzenu nimeshawahi kuwa Mjumbe wa Tume ya mipango Zanzibar kwa vipindi viwili. Aidha, nimeshawahi kuwa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya *NMB* kabla ya kubinafsishwa na vile vile nimeshakuwa Mjumbe wa Baraza la Chuo Kikuu Huria.

Mheshimiwa Spika, pia katika Bunge lililopita wenzenu walinchagua kuwa Kamishna wa Tume hii baada ya ile sheria kubadilishwa. Lakini kwa bahati mbaya sana nimetumikia nafasi hii kwa kipindi kifupi tu kuanzia katikati ya 2009 hadi Bunge lilipovunjwa tukaenda kwenye mchakato wa uchaguzi. Ndugu zangu, wenzenu wamenionesha imani na ninyi naomba imani yenu, nirudisheni ninatetea nafasi yangu. Sikufanya dhambi, nimefanya kazi nzuri. Mwenzenu ni mtulivu, ni msikivu, nitawasikilizeni, nitajenga hoja, nitawateteeni vizuri. Kichama, mimi ni Katibu wa Idara ya Oganaizesheni ya Chama, Makao Makuu. Kwa hiyo, nina uzoefu mpana wa kichama, wa Serikali na wa kwenye taasisi zisizokuwa za Serikali. Ndugu zangu, naomba kura zenu, tafadhalini naomba sana. Naomba sana ndugu zangu mnirudishe. Ahsanteni.

**SPIKA:** Maswali kwa mara ya kwanza?

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, lipo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Regia.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimuulize Mheshimiwa Mgombea, swali lifuatalo, Mheshimiwa Mgombea, naomba utuambie majukumu matatu tu ya Kamishna.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, majukumu matatu ya Ukamishna. Moja ni kushughulikia maslahi ya Wabunge, maslahi ya Watumishi, mambo ya *procurement* ya vifaa ndani ya Bunge na mambo mengine yote ya kuendesha Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi ni hayo tu ninayoweza kueleza.

**SPIKA:** Swali kwa mara ya pili?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Swali kwa mara ya tatu?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kidawa Saleh, kachukue nafasi yako.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kura zenu Waheshimiwa, *please!*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah. Yupo mbali sana?

*(Wakati Mheshimiwa Shah alipokuwa akiingia ukumbini Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakipiga makofi)*

**SPIKA:** Tumesema kwamba hatupigi makofi, inakuwaje? Tumesema hatupigi makofi.

Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah, tunakupa dakika tatu za kujieleza halafu kama maswali yapo, watakuuliza maswali matatu.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani, Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri, Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naitwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah, Mbunge wa Mafia, Mkoa wa Pwani. Nimesimama hapa mbele yenu kwa heshima zote zilizojaa unyenyekevu kuomba kura zenu zote mnipe mimi ili niendelee kuwa Mjumbe katika Kamisheni ya Tume ya Huduma za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, sina mengi ya kujieleza. Niliyoyafanya wakati wa kipindi kilichopita kwa kuwa, nilikuwa Mjumbe wa Tume ya Huduma kwa kipindi cha miaka mitano katika Bunge la Tisa, mazuri, mema na yote haya mliyoyaona mmoja wa wachangiaji na kuimarisha miundombinu ya Bunge lakini pia maslahi ya Waheshimiwa Wabunge na Watumishi kwa ujumla. Nisichukue muda mrefu, kwa heshima zote ninaomba kura zenu.

Mheshimiwa Spika, naomba kura yako. Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kura yako. Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kura yako. Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani, naomba kura yako na wenzako wote wa Kambi yako. Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri na Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, chama ninachotokea, naomba kura zenu zote; mniamini niendelee kupigania maslahi ambayo ni vipi yalikuwa na sasa tupo vipi na ni nini ambalo tunatarajia ni kuhakikisha kwamba Bunge letu linatakiwa liwe Bunge la kisasa na mategemeo yetu tuliyoyapanga kulifanya Bunge letu liwe la *Electronic Parliament*, Bunge la *TEKNOHAMA*.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima zote naomba kura zenu. Mnichague mimi ili niwe mjambe wa Tume. Ahsanteni.

**SPIKA:** Swali kwa mara ya kwanza? Lipo swali. Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kumwuliza Mgombea huyu swali.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Tume hii ya Huduma za Bunge, kipindi kilichopita na ulinipa ushirikiano mzuri. Unaahidi kumpa ushirikiano huo huo huyu Mwenyekiti mpya? (*Makofi/Vicheko*)

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani, Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Waziri na Wabunge wote. Nashukuru sana kwa swali zuri aliloniuliza Mheshimiwa Spika wa zamani ambaye nilifanya naye kazi kwa karibu na ndio maana akauliza swali hilo kwa sababu kwanza ni mnyenyekemu, mpenda watu, nahudumia Wabunge pale linapotokea tazito hata linapotokea majumbani. Naahidi kutoa ushirikiano mkubwa kwa Mheshimiwa Spika. Kama unavyofahamu yale mema yote ambayo wewe ndio ulikuwa mwalimu wetu, naahidi kutoa ushirikiano. Ahsante. (*Makofi/Vicheko*)

**SPIKA:** Swali kwa mara ya tatu?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah, nenda kachukue nafasi yako. (*Makofi*)

**MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naombeni kura zenu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Hayo makofi, niliwaambia hapana, kwani nyie hamsikii? Anayefuata, Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, aingie. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nasema makofi hakuna, inakuwaje tena?

Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, nakupa dakika tatu za kujieleza na kama maswali yatakuwepo, basi yatakuwa ni matatu.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani, Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Niliyesimama mbele yenu naitwa Beatrice Matumbo Shellukindo, ni Mbunge wa Jimbo la Kilindi, Mkoani Tanga. Nimesimama mbele yenu kuomba ridhaa yenu, niweze

kuwatumikia kama Kamishna katika Tume ya Utumishi wa Bunge. Sababu ni nyingi sana, lakini kwa sababu ya muda naomba niseme chache.

Nimekuwa katika Bunge la Afrika Mashariki na nilikuwa kwenye Kamati ambayo ilikuwa inashughulikia maslahi ya Wabunge na masuala mengine ya taratibu za Wabunge. Lakini vile vile nimekuwa mtumishi katika ofisi za Serikali kama Afisa Utumishi kwa zaidi ya miaka 16 katika Wizara mbalimbali. Nimeshiriki katika kupanga maslahi, sheria za watumishi na mambo mengine, elimu yangu inatosha. Waheshimiwa nawahakikisha kwa sababu ukiwa Kamishna pia lazima uwe na lugha ya kuongea na wafadhilli kwa kuongea mambo mbalimbali kupanga mikakati mbalimbali ya Wabunge lugha hiyo ninayo, ushawishi huo ninao.

Lakini mwisho kabisa, nilishiriki katika Kamati ndogo ya Mheshimiwa Ndugai ya kutunga Kanuni ambapo tulikuwa watu watano, mwanamke nikiwa pekee na tulizunguka nchi zote, Kanuni mnazotumia sasa ndizo hizo tulizozifanyia kazi, najiringia kwamba tuliweza kushawishi tukapata mfuko wa Jimbo, tukaanza wimbo wa Taifa na mengine mengi mazuri ambayo mnayaona katika kanuni hizo. (*Makofi*)

Mengi ambayo ningeweza kuyasema, lakini nimegawa maelezo yangu machache maana yake ni mengi mno lakini nataka niwahakikishie, kila Mbunge najua ana uwezo, kikubwa ni sisi mkitupa ridhaa yenu kama makamishna kuhakikisha kwamba kila mmoja anapata fursa, nawahakikishia Wabunge, uwoga sina natetea jambo na neno kushindwa haliko kwenye kamusi yangu. Baada ya kusema hayo naomba sana mniipe kura zenu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa hamsikii, hakuna makofi, sasa tumwulize maswali, kuna mtu ana swali jamani?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Kwa nini mnasema hakuna? Mheshimiwa Ester Bulaya naona una swali.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, labda ningependa kumuuliza swali dogo tu Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, tunajua ana uzoefu wa kutosha na alikuwepo katika Bunge la Tisa na anajiamini vilivyo, swali langu ni dogo tu. Je, tutarajie mambo gani mapya na hasa kwa sisi Wabunge wapya tulioingia, tutafaidika na nini na uwezo wako?

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa swali zuri sana, hayo maswali ndiyo mnatakiwa muwape makamishna. Kwanza kabisa posho za Wabunge ni ndogo sana kulingana na kazi ambazo tunafanya. (*Makofi*)

Lakini la pili naomba niwahakikishieni wananchi wanatarajia mengi sana kutoka kwetu, sasa sisi hapa lazima tujipange vizuri ili hata hii Mifuko ya Majimbo iweze kufanya kazi kule Majimboni. Kwa Wabunge wapya naomba niwahakikishieni kwamba,

niko tayari kama ambavyo nimekuwa nikifanya muda wote kuhakikisha kwamba ninyi mnakuwa wazoefu kwa muda mfupi, nataka nihakikishe kwamba mtapata semina za kuwaelekezeni kwa kushirikiana na Makamishna mtakaotuchagua na Ofisi ya Spika nataka niwahakikishieni yale yote ambayo mnaona yanawatatiza yatafanikiwa.

Lakini mwisho kabisa, naomba niseme kubwa ambalo nitalifanya ndani ya Bunge hili kuanzia dakika hii ni kuleta mshikamano na muungano na matatizo yote ambayo yanajitokeza yasiwepo asanteni sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali kwa mara ya pili?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Swali kwa mara ya tatu?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shellukindo naona maswali yamekwisha, chukua nafasi yako.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Kwa heshima na taadhima naomba kura zenu. Ahsanteni. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante anayefuata ni Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, tunakupa dakika tatu za kujieleza na kama maswali yatakuwepo basi tutakuuliza maswali matatu.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza nakushukuruni sana kwa kunipa fursa ya kuniskiliza lakini nichukue fursa hii kuwashukuru wote ambao wamenisaidia kufanya kampeni na naamini kulikuwepo na utayari wa kunipa kura. Lakini kwa kuzingatia msingi wa mahusiano na kuwa katika kundi langu wanaotakiwa ni watatu na tuko wane. Kwa hiari yangu na kwa kushauriana na marafiki zangu nimeamua niwaunge mkono wenzangu hawa watatu na kwa hiyo, naomba muwapigie kura na mimi mniangalie siku za usoni. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kuna maswali? Mheshimiwa Lema karibu.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, langu sio swali ila nataka nimpongeze kwa sababu ana maono ya mbali kwa sababu angepata kura chache sana. Kwa hiyo, nakupongeza sana Mheshimiwa. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Maswali kwa mara pili?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Maswali kwa mara ya tatu?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simbachawene chukua nafasi yako. (*Makofi*)

Hivi nyie huwa mnasikia Kiswahili! Hakuna makofi.

Anayefuata ni Mheshimiwa Godfrey Zambi. Mheshimiwa Zambi nakupa dakika tatu za kujieleza na kama kutakuwepo na maswali basi yasizidi matatu.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Waheshimiwa Wabunge wenzangu *Assalam Aleykum*.

**WABUNGE FULANI:** *Waaleykum salaam.*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Tumsifu Yesu Kristo.

**WABUNGE FULANI:** Milele Amina.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mwana Kondoo ameshinda.

**WABUNGE FULANI:** Na tumfuate.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, naitwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Jimbo la Mbozi Mashariki kule Mbeya. Naomba nafasi ya Kamishna Tume ya Utumishi wa Bunge, dakika ambazo tumepewa kujieleza si nyingi sana. Naomba niseme kwamba, nimechapisha vipeperushi, nina imani wengi mtakuwa mmeviona lakini niseme kwamba nimekulia ndani ya kazi za utawala, shule yangu yote niliyosoma, nimesoma masuala ya utawala na utumishi, ndizo kazi nilizofanya katika kipindi chote mpaka ninapokuwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu naelewa changamoto ambazo ziko mbele yetu na hasa zinazohusiana na Tume ya Utumishi ya Bunge, nilishaanza kule Dar es Salaam tulipokuwa kwenye semina, kutetea maslahi ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watumishi wa Wabunge. (*Makofi*)

Nazielewa changamoto nyingi, nina hakika, mkinifanya mionganii mwa wale ambao watakuwa kwenye Tume hii tutafanya kazi kubwa tukishirikiana na viongozi wengine akiwepo na Mheshimiwa Spika, ambaye anakuwa Mwenyekiti wa Tume. Naomba mnipe imani nina uwezo wa kujenga hoja, nina uwezo wa kutetea hoja, na nina

uwezo wa kujieleza, naombeni sana imani yenu na sitowaangusha. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Maswali kwa mara ya pili?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Maswali kwa mara ya tatu?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa Godfrey Zambi tunakushukuru, nenda ukachukue nafasi yako.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba kura, Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kura yako, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Wabunge wenzangu wote nawaombeni imani kwa kunipa kura zote za ndiyo. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge orodha ya kwanza ya Chama tawala tumemaliza, kwa sababu *ballot paper* imechanganya makundi yote, nalazimika kuingia tena kuwahoji Kambi ya Upinzani.

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taratibu zetu pale ambapo nafasi zinazogombewa zinapokuwa zina wagombea wale wale wanaotakiwa huwa wale watu wanakuwa wamepita bila kupingwa. Sasa hapa tuna wagombea watatu tu kwa wanaume na *ime-meet criteria* ya sheria ya kwamba angalau wawili wanawake, watatu wanaume, naomba mwongozo wako kwamba itakapofikia kupiga kura tupige kura za nafasi mbili za wanawake tu na hizi tatu ziwe zimepita bila kupingwa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto, kwanini unajikanyaga, umesema angalau wawili wanawake, tena unasema wako watatu, sasa vipi, lakini kama tulivyosema bahati mbaya hizi *paper* tumezipanga vibaya kama tungekuwa tumezipanga vizuri kundi la kwanza tungepiga kura halafu tuendelee kuhoji wengine, lakini kwa sababu ni *ballot paper*, basi naomba mniruhusu tuwaite na wale Kambi ya Upinzani pia tuweze kuwahoji halafu baadaye tutapiga kura pamoja, haya tunaendelea.

Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, tunakupa dakika tatu za kuweza kujieleza na kama yataulizwa maswali hayatazidi matatu.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** nashukuru sana. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, kwa jina naitwa Agripina Zaituni Buyogera, ni Mtanzania wa kawaida, mwenye elimu ya msingi lakini pia ambaye nimepata mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na muda mrefu, yaliyoniwezesha kushika nafasi mbalimbali katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, uzoefu nilionao katika kuwatumikia Watanzania au jamii ya Kitanzania, mwaka 1998 mpaka 2003 nilichaguliwa na Mkutano Mkuu wa Wafanyabiashara wa Wilaya ya Kasulu kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara *TCCIA* Wilaya ya Kasulu. Mwaka 2003 nilichaguliwa na Mkutano Mkuu wa *NCCR* Mageuzi, kupata nafasi ya kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama ambayo naitumikia mpaka hivi leo. (*Makofi*)

Mwaka 2005 nilikuwa ni mwanamke pekee niliyethubutu kugombea Ubunge kwenye Jimbo la Kasulu Mashariki, Mkoa Mzima wa Kigoma na nikapata kura zaidi ya 35,000, nilikuwa mshindi wa pili kitu kilichopelekea katika historia ya mfumo wa Vyama vingi Wilaya ya Kasulu Jimbo la Mashariki tulikuwa hatujawahi kupata Diwani hata mmoja. Nilipogombea mwaka 2005 nilisababisha kushinda Madiwani Kata nne na mimi nikapata Udiwani Viti Maalum. (*Makofi*)

Mwaka 2005 mpaka 2010 nilikuwa Diwani wa Wilaya ya Kasulu, 2010 ni Mbunge wa Jimbo la Kasulu Mashariki. Waheshimiwa Wabunge nawaomba sana nina uzoefu wa kutosha wa kutumika. Naomba mnipe kura niwe Kamishna wa Tume ya Utumishi kama mama mnaona wenyewe jinsi Spika anavyoongoza kikao chetu vizuri, naamini nitakuwa mshauri mzuri na mjumbe muadilifu katika Tume ya Utumishi wa Umma. Ahsante kwa kunisikiliza naomba kura zenu zote. (*Makofi*)

**SPIKA:** Haya maswali kwa mara ya kwanza.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Hakuna.

**SPIKA:** Maswali kwa mara ya pili?

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Hakuna.

**SPIKA:** Maswali kwa mara ya tatu?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agripina chukua nafasi yako. Anayefuata ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, aingie. Acheni kupiga makofi, yaani nyie hamjui Kiswahili, eeh!

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed tunakupa dakika tatu za kujieleza na kama yatakuwepo maswali hayatazidi matatu.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Ahsante sana. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima na taadhima, nasimama mbele yenu mimi Hamad Rashid Mohamed nikiwaomba kura zenu zote ili niwe mtumishi wenu katika Utumishi wa Tume ya Ofisi ya Bunge.

Uzoefu wangu na ujuzi wangu nina hakika nyote mnajua toka 1977 niliingia ndani ya Bunge hili niliwahi vile vile kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar, nimekuwa Mwenyekiti wa *PAC* katika Bunge hili, nimekuwa Naibu Mwenyekiti wa *SADCOPAC*, nimekuwa vile vile Katibu Mkuu wa *East African Public Accounts Committee*. Pia katika Bunge hili lililopita nilikuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani lakini pia kwa nafasi yangu kama Kiongozi wa Upinzani nimekuwa katika Tume hii. Uzoefu wangu katika Uongozi nauelewa na mafunzo mbalimbali niliyopata katika uongozi, nahakika wengi mnayaelewa.

Mheshimiwa Spika, bila kupoteza muda nakuomba wewe, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, namwomba Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani, naomba Waheshimiwa Wabunge wote kwa heshima zote mnipe kura zenu zote. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Maswali kwa mara ya kwanza, Mheshimiwa Khalifa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru Mheshimiwa Mgombea, vita ya kudai haki haisimami mpaka haki imepatikana. Katika Bunge lililopita la kumi Wabunge tuliokuwapo tulilalamika sana kuwa haki ya mishahara yetu miwili haijalipwa. Ninavyoolewa wewe na wenzako chini ya Mheshimiwa Spika aliyemaliza muda mmepegana kufa na kupona ili haki hii ipatikane, je, tukikurudisha utaendelea nayo vita hiyo? (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, kama mnavyofahamu majukumu makubwa ya Tume hii ni pamoja na kusimamia haki za Wabunge pamoja na Watumishi wa Bunge hili, huo ni wajibu wa kisheria kwa mujibu wa Sheria yetu Na. 14 ya 2008, huo ni wajibu wa kisheria, nawahakikishia kwamba, nitaendelea na kazi hiyo mpaka haki yetu ipatikane. (*Makofi*)

**MHE. MUSSA ALI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Hamad Rashid, ye ye alikuwa ni kiongozi wa Upinzani katika Bunge, Bunge lililopita amejitahidi sana kuunganisha umoja katika Kambi hiyo pamoja na Chama Tawala, sasa kidogo matatizo yametokea katika Bunge na kwa uwezo wako na nafasi unayoiomba utasaidia nini kurejesha umoja huo katika Bunge letu hasa kama wewe ni kiongozi mwenye uzoefu?

**SPIKA:** Kama Mjumbe wa Tume hawezi kufanya hicho kitu. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Nilitaka kuuliza kama lile la kwanza.

**SPIKA:** Aah! Kwa hiyo swalii la tatu.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, naomba chukua nafasi yako.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kura yako, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani, Waheshimiwa Wabunge wote kwa taadhima nawaomba kura zenu. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhonga Said Ibrahim Ruhwanya aingie!

Mheshimiwa Mhonga Said Ibrahim Ruhwanya, tunakupa dakika tatu za kujieleza na kama maswali yatakuwepo hayatazidi matatu.

**MHE. MHONGA S.I. RUHWANYA:** Ahsante. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, kwa jina naitwa Mhonga Said Ruhwanya.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa mmoja wa Wabunge wa Bunge hili la Kumi lakini pia kwa kuzingatia majukumu muhimu yaliyo katika Tume ya Utumishi wa Bunge, nimeona nijitose ili niweze kushiriki katika kutetea maslahi ya Wabunge. Vile vile kama tunavyofahamu Tume hii ya Utumishi wa Bunge ni muhimu sana kwa kumshauri Rais namna bora ya kuendesha Bunge letu la Jamhuri ya Muungano, ndiyo pekee inayoangalia vigezo vya mgawanyo wa fungu maalum au Mfuko Maalum wa Bunge na vile vile inahusika na utoaji ajira na pia inahusika na usimamizi wa nidhamu kwa watumishi ambao ni kiungo muhimu katika ufanisi wa kazi zetu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninao uwezo wa kugombea nafasi hii kwa sababu Mungu amenijaalia nimepata elimu ya kutosha na vilevile nikiwa kama kijana nimeangalia katika wengi waliogombea nimegundua pia kuwa kuna umuhimu wa kijana pia kuingiza katika Tume ya Utumishi wa Bunge kwa kuzingatia kwamba sasa hivi Chama cha Mapinduzi, NCCR Mageuzi kumekuwa na vijana wengi. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kijana pia kuingia katika Tume ya Utumishi wa Bunge kwa sababu zipo changamoto nydingi ambazo vijana wanazipata katika maeneo yao ya uwakilishi ambao ni viti maalum na ambao pia wako katika Majimbo.

Kwa hiyo, kutakuwa na mawazo, matatizo na mahitaji ambayo watataka yaingie katika Tume, kwa hiyo, nitakuwa kama daraja kwao. Lakini vile vile nimegombea pamoa na kwamba ni kijana, nimegombea kama mwanamke kuititia Kambi ya Upinzani, naamini kabisa akinamama wote mlioko katika Bunge la Jamhuri ya Muungano mtaniunga mkono bila kujali itikadi za vyama vyetu kwa sababu nchi yetu ni ya

kidemokrasia, lazima iwe mawazo mbadala kwa maana kwamba lazima iwe na Kambi ya Upinzani Bungeni.

Kwa heshima na taadhima nakuomba wewe Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani pamoja na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani aliyepita pamoja na Wabunge wote, naomba kura zenu zote za ndiyo ili niweze kushiriki katika Tume hiyo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Maswali kwa mara ya kwanza?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna!

**SPIKA:** Maswali kwa mara ya pili? Kuna swalii wapi? Mheshimiwa Bulaya karibu!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimuulize swalii Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya.

Ni vitu gani vitatu vyatya msingi unavyoona vinafaa kwenda kuvi-*present* kwenye Tume kwa maslahi ya Wabunge vijana ?

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Ahsante sana mwuliza swalii. Ukiangalia kifungu namba 13 cha Sheria hii namba 14 ya 2008 ya Uendeshaji wa Bunge letu kuna mambo kadhaa ambayo yameainishwa.

Kwanza, ni maslahi ya Wabunge na maslahi pia ya watumishi, ukiangalia kama alivyoniambia kwamba ni vitu gani ambavyo naweza kwenda kuvitetea kwa vijana, najua kuna mahitaji mengi sana ya vijana na wana changamoto nyingi ambazo wanakutana nazo ndiyo maana nimesema kwamba nitakuwa daraja kwenu ili ninyi kwa kushirikiana pamoja kuna mawazo mengine ambayo mtakuwa mkinipa niyapeleke katika Tume yetu ya Bunge ili yaweze kutatuliwa.

Lakini vile vile jambo lingine tukiangalia siyo vijana Wabunge peke yake, ukiangalia watumishi wa Bunge wengi pia ni vijana wana mahitaji yao ya msingi ambayo itakuwa ni rahisi kama kijana mwenzao kwenda kuya-*present* katika Tume yetu ya Bunge.

**SPIKA:** Ahsante sana. Maswali kwa mara ya tatu?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna!

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, ahsante sana kachukue nafasi yako.

Anayefuata ni Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Nakupa dakika tatu za kujieleza na kama kutakuwa na maswali hayatazidi matatu.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Ahsante. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Niliye mbele yenu kwa jina naitwa Magdalena H. Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Tabora kuititia Chama cha Wananchi, CUF.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nafasi ya Kambi ya Upinzani kwa upande wa wanawake inayotakiwa ni moja na kwa kuwa tuliojaza nafasi ni watatu kutoka kwenye Kambi moja, ili kudumisha umoja na mshikamano kwa Wabunge wote na ili kuendeleza umoja uliopo ambao tungependa uendelee kuwepo ndani ya Kambi ya Upinzani, kwa ridhaa yangu naomba Wabunge wote kwanza nishukuru kwa kunikubali kama mgombea lakini naomba nijitoe ili busara na hekima zitumike kwa Wabunge kupata mgombea kutoka kwa watu wawili ambao nimewaachia nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, ila nitaomba Wabunge wanifikirie kipindi kingine ambapo nitaomba nafasi yoyote bila kukatishwa tamaa na kujitoa kwangu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, maswali tafadhal!

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Swali kwa mara ya pili?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Na swali kwa mara ya tatu?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, naomba ukachukue nafasi yako.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Anayefuata ni Mheshimiwa John Paul Magalle Shibuda aingie.

Mheshimiwa John Paul Magalle Shibuda tunakupa dakika tatu za kujieleza na iwapo kutakuwa na maswali hayatazidi matatu.

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, shukurani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, jambo la kwanza kabisa napenda kutoa shukurani za dhati kwa kukubalika kwamba na mimi niwe mmojawapo katika dhamana hii.

Ijumaa wakati nachangia nilikuwa Babu kwa kutoa nasaha na kuwaasa kizazi kipywa, leo vivyo hivyo napenda kusema kwamba kila aliye na subira yuko na Mwenyezi Mungu na kuahirisha safari siyo kufuta safari. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wabunge wenzangu wote naomba kwa moyo mkunjufu mkubali niahirishe safari hii ya kuomba dhamana hii kwa sababu kama niliweza kuwanasihi vijana ya kwamba aliyekutangulia umheshimu, aliyenitangulia katika kundi letu la Upinzani, ni kaka yangu Hamad Rashid Mohamed, kala chumvi nyingi, alikuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, Mjumbe wa NEC na ni mkongwe wa mambo ya Vyama vya Upinzani. Hazina hiyo naona ni bora iende katika Tume hii, *Inshaallah*, Mwenyezi Mungu akinijaalia jambo lingine la kuja kuomba basi naomba mniweke katika nafsi zenu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Maswali kwa mara ya kwanza?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Maswali kwa mara ya pili?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Maswali kwa mara ya tatu?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Magalle Shibuda ahsante sana, naomba uchukue nafasi yako.

Waheshimiwa Wabunge, wale wote tuliopaswa kuwahoji tumewahoji, karatasi yetu ya kura itakuwa na sehemu mbili, iko moja lakini ina sehemu mbili kama tulivyosema, sehemu ya kwanza ya Chama Tawala. Sasa tuelewane hapa, sheria inasema idadi ya wanawake wasiopungua angalau wawili, angalau! Neno angalau siyo kwamba maana yake wawili na inabidi baadaye tuanze kubadilisha tuandike angalau wanaume maana yake hapa mnachanganya wenzenu.

Halafu sehemu ya pili ndiyo wenzetu kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani nayo pia tunachagua wawili angalau mmoja mwanaume na mwingine mwanamke hapa afadhali. Kwa hiyo, kuna swali kabla hatujaanza kupiga kura?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, katika nafasi ya Upinzani kwa mujibu wa sheria ni mmoja mwanamke na mmoja mwanaume. Kwa upande wa Kambi ya Upinzani kuna mwanaume mgombea mmoja kwa maana hiyo ni kwamba Mheshimiwa

Hamad Rashid Mohamed amepita bila kupingwa, tunapigia kura jina moja kupata mwanamke mmoja mionganoni mwa wanawake wawili.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo yako.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kufuatana na zile kanuni zetu hata mtu kama akipita bila kupingwa inabidi tumpigie kura ya ndiyo au hapana. Lakini kama sisi tunakubaliana kwamba yule aliye peke yake tusimpigie kura basi hapo ni uamuzi wa kwetu. Sasa mnasemaje?

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Wanje.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, siyo Wanje ni Wenje, usipokaa vizuri sasa utaita Wanja.

Mheshimiwa Spika, kama nakumbuka vizuri kipindi tulivyoanza mlipokuwa mnasoma Sheria inayosimamia hii *process* tunayoifanya ulisema kwamba *at least* yaani angalau wawepo wanawake wawili maana yake ni kwamba kwenye upande wa Upinzani hata tukiamua kuchagua wanawake wawili hakuna tatizo kwa sababu *that is the truth* hakuna *limit*, kuna *flow* lakini hakuna *ceiling* kwenye hiyo Sheria. Kuna *flow* kwa maana ya *at least two* lakini hakuna *ceiling* kwamba *at least whatever*. Kwa hiyo, ina maana tunaruhusiwa kupigia hata kura hawa akinamama wawili.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo.

**SPIKA:** Haya *returning officer* hebu jibu maswali hayo, semea huko huko.

**ND. JOHN JOEL - KATIBU:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ufanuzi kama ifuatavyo na baadaye nitaisoma Sheria yenyewe kama inavyosema.

*Group la kwanza tumesema angalau wawili na ndivyo inavyosema yaani at least two, five shall be elected from the Parliamentary part or parties from the Government at least two of whom shall be women.*

Kundi la pili ni la Upinzani nayo inasema, mmoja awe mwanamke *shall be* yaani *whom shall be a woman*, nasoma; *two shall be elected from the Parliamentary part or parties forming the opposition in the National Assembly one of whom shall be a woman*. Kwa hiyo, mmoja ni mwanamke kati ya wale wawili.

## HOJA

**KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja sasa kwamba Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed apite bila kupingwa. (*Makofi*)

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

## TAARIFA

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono kwanza, haya endelea na ni taarifa, ya nini ?

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, nadhani hawa wamefika kwenye *voting flow* kwa maana ya kwamba majina yao yamefika, walichofanya wao ni kuomba wasipigiwe kura, lakini haina maana kwamba sasa lazima tuwapigie wale wengine wapite bila kupingwa kwa sababu ukiomba upigiwe kura unaweza ukapigiwa au usipigiwe. Kwa hiyo, kwa sababu wamefikishwa hapa tupige kura kama kawaida isipokuwa tutazingatia maombi yao ya kutopigiwa kura.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba msichanganye sasa wale waliojiondoa, Sheria iko kimya haisemi kwamba kama ulishakuwepo hapa ni lazima upigiwe kura. Ninachowaomba katika kundi la wale wa Chama Tawala Mheshimiwa George Simbachawene ameondoa jina lake. Katika kundi la pili la Kambi Rasmi ya Upinzani Mheshimiwa Madgalena H. Sakaya ameondoa jina lake, Mheshimiwa Magalle John Shibuda ameondoa jina lake, naomba *m-note* hiyo. Hoja aliyoitao Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto ni kwamba kwa sababu anatakiwa mwanaume mmoja katika Kambi Rasmi ya Upinzani basi huyo apite bila kupingwa. Sasa kwa sababu kuna wanawake wawili, hawa wapigiwe kura na hoja imeungwa mkono.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kutopigiwa kura wagombea Wabunge  
wasio na Mpinzani ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA :** Haya tunaendelea, msimamizi wa uchaguzi!

**ND. JOHN JOEL :** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni zetu inabidi sasa kengele ipigwe halafu niweze kuhesabu Wabunge waliomo humu ndani na baadaye tutagawa *ballot paper* kwa ajili ya kupiga kura.

**SPIKA :** Kwa hiyo, kengele ipigwe !

*(Hapa Karatasi za Kura Ziligawanywa)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Nyie mnapenda mwongozo! Haya Mheshimiwa Sendeka!

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi japo sipendi sana.

Mheshimiwa Spika, nimeona limekwenda vizuri hili tulilomaliza sasa hivi kwa upande wa Hamad Rashid Mohamed na sasa tuna kazi ya kuchagua mwanamke mmoja kati ya Waheshimiwa wale wawili. Nafikiri busara hiyo hiyo ungeitumia kwa upande wa wale watano kwamba wamebaki wanaume watatu halafu *then* hao wapite bila kupingwa halafu Wanawake wale wengine tuwapigie kura ili kupata wawili. Nadhani wakati mwingine itasaidia pia kuangalia na sisi wanaume tuwepo kule badala ya kusema tu angalau Wanawake, utaratibu huu nao siyo mzuri sana.

**SPIKA:** Aisee! Hiyo haikubaliki kwa sababu wanaweza wakawepo Wanawake watatu na wanaume wawili na mimi ningefikiri ingekuwa hivyo sasa. Kwa hiyo, hiyo bado watapigiwa kura. Sasa naomba Maafisa mnaohusika mhesabu idadi yetu ndani ya ukumbi huu. Naomba hiyo ifanyike haraka, tuwahesabu Wabunge wote katika ukumbi lakini wale wagombea ukipata kura moja ambayo ni ya kwako utasema hata Spika hakunipigia? Mimi sipigi kura, kwa hiyo, usije ukasema hata Spika hakunipigia? Mimi sipigi kura hapa kama mmefungana basi nitapiga.

Waheshimiwa Wabunge, tuliopo humu ndani sasa hivi naomba msitoke wakati tunapiga kura tuko 294, sasa tunagawa karatasi za kura na naomba mpige kwa uangalifu ili zoezi hili liende haraka.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Jamani tunapopiga kura, naomba Mwongozo usiwepo.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, kuna jambo la muhimu, kura zitaharibika.

**SPIKA:** Eeh, sema basi.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, tunapigia kura wagombea wangapi? Ingekuwa vyema ikatamkwa, ingekuwa rahisi sana kwa watu wakati wa kupiga kura.

**SPIKA:** Kwenye karatasi imeandikwa kila kundi. Kundi la kwanza kura tano, kati ya kura hizo, pigia angalau wanawake wawili. Kundi la pili, kwa sababu kuna wanawake wawili tu, sasa inabidi upigie mmoja kwa sababu mwingine amepita bila kupingwa.

**SPIKA:** Kila mtu anachukua karatasi moja tu. Kila mtu amepata karatasi? Nyie *Page Boys and Girls*, chukueni hayo maboksi. Haya mya-*empty* kwanza yaonekane kwamba yako wazi, mbona yako matatu tu, mengine yako wapi?

*(Hapa masanduku ya kura yalioneshwa  
kwa Waheshimiwa Wabunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, nadhani mmepeiga, wakusanye?

**WABUNGE FULANI:** Bado.

**SPIKA:** Bado, haya! Tutakusanya kura kwenye maboksi, tafadhal! Kura zikusanywe kwenye maboksi. Naomba mpite mstari kwa mstari, watatumbukiza wenyewe huko, kura zikusanywe kwenye maboksi. Msubiri kura kwenye maboksi. Tufanye zoezi la kukusanya kura haraka ili tumalize. Maboksi matatu yako upande mmoja. Jamani mnaogawa karatasi, si tumemaliza, mbona naona mnaendelea kugawa karatasi?

*(Hapa kura zilianza kukusanywa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, mkinyamaza mtapiga kura, mnaongea nini? Kuna uchaguzi mwingine unaofuata, msiende moja kwa moja, nyie ndugu mnaotoka, kuna uchaguzi mwingine. Haya wote mmeshakusanya kura? Mbona nyie mmebakia kwenye kona moja tu? Nani hajarudisha kura yake? Kule nyuma, kuna wengine huku, ambaye hajarudisha kura anyooshe juu kura yake, yuko huku na kule nyuma. Kuna mwingine ambaye bado ana karatasi ya kura?

Sasa tunawaomba wahusika kila mtu kama anataka kuweka Wakala au anataka kwenda mwenyewe aende. Mheshimiwa Diana Chilolo, unamweka nani?

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mary Chatanda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mary Chatanda, sogea mbele. Mheshimiwa Maua Abeid Daftari?

**MHE. MAUA A. DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, nitakwenda mwenyewe.

**SPIKA:** Eeh, ye ye atakwenda mwenyewe. Mheshimiwa Cynthia Ngoye.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Kangi Lugola, Mbunge wa Mwibara.

**SPIKA:** Haya ahsante. Mheshimiwa Saleh Pamba.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Saidi Mtanda, Mbunge wa Mchinga.

**SPIKA:** Hao wanaotajwa wasogee hapa.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nimekubali uteuzi. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Umekubali. Wanaotajwa wasogee hapa. Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Ali Juma.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa hayupo.

**WABUNGE FULANI:** Anaumwa.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Yahya Kassim.

**SPIKA:** Yahya Kassim, umetaja wawili?

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Yule wa kwanza hayupo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdulkarim Shah.

**MHE. ABDULKARIM E.H.SHAH:** Mheshimiwa Iddi Azzan

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Azzan uende. Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, unamtaja nani?

**MBUNGE FULANI:** Simama, tamka Pindi Chana.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, namtaja Mheshimiwa Pindi Chana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pindi Chana. Mheshimiwa Godfrey Zambi unamtaja nani?

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, namtaja Mahmoud Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini.

**SPIKA:** Sawasawa Mahmoud Mgimwa, halafu Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, unamtaja nani?

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa David Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, unamtaja nani?.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Lucy Owenya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Owenya. Kwa hiyo, hao ndio Mawakala, aliye kwenda mwenyewe ni mmoja tu, Mheshimiwa Maua Daftari. (*Makofii*)

Kwa hiyo, pamoja na maboksi mnaenda kwenye *Speaker's Lounge*, mkafanye kazi hiyo ya kuhesabu kura. Haya *Returning Officer* tuendelee. Waheshimiwa Wabunge, tuna nafasi moja nyingine tufanyie uchaguzi sasa hivi. Hebu eleza Katibu.

**NDG. JOHN JOEL – RETURNING OFFICER:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowatangazia tena tarehe 9 Februari, 2011 na Jumapili ya tarehe 13 Februari, 2011, leo Jumatatu tarehe 14 Februari, 2011 kama inavyooneshwa kwenye *Order Paper*, tutakuwa na uchaguzi wa Mbunge atakayeliwakilisha Bunge kwenye Baraza la Uongozi la *African Peer Review Mechanism (APRM)*. Muda wa mwisho wa kurudisha fomu za kuomba uteuzi ilikuwa ni Jumapili tarehe 13 Februari, 2011, saa 10.00 jioni. Muda huo ulipofika, Wabunge waliokuwa wamejitokeza kuchukua na kurejesha fomu ni wawili ambao ni Mheshimiwa Magalle John Shibuda, pamoja na Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla. Hata hivyo, nimepokea barua kutoka kwa Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, kuwa anajitoa kugombea katika nafasi hii.

Uchaguzi huu unaendeshwa kufuatana na Masharti ya Nyongeza ya Pili ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 ambazo zinafafanua taratibu za uchaguzi wa Wabunge wanaowakilisha Bunge katika vyombo vingine vya uwakilishi.

Kwa mujibu wa Kanuni ile ya 5(2)( c ) ya Nyongeza hii; endapo atajitokeza mgombea mmoja wa nafasi inayohusika, Wabunge watampigia kura ya ‘Ndiyo au Hapana’. Hata hivyo, Bunge hili limejiwekea utaratibu ‘*Convention*’ kuwa inapotokea Mgombea mmoja kwa nafasi moja basi mgombea huyo anapita bila kupingwa.

Hivyo, katika hili Waheshimiwa Wabunge tunaomba muamue utaratibu upi ufuatwe. Mheshimiwa John Magalle Shibuda, apigiwe kura ya ‘Ndiyo au Hapana’ au apite bila kupingwa baada ya Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, kujiondoa.

**SPIKA:** Kwa hiyo, Mheshimiwa John Magalle Shibuda, naye amepita bila kupingwa. Ajieleze kidogo, sauti yake nzuri, ndiye Mwakilishi wetu katika Shirika la *APRM*. (*Makofii*)

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walimpitisha  
Mheshimiwa John Magalle Shibuda bila kupingwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasubiri kuhesabu kura, naomba tuendelee na majadiliano ya Hotuba ya Mheshimiwa Rais na wakimaliza kuhesabu, tutatangaza matokeo. Katibu endelea na *Order Paper!*

## HOJA ZA SERIKALI

**Hoja ya Kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Kufungua Bunge Jipyä, 2010**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha leo kusimama katika Bunge lako Tukufu, huo ni uweza wake na si ujanja wangu.

Pia napenda kumshukuru Mke wangu, Bi. Ashura pamoja na familia yangu yote akiwemo mama yangu, pamoja na wananchi wote wa Jimbo la Nyang'hwale, kwa kunichagua na kuwa Mwakilishi wao. Pia napenda kuwapongeza Wabunge wote, Mawaziri pamoja na Naibu Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kidogo Hotuba ya Mheshimiwa Rais kuhusiana na mambo machache. Kwanza, nitaanza kuchangia kidogo kuhusu suala la elimu. Kwa kweli suala la elimu Waheshimiwa wengi wamelichangia, lina matatizo mengi na mimi napenda nichangie kidogo katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, Jimboni kwangu upungufu wa Walimu ni mkubwa sana. Nimejaribu kufanya ziara katika shule, nimekuta shule ina Wanafunzi 700 na Walimu wawili. Upungufu mwingine ni vitendeakazi, madawati na nyumba za Walimu. Ni matatizo sana, lakini cha kushangaza shule hizo ambazo ziko Jimboni kwangu unakuta Shule ya Sekondari ina Walimu wawili, lakini unakuta Shule ya Sekondari ya aina hiyohiyo iko mjini ina walimu 18 mpaka 30. Naiomba Serikali ijaribu kuliangalia hili suala la uwiano wa Walimu, kwa nini Vijijini Walimu wanakuwa wachache sana na shule za Mijini zinakuwa na Walimu wengi? Kwa nini? Naiomba Serikali ijaribu kuliangalia suala hilo na kuwaangalia hao Walimu ambao wako Vijijini angalau basi mishahara iongezwe labda inaweza ikawa changamoto kwa Walimu ambao wanang'ang'ania Mijini waweze kwenda Vijijini.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchangia kidogo kwenye suala la kilimo. Katika Jimbo langu 95% ni wakulima. Wakulima hao namshukuru Mungu kwamba wanajitahidi sana katika kilimo lakini kuna mambo mengi ambayo yanakwamisha maendeleo yao ikiwemo ukosefu wa soko la mazao yao. Soko la mazao si zuri na halina msimamo. Mavuno mengi yanapatikana lakini cha kushangaza unakuta gunia la mpunga linauzwa kati ya Sh.15,000 na Sh.20,000, mkulima huyu atajikomboa vipi wakati gharama za uendeshaji wa kilimo ni kubwa? Naiomba Serikali ijaribu kuliangalia suala hili la soko, tutafutiwe wafadhili, yajengwe maghala ili wanunuzi waweze kuja kununua mazao yetu kwa bei iliyo nzuri.

Mheshimiwa Spika, pia mazao mengi yanapatikana hususani ndani ya Vijiji ambavyo vina matatizo mfano barabara ni mbovu, hivyo kuyaleta mazao yale katika sehemu ambayo angalau bei nzuri inakuwa haiwezekani. Naiomba Serikali hususani Wizara ya Kilimo na Chakula, ijaribu kuwaangalia wakulima kwa kuwawezesha kwa pembejeo na kuliweka imara soko la mazao ili tuweze kumnyanyua mkulima.

Mheshimiwa Spika, pia naiomba Serikali iweze kuja kuwapimia mashamba yao ili waweze kupata hatimili ki waweze kupata mikopo Benki hatimaye waweze kupanua kilimo. Naiomba Serikali iangalie sana suala hilo la kuwawezesha wakulima kwa kipitia *asset* waliyonayo ikiwemo ardhi, mkulima hawezi akakopeshwa bila kuwa na hatimili. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijaribu kuliangalia suala hilo ili tuweze kuwanyanya wakulima kwa kuwamilikisha ardhi yao waweze kupata hatimili na hatimaye waweze kupata fedha katika Benki.

Mheshimiwa Spika, napenda kidogo kuchangia kwenye suala la maji. Jimboni kwangu kwa kweli kuna tatizo kubwa sana la maji. Kuna sehemu akina mama wanaondoka saa tisa za usiku kufuata maji umbali wa kilomita tano, ni shida. Cha kushangaza sisi katika Jimbo letu, Ziwa Victoria ni kilomita moja unayapata maji lakini Jimbo langu halina maji, kwa nini? Miaka ya nyuma, mwaka 1972 palifungwa pampu ya kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria na kusambazwa baadhi ya Kata. Lakini cha kushangaza mwaka 1975 pampu hiyo ikawa imesimamishwa kusukuma maji na hivi ninavyoongea mashine hiyo leo miaka 36 karibu ipo, pampu yake ipo na baadhi ya matenki yapo, lakini maji hatupati. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijaribu kutuangalia kwa jicho la huruma, yaletwe maji hayo ili waweze kupunguza adha ya kufuata maji umbali mrefu. Kwa kweli tatizo la maji ni kubwa hata mifugo yenewe wananyweshwa yale maji kwa kufuata kilomita tano kwenye balskeli. Mtu anachukua balskeli kufuata maji umbali wa kilomita tano kuja kuwanywesha ng'ombe na ng'ombe hao hawana afya nzuri, afya yao ni mbovu kwa sababu hawapati maji.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuzungumzia kidogo upande wa afya. Katika Jimbo langu, Zahanati zipo, Vituo vya Afya viko viwili, Kituo kimoja kimeelemewa. Kituo kimoja kipo Kharumwa ambapo sasa hivi ndio Makao Makuu ya Wilaya. Kituo kingine cha pili kiko Nyang'wale, ni kituo kizuri, kina majengo mengi lakini kimetelekezwa, hivi ninavyoongea popo ndio nyumba yao ya kuishi. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijaribu kukihuisha hicho Kituo ili kiweze kutoa huduma kwa sababu Kituo kimoja cha Kharumwa kimezidiwa. Tuko wananchi zaidi ya 350,000, kituo ni kimoja. Zahanati pia zipo lakini na zenyewe zina upungufu, Wauguzi, madawa pamoja na vitendea kazi. Lakini pamoja na hivyo Zahanati hizo hazitoi huduma inavyopaswa kwa sababu huduma zenyewe zinatolewa kwa upendeleo. Nikizungumza kwa upendeleo kila mmoja anaelewa upendeleo huo ni upi. Kwa kweli naiomba Serikali ijaribu kulifuatilia suala hili, kwa nini upungufu wa madawa upo na ukienda kwenye maduka ya madawa binafsi unakuta dawa zile za *MSD* zimo kwenye maduka yao, wao wanazipata wapi? Lakini ukienda Zahanati na kwenye Vituo vya Afya unakuta dawa hizo hazipo. Ukweli ni kwamba naiomba Serikali ijaribu sana kufuatilia hususan Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie kidogo upande wa miundombinu. Miundombinu ya Jimbo la Nyang'wale, tunashukuru kwamba kuna barabara moja tu ambayo ndio inapitika kipindi chote lakini baadhi ya barabara za ndani ni mbovu na pia kuna mito ambayo haipitiki hususan wakati wa masika na Mito hiyo inasababisha mpaka wanafunzi wanashindwa kusoma kwa sababu ya kujaa. Mto huo ukijaa, unakata

mawasiliano kati ya Kijiji hiki na Kijiji kingine na kusababisha wanafunzi wasiende kusoma hata huduma zingine zisifanyike. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijaribu kuliangalia sana suala hili ili tuweze kujengewa angalau daraja ili mawasiliano yawepo kipindi chote. Kuna Mito kama mitano ni matatizo makubwa, naiomba Serikali kilio hiki ijaribu kukisikia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwenye upande wa usalama wa raia hususan upande wa Polisi. Jimboni kwangu Polisi kwa kweli wanaishi kwa taabu, nyumba zao ni mbovu kuliko, Vituo vya Polisi karibu vinaanguka, nyumba hamna, Mahabusu zile ni mbovu kabisa. Kwa hiyo, naomba angalau basi Serikali iweze kujenga nyumba nzuri za ofisi za Polisi pamoja na kuwajengea nyumba za kuishi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wananchi wanalamika sana kwa huduma ambayo inatolewa na Polisi wa Jimboni kwangu. Kuna unyanyasaji wa hali ya juu na pia rushwa imekithiri. Nazungumza hivyo kwa sababu kuna matukio mbalimbali ambayo yamejitokeza yanawahu Polisi. Mfano mwezi uliopita, kuna watoto takribani watano wameliwa na fisi, lakini taarifa zikitolewa kwa Polisi hebu njooni muangalie tatizo hili, wakifika pale wanawanyanyaapaa waliofiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais. (*Makofî*)

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Nami nianze kwa kuwashukuru wananchi wa Ngara, kwa kuniamini na kunipa ridhaa ya kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu. Hotuba hii ni muhimu sana. Rais alipokuja Ngara wakati wa kampeni wananchi walimshukuru sana kwa kazi nzuri aliyoifanya katika miaka mitano iliyopita na wakamuahidi kumpigia kura nyingi na kwa taarifa ya Bunge hili Ngara ilikuwa ya kwanza katika Mkoa wa Kagera katika kumpigia Rais kura nyingi na tukawa watano Kitaifa. *Mimi I am very proud of that.*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumzia vipaumbele karibu vyote 13. Mimi naviunga mkono, vyote ni muhimu sana, nadhani tutakavyoendelea, tutawenza kuzungumzia vipaumbele hivyo.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mwalimu *by profession*. Naomba nizungumzie elimu, lakini sitazungumzia yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wameshayazungumzia. Nitazungumzia jambo lingine muhimu sana tofauti na yale ambayo yameshazungumzwa na Waheshimiwa Wabunge. Najua Waheshimiwa Wabunge katika kuzungumzia elimu wamesema kuna matatizo ya uhaba wa Walimu, maslahi madogo ya Walimu, vitabu vichache, madarasa yanahitaji kuongezwa, lakini mimi kama Mwalimu nimefanya utafiti mdogo kule Ngara kwa kuzungumza na Walimu mbalimbali, nikaona kwamba kuna tatizo la ufundishaji, *teaching* yenye inaweza ikaleta matatizo na kuathiri matokeo ya mitihani ambayo mnayaona.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda Chuo Kikuu, nilisomea Ualimu Butimba *Teacher's College* lakini pia nilipokwenda Chuo Kikuu, nilisoma Elimu pamoja na

*Management and Administration.* Sisi wakati huo tumeingia Chuo Kikuu mwaka 1968 – 1971, tulijizatiti katika *psychology of education, philosophy of education* na *methodology*. Mtaalamu mmoja ambaye nataka kumzungumzia sasa hivi kwa kazi yake alioifanya alikuwa anaitwa Prof. Benjamin Bloom. Benjamin Bloom alikuwa *a great psychologist* huko Marekani. Prof. Bloom anasema kwamba wewe Mwalimu unapokwenda darasani ujue kwamba kuna *six levels of learning* ambazo Mwalimu unatakiwa kuzizingatia. Nizitaje halafu nitafafanua kwa sababu zinazidiana. Hatua ya kwanza ni *knowledge, you will impart knowledge to the students or to the pupils*. Pili, ni *comprehension*, lazima kama Mwalimu uhakikishe kwamba watoto wameelewa. Hii nitazungumzia kwa kirefu zaidi. Ya tatu ni *application*, kuona kama watoto wanawenza ku-*apply* hizo *concepts, principles* na hizo theories ambazo wamefundishwa. Ya nne, ni *analysis*, lazima uhakikishe kwamba watoto unawafundisha namna ya kuchambua mambo, *you develop their analytical abilities*. Kwa mfano, unapofundisha Katiba ya Tanzania, ukishafundisha unamwuliza mtoto Katiba hiyo imegawanyika katika sehemu gani? Watakueleza sehemu ya Serikali ambayo ni *Executive branch*, sehemu ya Mahakama ambayo ni *Judiciary*, sehemu ya Bunge ambayo ni *Legislative Branch*. Unaanza kuwfundisha namna ya kuanza ku-*analyze*. *To analysis* kwa Kiingereza maana yake ni *to break something into parts*. Ukitoka kwenye *analysis* unakwenda kwenye *synthesis*, Mwalimu lazima darasani uhakikishe kwamba mtoto anaweza akayaweka pamoja yale yote uliyoyafundisha. *To synthesize* ni *to put things together*, ni tofauti na *analyse* ya ku-*break something into parts*. Ya mwisho ni *evaluation*. Wewe kama Mwalimu lazima uhakikishe kwamba yale malengo uliyokuwa nayo wakati wa kufundisha umeyafikia.

Mheshimiwa Spika, vijana wa siku hizi sijui kama wanakwenda kwa utaratibu huo. Mimi nilikuwa Mwalimu na nilikuwa nahakikisha kwamba nafuata hizo *six levels*. Baada ya kusema hayo ya *knowledge*, huwezi ku-*impart knowledge* kama wewe huna *knowledge*. Kwa hiyo, Mwalimu lazima aandaliwe vizuri, apewe *knowledge* ya kutosha. Kama wewe ni mtaalamu wa *Chemistry* unaweza ku-*impart knowledge* ya *Chemistry*?

Mheshimiwa Spika, pia Mwalimu lazima ajue kwamba darasani kuna watoto wa aina tatu. Wa kwanza ni *normal students*, wa pili ni *bright students* na wa tatu ni *slow learners*. Naomba kama kuna Waziri wa Elimu anisikilize vizuri. Kuna tatizo la *slow learners* ambalo linaweza kusababisha matatizo makubwa katika mitihani. Hizi *syllabus* tunazozungumzia na *curriculum*, zinatengenezwa kwa ajili ya *normal students* na sisi Walimu tunasema a *normal students* ni yule ambayo ana *IQ* ya 100, *Intelligence Quotient* ya 100. *Bright student's* wanakwenda *beyond 100*, *slow learners* wako kwenye 75 au 80. Kwa hiyo, Mwalimu lazima ajue matatizo hayo na aweze ku-*address* tatizo la *slow learners*. Nashauri Wizara ya Elimu, kwa kuwa tatizo la *slow learners* ni kubwa sana, watafute wataalam ambao wanawenza kuendesha semina za (TOT) *Training of Trainers*, ili hawa watakaokuwa *trained* waweze kusaidia hawa *slow learners*. Hilo ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna *three other factors* ambazo zina-affect *learning*. Moja ni *personal factors*, mtoto umjue vizuri matatizo yake, huko nyumbani anakotoka na kadhalika. *Environmental factors* na mwisho ambalo nataka kulizungumzia ni *language barrier*. Kiingereza ni tatizo katika nchi yetu. Katibu

Mtendaji wa Baraza la Mitihani amezungumzia kwamba anafikiri tatizo la *language* limekuwa ni *problem* katika kushindwa watoto wengi katika mtihani uliopita.

Mheshimiwa Spika, sisi tulipokuwa tunasoma, tulikuwa tunaambiwa kwa Kiingereza “*You must frame examination questions in the examinee language not in the examiners language*”. Tafsiri yake ni kwamba “unapotunga mitihani uitunge kwa lugha ya mtahiniwa sio kwa lugha yako kama Mwalimu”. Kwa hiyo, kwa mtahiniwa unatakiwa utumie lugha rahisi. Nimeona nizungumzie tatizo hilo kwa sababu nafikiri Wabunge wengine wamezungumzia matatizo ya Walimu lakini hilo nalo ni tatizo, *teaching six levels of learning* ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, katika elimu pia nizungumzie Elimu ya Watu Wazima, siwezi kuishia kwenye kuzungumzia elimu ya msingi, sekondari na vyuo vikuu, tunahitaji pia kuhakikisha kwamba tunarudisha kisomo cha watu wazima. Mimi nimeshiriki sana katika kisomo cha watu wazima kwenye miaka ya 1970. Wananchi, wazee, kinamama na kinababa wakitoka mashambani walikuwa wanakwenda kujifunza kusoma na kuandika. Tukafikia kwenye *level* ya *literacy* ya 95% na tukawa wa kwanza duniani kwenye miaka 1970 na 1980. Wakati huo *level of literacy* Marekani ilikuwa 85% tulikuwa tunawazidi. Mwaka 1986/87 nilikwenda kusoma Marekani nikawa nawaambia *you can be a super power* lakini sisi tunawazidi kwenye *literacy*, sisi 95% ninyi ni 85%. Sasa juzi nimetembelea Idara ya Elimu kwa Njia ya Posta nikawaauliza hivi tumetoka 95% tumefika wapi? Wakasema Mheshimiwa Ntukamazina kwa kweli *official figure* imefikia 68% lakini tu nadhani tuko chini zaidi. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Elimu irudishe kisomo cha watu wazima. Jambo hili limejidhihirisha mwaka jana wakati wa uchaguzi. Wakati wa Uchaguzi, watu wengi wazee wameandikiwa majina. Walikuwa wanaaulizwa, mnamtaka nani, wakijibu kama wanamtaka Ntukamazina Mawakala wanaandika Rugumyamheto au Banyikwa. Kwa hiyo, unaweza ukapoteza kura nydingi sana kwa sababu *illiteracy* imeanza kuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie kwenye elimu ambalo Rais amelizungumzia ni masomo ya sayansi. Tatizo tulilonalo, vijana wanaomaliza Kidato cha Sita kama wamesoma sayansi wengi wanakwenda Uduktari au Uhndisi, wachache wanakwenda kuchukua *Bachelor of Science with Education* kama zamani. Kwa hiyo, nadhani vijana wahamasishwe wachukue *Bachelor of Science With Education* ili waweze kwenda kufundisha sayansi kwenye shule mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwenye upande wa elimu ambalo nataka nniombi Wizara ya Elimu ilifikirie au Serikali, naomba tumuenzi Marehemu Baba wa Taifa ambaye alikuwa na ndoto nydingi sana, aliona mbali sana, akasema tuanzishe *a Science Village*. Akatoa fedha na akamteua Marehemu Prof. Shayo aanzishe kijiji hicho lakini bahati mbaya kijiji hicho hakikuanzishwa. Lengo la Marehemu Baba wa Taifa lilikuwa ni kwamba tuanzishe kijiji hicho, tuchukue vijana wenye akili sana, tuwafundishe sayansi kwenye kijiji hicho na kuwepo na *library* ...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji*)

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA:** Kengele ya pili? Nimalizie kwa kusema tuanzishe *institution* mbili, *National Service* pamoja na *Leadership College* itasaidia vijana wetu...

**SPIKA:** Aah, hapana! Mheshimiwa hatufanyi hivyo, hapa ikigongwa kengele ndio umeishia hapo hata kama hujamaliza.

## TAARIFA

**MHE. MUHAMMAD I. SANYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa ya dharura.

**SPIKA:** Sio taarifa ya dharura, wewe changia tu halafu useme hayo unayotaka kusema.

**MHE. MUHAMMAD I. SANYA:** Mheshimiwa Spika, ninachotaka kukielezea katika Bunge lako Tukufu ni kwamba, hivi karibuni Benki Kuu ya Tanzania ilichapisha na kutoa noti mpya mbalimbali kwa dhamira njema na nzuri kabisa ambayo Serikali inailewa. Jambo la kusikitisha ni kwamba hata siku 100 baada ya kuchapishwa noti hizo na kutumika katika nchi yetu hazijapita, hata ile *circulation* yake hajamalizika, tukapata hizo noti mpya, kuna wajanja wachache ama wa ndani ama wa nje tayari wameshachapisha noti hizo mpya na zimesambaa katika nchi ya Tanzania na nyingine zikiwa hapa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, natoa tahadhari na taarifa hii ili vyombo husika vya usalama wa nchi vikishirikiana na Benki Kuu, viweze kuwasaka watu hawa kwa sababu hali ya uchumi itaendelea kudidimia, hali ya *inflation* ambayo ipo itazidi kuwa kubwa. Badala ya watu kupewa uwezo na nguvu kwa kufanya mambo muhimu, kwa kufungua viwanda vidogo vidogo vya kuzalisha kwa ajili ya kuinua uchumi wa nchi, wao wameanzisha viwanda vya kuchapisha noti ambazo zimesambaa nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima zote, napenda noti hii ambayo nimeipata ya shilingi 10,000/= ambayo ni *fake* niikabidhi kwako ili ifanyiwe kazi kwa sababu noti hii ukiiangalia kwenye sehemu ya upande wa kushoto ambako kunatakiwa kuwe na *watermark* ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, hii haina, noti mpya iliyo toka karibuni ninayo. Ni jambo la kusikitisha, kufadhaisha na linawenza likaangusha uchumi na kuwatahirisha wajanja wachache ama wa ndani au wa nje bila ya kuwa na athari.

Mheshimiwa Spika, naikabidhi noti hii kwako ili Benki Kuu na vyombo vya usalama vifanye kazi ili tuwaokoe wananchi ambao wanakuwa katika hali mbaya wanapofanya biashara ndogondogo na kupata noti ambazo ni za bandia zinazoweza kurudisha maendeleo yao na ya nchi yetu ya Tanzania. Ahsante sana.

**SPIKA:** Sasa, wewe mbona hukusema umeipataje?

**MHE. MUHAMMAD I. SANYA:** Mheshimiwa Spika, hii nimeipata kwa mfanyakishara wa chini kabisa, mjasiriamali ambaye anajitegemea, nilipopita njiani akaniita na akaniambia Mbunge nakuomba uitolee taarifa ili hali kama hii isiwafike wenzangu na yeye akaniambia kwamba hii shilingi 10,000/= ni *income* yake ya wiki nzima imepotea kwa sababu ya kupewa noti bandia bila ya yeye kuifahamu kwamba ni ya bandia. Baadaye alivyoitoa yeye kumpa mtu mwingine akaikataa kwa sababu ya wepesi wake na kwa sababu ya kutokuonekana ile *watermark* ya Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante kwa taarifa hiyo, nadhani Serikali itabidi itoe maelezo ni hatua gani zinachukuliwa.

Nilikuwa nimemwita Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare sijui kama yupo?

**MBUNGE FULANI:** Hayupo Mheshimiwa Spika, naomba niongee mimi kwa niaba yake. (*Kicheko*)

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya dakika kumi kulihutubia Bunge lako na Taifa kwa ujumla.

Napenda kuwashukuru sana wapigakura wa Jimbo la Magu kwa kunipa kura za ushindi, kuniamini na kuwa Mbunge kwa awamu ya tatu. Naahidi kwamba sitawaangusha na nitawatumikia kwa moyo wangu wote. Nitashirkiana nao katika kutatua changamoto na kero ambazo zinatukabili. Nawashukuruni sana Wanajimbo la Magu.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda niipongeze sana Serikali kwa uamuzi iliyochukua kwa kuanzisha Mikoa miwili, Mkao wa Geita na Mkao wa Simiyu. Msongamano wa watu katika Mkao wa Mwanza ulikuwa mkubwa sana, ulikuwa unaongoza baada ya Dar es Salaam. Msongamano wa watu katika Mkao wa Mwanza ni wakazi 177 katika kila kilomita ya mraba ikifuatiwa na Kilimanjaro yenye watu 120, Mara yenye watu 90 na mwisho kabisa ni Lindi wenye watu 14 na Ruvuma na Rukwa zenye watu 21. Kwa hiyo, uamuzi wa Serikali kugawa Mkao wa Mwanza, Geita ikawa Mkao na Simiyu ikawa Mkao, itafanya Serikali iongeze *resources* katika Mikoa hiyo na hatimaye tunaamini kwamba maendeleo yatakwenda haraka zaidi. Ninaamini kwamba kwa utaratibu wa Mkao, Makuu ya Mkao lazima yaunganishwe na Mikoa mingine kwa barabara ya lami, sasa kutoka Mwanza kwenda Bariadi barabara itakuwa ya lami ambapo naamini ndipo patakuwa Makao Makuu ya Mkao wa Simiyu.

Mheshimiwa Spika, napenda nilete kilio cha wana Magu cha njaa. Hali ya hewa haikuwa nzuri, mwaka huu wakulima na wananchi walijitahidi sana, mvua ziliponyesha wakapanda lakini sasa mahindi yamekauka na mazao mengine yamekauka na hali ni

mbaya. Kwa hiyo, naomba kwanza mgao wa chakula au tathmini ya chakula ifanywe haraka katika Jimbo la Magu na Wilaya ya Magu kwa ujumla ili wananchi waweze kupata msaada huo. Kuna Kata nyingi za Jimbo la Magu zimeathirika ikiwemo Kata ya Ng'aya, Shishani, Jinjimili, Sukuma, Magu Majini, Lubugu pamoja na Tarafa ya Sanyo, kwa ujumla sio nzuri.

Mheshimiwa Spika, ombi la pili naiomba Serikali kipindi hiki ambapo mvua zimeonesha dalili za kunyesha tupatiwe msaada wa mbegu za mtama ambazo zinastawi kwa muda mfupi. Halmashauri ya Wilaya imenunua na kusambaza tani saba mpaka sasa tunaomba Serikali iweze kutusaidia ili wananchi waweze kupata mbegu hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende kwenye mambo ya Kitaifa kuhusiana na hotuba ya Mheshimiwa Rais ya kulifungua Bunge lako Tukufu. Tunasheherekeea miaka 50 ya uhuru mwaka huu. Miaka 25 ya kwanza ya uhuru nchi yetu, tulijaribu kujenga ujamaa, mwaka 1961 mpaka mwaka 1986. Kwa kweli mambo makubwa na mambo mengi yamefanyika. Miaka 25 iliyofuata tukawa na kitu soko huria na hatukutangaza moja kwa moja kwamba sasa hatujengi ujamaa lakini tukawa na soka huria lakini Ibara ya 3 na ya 9 ya Katiba inasema nchi yetu inafuata siasa ya ujamaa na kujitegemea. Kwa hiyo, tumeachana na ujamaa na kujitegemea kihalisia lakini bado kwenye Katiba yetu tunasema tunajenga siasa ya ujamaa na kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, sasa soko huria na ujamaa na kujitegemea sikuelewa sana kama hivi vitu vinaendana. Tulifanya *liberalization* kwa kizungu tukaruhusu kwamba sasa mishahara miwili ni ruksa, kufanya biashara ruksa, lakini Katiba yetu bado inasema tunafuata Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea sio mbaya lakini lilitakiwa liwepo tamko kama walivyofanya China, China walisema sasa tunaendelea kujenga ujamaa lakini tunasema tunakuwa na soko huria na mtu kuwa tajiri ni ruksa. Lakini sisi mpaka leo tunajificha, ukitaka kuonekana tajiri unajifichaficha wakati tumetangaza tunasoko huria. Nafikiri haya ni makosa ambayo yametufanya turudi nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa wazito kama nchi kufanya maamuzi. Kuna maamuzi yamechukuwa muda mrefu sana ambayo yametuvuta nyuma. Wenzetu kwa mfano mdogo, jirani zetu Kenya wamejenga Airport katikati ya Rombo na Mombasa ambayo inakuja kuua kabisa *Kilimanjaro International Airport (KIA)*, wanajenga Bandari ya Lamu ambayo inakuja kuua kabisa Bandari ya Tanga, wamejenga bomba la mafuta kutoka Mombasa linakaribia Kampala, sisi tumeponga kujenga bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza liko kwenye makarasi, tumekuwa wazito sana kufanya maamuzi ya msingi ambayo yangebadilisha maisha ya Watanzania. Tunahitaji tujifunze, katika miaka 25 inayokuja lazima na kwa sababu kuna fursa sasa kwamba tunaandika upya ama tunarekebisha au vyovoyote utakavyosema Katiba yetu, naamini kwamba tutajipanga vizuri zaidi ili kwenda kwa *speed* zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye Idara ya Nishati na Madini. Kulingana na taarifa ya hali ya uchumi wa Taifa ya mwaka 2009, ukurasa wa 205, inasema kwamba umeme unaopotea ni mwangi kuliko umeme unaotumika kwa ujumla

kwenye viwanda na kwenye biashara mbalimbali. Mwaka 2009 umeme uliotumika viwandani ni *Kilowatt/hour* milioni 1500, viwanda vyote pamoja na biashara zote lakini umeme uliopotea ni *kilowatt/hour* milioni 1700. Sasa wakati tunafanya juhud ya kupata umeme wa ziada lazima tujiulize tunafanya nini kupunguza huu upotetu wa umeme, vinginevyo tutaongeza umeme kwenye gridi, umeme mwinge utaendelea kupotea na hii itakuwa sio kitu kizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye mazingira, asimilia 97 ya wananchi hutumia kuni na mkaa. Bei ya umeme imepanda, bei ya gesi imepanda, sasa tunategemea nini? Wananchi hawa wataendelea kutumia mkaa na kuni, miti itaendelea kukatwa, mvua itaendelea kukosekana, jangwa litakuja, umeme wa maji utapungua, mgao utaendelea kuwepo na uchumi utaendelea kudorora. Naomba suala hili la bei ya umeme na gesi na matumizi ya kuni liangaliwe kwa makini, kama hakuna njia nyingine ya kufanya Watanzania wafanye nini sasa? Kama Watanzania asimilia 97 wanatumia kuni na umeme umepanda, lazima waendelee kukata kuni na hatuna juhud za makusudi za kuhakikisha kwamba tunapanda miti kwa wingi ambayo ni ya mvua, tunasema kila mwaka tuna siku ya kupanda miti lakini baada ya hapo hakuna tunachofuatilia. Kasi ya kukata miti ni kubwa zaidi kuliko ya kupanda na kuongeza miti. Tunakata miti kama wendawazimu lakini hatupandi miti kama wendawazi. Naomba tujipange, tupande miti kama wendawazimu.

Mheshimiwa Spika, gesi ya magari, kuna wataalam wetu wamegundua kwamba unaweza ukabertilisha gari badala ya kutumia mafuta likatumia gesi. Wamefanya kazi nzuri na teknolojia hii inapunguza asilimia 50 ya matumizi ya mafuta ambayo sasa hivi tunatumia. Naomba pia tuingie huko.

Mheshimiwa Spika, madini tulioanza kuyachimba miaka ya karibuni, yametufanya tubweteke. Tumesahau sekta nyingine muhimu kama kilimo wakati tunajua kwamba madini yana mwisho. Tunayatumiae kujenga *economic base* yetu hatimaye hata kama madini yatakuwa yameisha yaweze kutusaidia kwa miaka mingine ijayo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuzungumza, naomba nimshukuru sana Mungu kwa ajili ya kunipa nafasi na kufika hapa nilipofika leo.

Vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri. Naamini kabisa nitakuwa sijawatendea haki wanawake wote wa UWT Mkoa wa Mbeya, nisipowashukuru kwa dhamana walionipa ya kuja kuwakilisha hapa Bungeni, nami ninaahidi kwamba hakika sitawaangusha.

Mheshimiwa Spika, katika vipaumbele 13 vilivyoko kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Rais, naomba nichangie katika maeneo matatu ama manne. Eneo la kwanza likiwa ni elimu, miundombinu, mazingira na ardhi. Mengi yamekwishazungumzwa na mara nyingi wanaozungumza mwishoni wanakuwa hawana pointi nyingi sana. Lakini pamoja na hayo, Serikali yetu inasomesha Walimu, mengi yamezungumzwa juu ya

maslahi ni sawa, juu ya ufundishaji, juu ya vifaa ni sawa na mambo mengimengi lakini tunatakiwa tuijilize chanzo hasa ni nini cha kushuka kwa elimu. Nilikuwa najiuliza sana, nimegundua kwamba ukaguzi katika shule zetu bado hautoshelezi. Tuna Wakaguzi wa Wilaya, tuna Wakaguzi wa Kanda ambao ni wa Sekondari, naomba Wizara husika ambayo ni ya Elimu na Mafunzo itilie mkazo sana suala la Wakaguzi wa Kanda kwa sababu hii ni sababu mojawapo ambayo inasababisha kushuka sana kwa kiwango cha elimu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, kwa mfano pale katika Mkoa wa Mbeya, Shule nyingi za Sekondari za Wasichana sio za *Boarding*, ni za kutwa na hii inapelekea sana kushuka kwa kiwango cha elimu. Nashauri Serikali kupitia Wizara husika waweze kuweka *boarding schools* ambazo zitakuwa na *facilities* zote, zisiwe *boarding schools* ambazo zitakuwa na majengo peke yake na vifaa. *Facilities* ni muhimu sana ili hao wasichana waweze kusoma vizuri masomo yao na kufaulu.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais, ukurasa wa 28 amezungumzia kuhusu Taasisi ya Teknolojia ile ya Mbeya. Tukumbuke kwamba hii Taasisi ilikuwa ni ndoto nzuri ya Mwasisi wa Taifa hili, Baba yetu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na kilikuwa Chuo cha Ufundi. Kulingana na hiki kipengele, naamini kabisa kitatekelezwa na naomba Wizara husika kwenye Bajeti ya mwezi wa sita, watutengee fungu kwa Chuo hiki ili kianze kufanya kazi na hakika kiweze kuwa Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la miundombinu, Mbeya kama tunavyoolewa sote ni *gate away* ya kwenda nchi mbalimbali. Sasa unaweza ukafika pale Uyole mpaka Mbeya kama jina langu linavyosema eneo la Mwanjelwa, unaweza ukachukua muda wa saa nzima badala ya dakika kumi tu. Ni kweli katika Bodi ya Barabara ya Mkoa jambo hili lipo lakini Wizara husika naomba iongeze nguvu kwa Jiji la Mbeya angalau kuchepusha barabara, itoke hapo Uyole mpaka eneo la Mbalizi maana foleni ni kubwa sana. Vilevile kutoka Uyole tukifika eneo la Mwanjelwa kama jina langu lilivyo basi kuwe na *round about*. Jambo hili kweli liko kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa lakini vilevile naomba Serikali kupitia Wizara husika iongeze nguvu katika Fungu husika. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwenye suala la ardhi. Ardhi inatumika visivyo na sielewi ni kwa nini. Unakuta eneo la shule, eneo la hospitali, makazi yanajengwa holeholela tu. Kwa hiyo, naomba Serikali kupitia Wizara husika waliangalie jambo hili, Tume ya Ardhi ipewe nguvu, ipewe Fungu ili hakika kila jambo lifanyike vile inavyostahili na tuweze kupata sifa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tumezungumza sana masuala ya ufundi stadi kwamba Vyuo vya VETA vijengwe. Ni kweli Ilani ya Uchaguzi inazungumzia hivyo lakini je, haya majengo yakijengwa vifaa viro? Lazima tuangalie sana *production*, *Craftsman* ni wachache sana. Sasa tukiwa na haya majengo, Walimu tunao? Wizara husika naiomba iliangalie jambo hili kwa kina sana, tusije tukajikuta tuna majengo tu

halafu Walimu hatuna. Ni jambo la msingi ambalo Wizara husika inapaswa iliangalie kwa makini.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, Mbeya ni Mkoa ambao una milima mingi sana na milima hii ni chanzo cha maji lakini unakuta kuna kuchoma moto sana katika misitu. Sasa naomba kupitia Wizara husika iliangalie jambo hili chanzo chake ni nini kwa sababu tunazungumzia mazingira. Mazingira haya na milima hii ambayo ni chanzo cha maji halafu wakati huo huo moto ukawa unachomwa ovyo, Serikali kupitia Wizara husika inachukua hatua gani. Naomba iliangalie kwa uhakika na kwa ukaribu sana suala hili.

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa, nisingependa nirudie yaleyale. Baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu. Naomba na mimi nishiriki katika kuchangia hoja ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, naomba kwanza niwashukuru wapigakura wangu wote kwa ujumla, wananchi wa Ukerewe bila kujali itikadi zao za vyama. Mwenyezi Mungu awasadie sana, awazidishie maisha marefu ili niendelee kuwa kiongozi wao vipindi vitatu mfululizo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sitendi haki kama nitakuwa sijafikisha kilio chao kwa Serikali. Tatizo kubwa linalowasumbuwa watu wa Ukerewe, kabla sijaendelea kuchangia, ni tatizo la uhaba wa chakula. Tatizo la uhaba wa chakula linatokana na ugonjwa wa muhogo. Ugonjwa huu wa muhugo umeenea sana katika Bonde la Mto Mara pamoja na Kisiwa kizima cha Ukerewe. Zao kubwa tunalotegemea Ukerewe, ni zao la Muhogo, ndicho chakula chetu kikubwa, kimetukuza na mpaka tumezeeka. Sasa ugonjwa wa baobao ambao sasa hivi naweza kusema kwamba ni Janga la Kitaifa, umevamia katika Kisiwa cha Ukerewe. Siku ya kikao cha *briefing* nililifikisha kwa Waziri Mkuu lakini bado naendelea kulifikisha zaidi kwenye Wizara husika hasa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa. Wakerewe wanashida kubwa sana, hawana zao mbadala wanadolitegemea kama zao la chakula zaidi ya zao la muhogo. Sasa hivi wanategemea kupata muhogo wa kununua kutoka katika Mkoa wa Mara kwa uchache zaidi lakini kwa wingi wanapata kutoka Wilaya za Sengerema na Geita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kikubwa zaidi kinachowaliza wana Ukerewe...

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa umetukatisha kati yangu mimi na msemaji, endelea Mheshimiwa Naluyaga.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Spika, sanasana kinachowaliza wana-Ukerewe ni kwamba wamekabiliwa na njaa wakati hawana zao mbadala la biashara linalowaingizia pesa ya kuweza kununua hicho chakula. Debe moja la udaga au kile kisado cha lita tano, sasa hivi kwa Ukerewe kinanunuliwa kwa Sh.2500/-

mpaka Sh.3000/- mtu mwenyewe familia ya watoto 15 au 10 au watano anakitumia kile kisado kwa muda wa siku moja kwa milo miwili, mchana na jioni na hana zao lingine mbadala la biashara analoweza kuuza ili aweze kununua kasado kamoja ka udaga, naiomba Serikali itilie mkazo suala hili ilione kama Janga la Kitaifa, iwasaide wana-Ukerewe kwa haraka sana, iwavelekee chakula cha msaada na wapewe bure.

Mheshimiwa Spika, kwa nini wapewe bure? Nasema wapewe bure kwa sababu uchumi wa Mkerewe unategemea uvuvi na uvuvi wenyewe wanaotegemea zaidi ni ule uvuvi wa makokoro, ndiyo waliokuwa wanautegemea zaidi kwa sababu kipato chao ni kidogo. Serikali imesema sasa hivi uvuvi ule ni harama kwa sababu unatumia matundu madogo. Kwa hiyo, makokoro yote yamefungiwa, yako jela na yamefungwa pingu ina maana wananchi wetu wenyе kipato cha chini hawana zao lingine mbadala la biashara wanalueza kuuza wapate hela ya kununulia udaga au mahindi. Kwa hiyo, rai yangu ni hiyo, nifikishe kilio kwa Waziri husika na Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa, aweze kuwasaidia kwa haraka sana kuokoa maisha ya Wakerewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais. Wakati Mheshimiwa Rais anafanya mikutano yake ya kampeni aliahidi kwamba ataleta meli nyingine kubwa katika Ziwa Victoria, kama meli hii itakuja, basi ifanye haraka na ipolekwe Ukerewe kwa sababu usafiri unaotumika sasa hivi ni usafiri wa *Boat* ya *MV Clalias*. Mimi ni mjukuu wa tano wa ile *Boat*, inapata matatizo, wakati mwingine inakwenda hadi katikati ya Ziwa inazimika. Yaliyotukuta kwenye MV Bukoba yanaenda kutukuta Ukerewe. Kwa hiyo, tuchukue tahadhari ya dhati, Serikali iliangalie kama nalo ni janga linatunyemelea, ituletee meli nyingine ili kusaidia usafiri na kuondoa kero inayowapata wananchi ambao wametengwa na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, Kisiwa cha Ukerewe kimezungukwa na maji asilimia 90, lakini cha ajabu leo wakazi wa Ukerewe wanapata shida ya maji ya kunywa. Serikali ya Awamu ya Kwanza iliweza kuweka mitambo ya kusukuma maji katika Vijiji vya Nansio, Chabilungo, Ihebo, Galu, Bukonyo, Bugolola, Bukindo, Bwisha na Kisiwa kidogo cha Ilugwa lakini katika mashine zote hizi, katika mitambo yote niliyoitaja, ni mtambo mmoja tu wa Nansio ndio unaosukuma maji. Sasa hivi Serikali inabuni kwenda kuchimba visima katika Kisiwa, inatumia pesa nyingi, mradi unaoendelea sasa hivi, maarufu kama mradi wa Koi, kila Kijiji kinatumia shilingi milioni 300 kuchimba visima. Hizo milioni 300 zingeenda kwenye mashine moja, ikanunua vipuri, hiyo mashine au pampu moja ingeweza kusambaza maji katika Vijiji au Kata zipatazo tatu au Kata nne. Kwa nini Serikali sasa isifikirie kubadilisha mradi badala ya kupeleka visima vingi katika Wilaya ya Ukerewe ambayo haina miinuko mingi, wakichimba wanapata maji ambayo siyo safi kwa chini, basi, ivute maji ya Ziwa Victoria. Kama Serikali imeweza kupeleka mradi wa maji katika Mkoa wa Shinyanga mpaka Kahama, leo sisi wana-Ukerewe tunapiga kelele kupata maji salama na ya kunywa, huku ni katuonea. Tunaiomba Serikali ifikirie kwa makini zaidi kuzifufua hizi mashine nilizozitaja katika Vijiji hivyo nilivyovitaja hapa.

Mheshimiwa Spika, suala la ulinzi na usalama, Kisiwa cha Ukerewe ndiyo kiko mpakani na nchi ya Kenya na Uganda. Serikali ifikirie sasa kwamba ni wakati muafaka wa kuweza kuweka doria za kutosha kwa sababu wananchi wa Ukerewe ambao

wanategemea zao kubwa la uvuvi, wanakufa bila kuwa na hatia. Limetokea tukio hivi karibuni, mwaka jana wavuvi 15 wameuwawa kwa mashine ya kivita, *SMG* na ikaonekana kwamba kuna *element* fulani za Usalama wa Raia zimehusika kwa sababu kuna nembo za Polisi zilikutwa katika eneo la tukio lakini Serikali inajivua katika tatizo kama lile. Ni kutowatendea haki wananchi wanaokaa sehemu ile. Tuzibe mianya inayosababisha wananchi kukosa amani kwa sababu ni Kisiwa na siku moja Serikali ifikirie kuweka Kambi ya Jeshi katika Kisiwa cha Ilugwa kilichoko mpakani.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wavamiaji wakitoka Kenya au Uganda wanaingia Tanzania bila kuwa na kikwazo chochote. Ukiingia katika Visiwa vya Gana, ukaingia katika Visiwa vya Izinga kule yalikotokea mauaji ya Kimbari, kuna wavamizi wanaotoka Somalia, wanaotoka Kenya wanaishi kama wako kwenye nchi zao. Wanaiba, wanavua eneo lile, wanaondoka wala hawaaulizwi. Tunapoteza Pato la Taifa kwa kutoweka ulinzi katika hali kama hiyo. Wavuvi sasa hivi wanavua katika Visiwa vya Ilugwa, wanawasha mashine zao, wanaenda kuuza samaki Kisumu kwenye viwanda vyao vya Kenya, kiasi kwamba kama ingekuwa imedhibitiwa, hawa samaki wangeletwa katika viwanda vya Musoma na viwanda vya Mwanza hatimaye vingeleta mapato kwenye Taifa letu. Kwa hiyo, Serikali ifikirie kwa makini zaidi, isikiache Kisiwa cha Ukerewe kuwa na mianya ambayo kinaweza kuwa na mwingiliano wa nchi nyingine za jirani bila Serikali kufuatilia.

Mheshimiwa Spika, nigosie kidogo suala la barabara kwa sababu mimi ni Waziri Kivuli wa Miundombinu...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Regia Mtema!

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais kufanya mambo mawili makubwa yafuatayo:-

La kwanza kabissa, ni kutoa pongezi za dhati kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kwa matokeo mazuri yaliyopatikana katika Uchaguzi Mkuu uliopita wa mwaka jana. Natambua ni kutokana na juhudhi za pamoja, viongozi, wanachama na wapenzi wa CHADEMA, tumeweza kufika hapa tulipofika. Kwa matokeo haya tuliyoyapata CHADEMA, ni ishara za wazi kwamba utawala wa Chama cha Mapinduzi kuendelea kuwa madarakani unahesabika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kilombero, Morogoro kwa jinsi ambavyo walikuwa na imani nami. Nilishiriki kwenye Uchaguzi Mkuu mwaka jana, walinipa kura nyingi pamoja na kwamba sikubahatika kutangazwa mshindi. Nawashukuru kwa kuwa hawakuangalia

ulemavu wangu, hawakuangalia jinsia yangu ya kike wala hawakuangalia hali yangu ya kiuchumi, waliweza kunimiminia kura nyingi, nilipata kura 38,550, nawashukuru sana ndugu zangu wa Kilombero. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni hili kubwa la kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Katika hotuba hii, Mheshimiwa Rais ameainisha mambo kadhaa na ya msingi kabisa ambayo kwa hakika yalihitaji kujadiliwa kwa kina na sisi Wabunge ili kuweza kutoa mwelekeo na kumsaidia Rais kulifikisha Taifa letu kwenye miaka 50 ya pili ya uhuru wa Tanzania Bara na miaka michache ijayo tutaazimisha miaka 50 ya Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, ameainisha wazi kwamba uchumi wa Taifa letu umekua kwa asilimia 7.1 lakini kuna mambo kadhaa ambayo yamesababisha kwamba pamoja na ukuaji huu wa uchumi wa Taifa letu, bado uchumi huu hauendani na maisha halisi ya Watanzania walio wengi. Natambua kuna sababu mbalimbali yakiwemo mambo makubwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tumeona kabisa katika awamu iliyopita kumekuwa na ubadhirifu mkubwa uliofanywa na Viongozi wa Umma, matumizi mabaya ya madaraka, kumekuwa na kutowajibika, kumekuwa na uzembe, kumekuwa na kuoneana aibu na hata kubebana pale pasipostahili kubebana. Haya yote yamesababisha uchumi wetu kutoendana na hali halisi ya Watanzania. Napendekeza tuiangalie upya hali hii ambayo inaendelea katika Taifa letu la Tanzania. Ninapendekeza kama inawezekana, basi tuwe na Wizara Maalum ambayo ingekuwa ina-*deal specifically* na maadili ya watumishi ili kuhakikisha kwamba maadili ya Watumishi wa Umma kuanzia ngazi ya juu mpaka kwenye ngazi ya Kitongoji, yanafanyiwa kazi au yanatekelezwa kwa mapana yake ili tuweze kuendana na kasi yetu ya uchumi amba tunajivunia leo kwamba uchumi umekua, lakini Watanzania walio wengi bado ni maskini.

Mheshimiwa Spika, leo hii Rais wetu anasema nchi yetu imepaa kiuchumi, lakini hali ya elimu sisi wenyewe tumeshuhudia kwamba bado ni duni. Leo hii kiwango cha elimu kimeshuka kwa kiwango kikubwa sana. Inasikitisha miaka 50 baada ya uhuru watoto wetu wanaingia Vyuo Vikuu kwa viwango vya chini, unakuta mtu ana E, E, E anaingia Chuo Kikuu. Matokeo yake leo hii hakuna tofauti ya mtu mwenye *PhD* na mtu ambaye amepata *Degree* ya kawaida. Kwa kweli kiwango chetu cha elimu kimekuwa...

**MBUNGE FULANI:** Siyo kweli!

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Huo ndio ukweli.

**MBUNGE FULANI:** Siyo kweli!

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika, kiwango chetu cha elimu kimepungua, mtu mwenye *Ph.D* hana tofauti na mtu mwenye *Degree* ya kawaida.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, wenye *degree* wako wengi humu! Wenye *degree* hizo wako humu humu na wamesomea humu humu, sasa sijui ndio hao unaowasema! Haya Mheshimiwa Regia endelea! (*Kicheko*)

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni kweli kiwango chetu cha elimu...

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge!

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, ukirejea Kanuni za Bunge letu Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kanuni ya 64(a) inayosema kwamba:-

“*Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli*”.

Mheshimiwa Spika, ni vyema msemaji angetupa taarifa za kina zenyé ukweli ili iweze kusaidia Taifa letu.

**SPIKA:** Ingawa ni maoni yako Mheshimiwa Regia, lakini hawa waliosoma hapa hapa ndiyo waliomo humu humu na ndio wengine Mawaziri Vivuli na wengine Mawaziri kweli kweli. Nadhani kweli elimu imeshuka lakini hebu jaribu kusema vizuri zaidi kuliko hivyo.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo maono yangu, kwamba mimi sasa hivi sioni tofauti kati ya mtu mwenye *Ph.D* na mtu mwenye *degree* ya kawaida kwa maana ya *thinking capacity*.

Mheshimiwa Spika, leo hii tukiwa tunajivunia kwamba uchumi wa Taifa letu umepaa lakini tunaona ni jinsi gani ambavyo wananchi kule vijijini wanapata shida kupata huduma muhimu, wanapata shida kupata huduma za afya, wanapata tabu kupata mbolea ya ruzuku, wanapata shida hata katika masuala ya msingi kabisa ya maji kama ambavyo Wabunge wengine wameainisha.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kengele ya kwanza imegonga, nitakuwa sijatenda vyema kama sitazungumzia watu wenye ulemavu pamoja na wananchi wa Jimbo la Kilombero.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunaadhimisha miaka 50 ya uhuru wa Taifa letu lakini bado watu wenye ulemavu tupo katika matatizo makubwa, bado mpaka leo *enrollment ratio* ya wanafunzi wenye ulemavu ni ndogo, bado mpaka leo ajira kwa watu wenye

ulemavu ni tatizo, bado mpaka leo maeneo muhimu ambayo watu wenyewe ulemavu tunatakiwa tufike tunashindwa kufika, bado mpaka leo hata kwenye vyombo vyaa maamuzi watu wenyewe ulemavu hatupati nafasi za kutosha. Namwomba Mheshimiwa Rais aliangalie suala hili kwa mapana yake.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie wananchi wa Jimbo la Kilombero. Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kwamba mpaka leo miaka 50 baada ya uhuru pamoja na kwamba Wilaya ya Kilombero imekuwa ni mionganini mwa Wilaya chache katika Taifa hili la Tanzania, kwa kuwa na rasilimali mbalimbali, Wilaya ya Kilombero imebahatika kuwa na migodi miwili ya kuzalisha umeme, tuna Kihansi na Kidatu, lakini inasikitisha taarifa za TANESCO zinaonyesha kwamba watu wa Kilombero wanaopata umeme ni chini ya asilimia moja peke yao. Zahanati karibu zote ndani ya Wilaya ya Kilombero tunatumia chemli, tunatumia vibatari, inasikitisha sana, naomba liangaliwe kwa mapana sana suala hili.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na Kanuni ya 28(5) ambayo inasema:-

*“Iwapo shughuli zilizopangwa kwa siku hiyo zimemalizika kabla ya saa 1.45, Spika ataliahirisha Bunge bila kuhoji, lakini iwapo zimesalia dakika 15 kabla ya kufikia muda wa kuahirisha kikao na Bunge au Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi bado haijamaliza shughuli zake, Spika anaweza kuongeza muda usiozidi dakika 30 bila kulihoji Bunge au Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi ili kukamilisha shughuli zilizobaki”.*

Sasa wale wanaohesabu kura wanakaribia kumaliza, naongeza dakika 30 Bunge liendelee na kwa maana hiyo namwita Mheshimiwa Mariam Mfaki aendelee kuchangia wakati tunaendelea kusubiri matokeo. Kama hayupo, namwita anayefuata, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Maria Mfaki yupo?

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nipo!

**SPIKA:** Basi, karibu Mheshimiwa Mariam Mfaki.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia jioni ya leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi sote tulioko kwenye Jengo hili kupata ridhaa kutoka kwa wananchi wetu kila mmoja mahali pake na kuweza kuingia katika Jengo hili, kwa hiyo, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kwake kwa kura nyingi na kuweza tena kuongoza nchi hii. Vilevile naomba niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyotenda kazi zake. Ni mtu ambaye ni mvumilivu, ni mchapakazi, ni mtu aliye na uwezo wa hali ya juu. Kwa ujumla aliongoza miaka mitano kwa kiwango kizuri na sasa hivi ataendelea kutuongoza kwa amani na utulivu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe mwenyewe kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili. Sisi wanawake wenzio kwa kweli tunajivuna. Naamini kwa uwezo mkubwa ulionao, utafanya kazi hii na wala hakuna chochote kitakachokutisha na hata likitokea jambo lolote, nina uhakika, kwa uwezo wako litayeyuka na wala halitafika mahali popote.

Mheshimiwa Spika, wako wengi wa kupongeza, lakini vilevile nirudi mimi mwenyewe katika Mkoa wa Dodoma. Naomba nichukue nafasi hii, kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Dodoma kwa kuniwezesha kunichagua kuwa Mbunge kwa kipindi hiki cha tatu. Naamini ni kwa ajili ya ushirikiano wao mzuri na mimi ndiyo maana wanaendelea kuniamini. Nawashukuru sana na Mungu awajalie na wafanye kazi zao vizuri kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kuzungumzia suala kubwa ambalo binafsi nimeona ni vizuri kwa upande wa wanawake liweze kupewa umuhimu na kufanyiwa kazi. Sisi wanawake tumeamua kuanzisha Benki ya Wanawake ambayo kwa kweli ikizidi kukua itatusaidia sisi wanawake katika nchi nzima. Nachoomba ni kwamba Benki hii sasa iweze kufungua matawi Mikoani na ikiwezekana hata Wilayani. Lakini kwa sababu mtaji wake ni mdogo, tunaomba wale wanaoshughulikia Benki hii waendelee kuitangaza na vilevile uandaliwe utaratibu mzuri ambao utawawezesha wanawake wengi kutoka katika Mikoa mbalimbali na Wilaya mbalimbali kujiunga katika Benki hii. Wakijiunga wengi, tuna uhakika kwamba Benki hii inaweza ikawa na mtaji mkubwa na ndipo matawi yatakapofunguliwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda nizungumzie, ni suala la amani na utulivu. Nina hakika kama si amani na utulivu ambao umejengwa na Chama cha Mapinduzi kuanzia mwanzo mpaka hivi sasa, bila amani humu ndani tusingeweza kukaa, bila utulivu wa nchi yetu hii, humu ndani hatuvezi kukaa maana yake ni kwamba ingekuwa ni vita moja kwa moja. Wale ambao hawaitakii mema nchi hii, nawaomba sana warudi wakakae chini waweze kujipanga vizuri na waone ni vipi ambavyo nchi hii tutashirikiana kwa pamoja na kuweza kusaidia na kuimarissha amani na utulivu tulionao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ninauhakika, bila ya kuwa na amani hatuvezi kufanya kitu chochote na ninaamini wananchi wa Tanzania sasa hivi wanajua ni nini tunachofanya ndani ya Bunge, tunatakiwa tuwe mifano, wao ndiyo wanatakiwa watuige sisi. Kitu cha msingi, ni vizuri basi wenzetu waliopo Kambi ya Upinzani walione hilo, kwa sababu wananchi wametuchagua ili kuja kufanya kazi zao na kuwatetea na kuwalettea maenedeleo, kama tutakuja kuanza kazi ya kutoka na kuingia, ninahakika

hawatatumchagua tena, kwa sababu wananchi hawakutuambia nendeni mkatoke kwenye Bunge na mrudi kwenye Bunge. Ninaamini wewe uliyekaa katika kitu hicho, unayetuongoza tunapaswa kukuongoza na tunapaswa kukutendea haki, pamoja na kwamba kuna haki ya kutoka na kuingia lakini vilevile ni vizuri kutumia busara zaidi ili nchi yetu na Bunge letu liweze kuheshimika ndani ya nchi na nje ya nchi na wale waliochagua watusifu kwamba tunafanya kazi zetu vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la maji, tunazo Wilaya ambazo ni mpya ukiacha hizi zilizotajwa mwishoni, Wilaya hizi nyingi ambazo bado hazijaweza kukamilisha majengo yao kwa mfano Wilaya ya Bahi katika Mkoa wa Dodoma tayari majengo ya Ofisi ya Halmashauri yameshajengwa, bahati mbaya tunashindwa kuhamia kule kwa sababu ya maji. Rais alipokuwa kwenye kampeni tulimlalamikia kuhusu tatizo hilo na ye ye akaahidi kwamba suala la maji litashughulikiwa, tungeomba basi lishughulikiwe kwa sababu Wilaya ya Bahi ni kubwa, ina watu wengi na kwa kweli sasa hivi wengi wanatamani kwenda kujenga Bahi, lakini bahati mbaya hatuna maji ya matumizi kwa ajili ya binadamu, maji yaliyopo yana chumvi nyingi hayafai kwa kunywa wala hayafai kwa shughuli mbalimbali. Naiomba Wizara inayohusika iweze kuliona hilo na iweze kulishughulikia suala la Bahi.

Mheshimiwa Spika, vilevile watumishi wa Wilaya ya Bahi amba kwa sasa hivi bado wanaishi Mjini Dodoma na wanaendelea kufanya kazi hapa Dodoma, lakini tukizungumza suala la kuhamia Bahi bado tatizo linakuwa kwamba pesa za kujikimu au malipo ya uhamisho hawapewi. Tunaiomba Wizara inayohusika iweze kufanya maandalizi ya kuwapatia hawa watumishi pesa za kujikimu ili waweze kuhamia Bahi. Kwa maana hiyo basi majengo yaliyojengwa na Serikali kwa maana ya kwamba watumishi hawapo pale yataharibika haraka na hayatumika tena. Tunaomba Wizara inayohusika iweze kulishulikia suala hili ili majengo yale yaweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la maslahi ya wafanyakazi. Wafanyakazi wetu wengi waliopo kwenye Wizara na Halmashauri, wana madai ya aina mbalimbali. Naiomba sana Wizara zinazohusika zijaribu kushughulikia madai hayo na hasa Walimu. Bahati mbaya Walimu hao wametawanyika katika nchi nzima, kila Kijiji kuna shule na kila Kijiji kuna Walimu, matokeo yake ni kwamba hata madai yao namna ya kuyafuatilia inakuwa kazi. Sasa tunaiomba sana Wizara ya Elimu ijaribu kuliangalia hilo na iweze kulishughulikia ili waweze kupata malipo yao.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la vijana. Kama tunavyosema ni kwamba, vijana ni wengi kuliko watu wazima na leo kulikuwa na ajenda ya suala moja kwamba, wazee tupo ni dawa kama alivyosema Spika na kwa kweli bila ya wazee, mengi yanaweza yakaharibika. Nawaomba vijana wetu amba wanamaliza shule unakuta hawana maeneo au hawana kazi za kufanya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, sasa nitamwita Mheshimiwa Maria Hewa.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili niseme machache kuhusu hotuba ya Rais wetu mpandwa, Jakaya Mrisho Kikwete.

Awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka salama hadi sasa na kwamba naendelea kuimarika, anaendelea kuniinua na afya yangu ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nipende tu kuchukua nafasi hii kuwaambia wana-Mwanza kwamba aliye na macho haambiwi tazama, wanatuona humu tunavyohangaika na kuona hali halisi kwamba Mwanza ilifanya nini na nini kinatendeka humu Bungeni. Lakini pia nizidi kuwatia moyo kwamba kutereza siyo kuanguka, nipo, tutaendelea kushauriana na tutajipanga vizuri.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwasifu wale waliofanya vizuri. Ni ukweli usiofichika kwamba Tanzania hii bado inaendelea kuipenda CCM na Rais wao wa kweli na uhakika, ni Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Tuseme tu iliyo kweli kwamba katenda mema mengi, katenda mazuri mengi, lami, barabara, maji, na sehemu nyingi tu ameweza kutenda yaliyo mazuri na ndiyo maana Tanzania ikaona imrejeshe kwa maana ya miaka mitano tena, mtaona maajabu mbele ya safari.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wachangiaji wamesema amani Tanzania ipo tu, eti utulivu upo tu, upendo upo tu, jamani amani ni gharama, upendo ni gharama na utulivu ni gharama. Si rahisi mkakaa katika amani eti mpo mpo tu! Iko gharama yake, inahitaji kukaa na kuwaza hivi tunapaswa kufanya nini ili tuwe na amani, tunapaswa kufanya nini ili utulivu uendelee, tunapaswa kufanya nini ili upendo uendelee. Naomba mkariri hayo kwamba yote hayo matatu ni gharama na CCM imeghamika katika hili ndiyo maana tuna vyote hivyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia machache tu katika hotuba ya Mpandwa wetu Rais. Jambo la kwanza, napenda kuzungumzia suala la ufu fuaji wa viwanda. Viwanda tutake ama tusitake, ni maeneo ambayo ndiyo yanabeba vijana wetu wengi sana katika suala zima la ajira. Tuone umuhimu wa kuvifufua viwanda vyetu vilivyopo na tuweze pia kuweka vipyta kwa sababu maeneo yapo. Nasema hivi kwa sababu ninaona kwa macho viwanda vipyta vinavyojengwa, mimi huwa natoka Dodoma wakati fulani nachukua basi au gari binafsi au gari langu ambalo nimewezeshwa na wapigakura wangu wa Mwanza, unapita eneo kwa mfano Mkoa wa Singida wamejenga Kiwanda cha Mafuta, unaona watani zangu hawa Wanyiramba na Wanyaturu wamechangamka kweli na mafuta hayo, tunaenda tunadondosha hela tu, yote hiyo ni kwa sababu wanatuuzia mafuta, akipata galoni yake moja kwa elfu kumi na mbili au kumi na nne anachomoka haraka, anaenda kununua kipande cha bat. Kwa lugha nyingine viwanda vinachangamsha kwa kutoa ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali, kwa yeote aliye Waziri wa Viwanda, Mwanza sisi viwanda viwo, siku zote tunapiga kelele humu Bungeni viwanda vifufuliwe Mwanza uanzie na Kiwanda cha Ngozi ili tuweze kuwaweka vijana wetu Mwatek, tuweze kuwewka Vijana wetu Nyanza *Glass* ili vijana wetu wafanye kazi, hivi kuna ugumu gani? Tunaiomba Serikali kufufua viwanda angalau hata kimoja baada ya kingine, tutaweza kufika.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, naomba nizidi kusisitiza suala la wavuvi. Tunawakamata wavuvi wa mwisho waliouziwa hivyo vifaa vya kuvulia, hivi wavuvi wakubwa mnawaogopa nini? Kipindi kingine tutakuja kuuliza maana wale wanaochomewa nyavy tunawaona, wale wanaotuletea nyavy mbona hatuwaoni? Tufike mahali na wao muwa-expose, muwaoneshe tuwaone. Watoeni hadharani na wenyewe tuwaone, ndiyo hao wanaofanya hawa wanunue, mnunuaji wa kawaida asipoiona hawezi kufanya uharamu huo lakini kama viwo alale njaa na anaviona? Tuone mnawakamata na hawa amba wanasababisha hawa watu kulala na njaa kwa sababu kanunua kutoka kwa mtu tajiri na wenyewe muwaoneshe tuwaone. Tendeni haki kwa watu wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu, nazidi kusisitiza jamani Serikali iingie kazini. Ahsanteni kwa kunisikiliza, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante, huyu ndiye msemaji wetu wa mwisho na naona matokeo ya kura yapo tayari, *Returning Officer* asome.

## MATOKEO YA UCHAGUZI

**NDG. JOHN JOEL - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, baada ya zoezi lote la kupiga kura kukamilika, naomba nitangaze matokeo kama ambavyo Wabunge wamepiga kura hizo.

Mheshimiwa Spika, kundi la kwanza la Wabunge wa Chama Tawala, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo amepata kura 77; Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye amepata kura 95; Mheshimiwa Kidawa Hamad Salehe amepata kura 94; Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo amepata kura 221; Mheshimiwa Salehe Hamed Pamba amepata kura 231; Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari amepata kura 243; Mheshimiwa Godfrey Zambi amepata kura 250 na Mheshimiwa Abdulkarim Shah amepata kura 270. Mheshimiwa Boniface Simbachawene alijitoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kundi la Chama Tawala waliochaguliwa kuwa Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge, ni Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah, Mheshimiwa Godfrey Zambi; Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari; Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kundi la pili la Wabunge wa Kambi ya Upinzani, walikuwa wanapigwi wajumbe wawili mmoja amepita bila kupingwa, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kura zilizopigwa kwa wale wawili Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya amepata kura 85, Mhehsimiwa Agripina Zaituni Buyogera amepata kura 200. Kwa maana nyingine, Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera amechaguliwa kama mwanamke kuungana na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed ambaye amepita bila kupingwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo wajumbe wa Tume ambao wamechaguliwa na sisi wenyewe ndani ya Bunge hili ni Mheshimiwa Abdulkarim Shah; Mheshimiwa Godfrey Zambi; Mheshimiwa Dokta Maua Abeid Daftari; Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo; Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Agripina Buyogera. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hawa ndio tuliochagua sisi, katika ile Tume, Spika ni Mwenyekiti, Naibu Spika ni Makamu Mwenyekiti na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani anaingia kwa nafasi yake, pia Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, ndio wanaofanya kazi hii. Kwa hiyo, nawashukuru sana, naomba kuwapongeza, tunakaribia kumaliza muundo mzima wa viongozi ndani ya Bunge letu. Tumeacha kazi nzito sana ile ya Wenyeviti wa Kamati, nilifikiria kwamba tuzoeane kidogo kwa kipindi hiki ili tutakapochagua baadaye iwe rahisi kufanya maamuzi.

Waheshimiwa Wabunge, nawapongeza wote waliochaguliwa, nawapongeza na wengine pia waliodiriki kugombea. Kazi hii zamani nilikuwa nafikiria ni mambo rahisi lakini kumbe siku hizi imekuwa ni kazi kweli, kwa hiyo, nawapongeza sana wote kwa kujaribu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo machache, kwanza kabisa, Waziri wa Fedha anakumbusha kwamba zile fomu hamjajaza na shughuli nzima inatakiwa ikamilike na pia mkijaza mapema ni vizuri zaidi kwa sababu kama ni mkopo ukianza kulipa mapema unakuwa mdogo zaidi, ukichelewa unarundika deni katika kipindi kifupi. Kwa hiyo, ni vizuri mkijaza fomu mapema na zikarudishwa panapohusika.

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Kamati ya Wabunge wa CHADEMA, anawatangazia kutakuwa na kikao cha Kamati siku ya Jumanne tarehe 15 Februari, saa saba mchana mara baada ya kikao cha asubuhi, chumba 231.

Katibu wa Chama cha Mapinduzi hapa Bungeni anaomba niwatangazie Wabunge wote wa CCM kwamba wana kikao katika ukumbi wa Msekwa baada tu ya kuahirisha Bunge, kwa hiyo wakitoka hapa waende kule.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyoeleza, kesho tena tuna uchaguzi mwingine wa Wawakilishi Vyuoni, tutafanya baada ya kipindi cha maswali, wakati tunaendelea kuhesabu, tutaendelea na majadiliano, lakini jioni tutawaachia upande wa pili wa Serikali waweze kutoa ufanuzi wa hapa na pale kutokana na mjadala mlionfanya. Kwa hiyo, watakaopata nafasi watakuwa wachache sana lakini kama ninavyosema ni kwamba hotuba ya Rais, bado mna kipindi cha bajeti ambapo mtajadili kwa kirefu sana, haya ya kusema kwangu hakuna maji, hakuna nini, kwa hotuba hii kwa kweli wamesikia lakini haina uzito unaostahili, wakati wa bajeti ndipo mtakaposema na mnawenza kuchukua hatua zinazofaa.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana, kwa jioni hii. Kwa kuwa sina matangazo mengine, napenda kuahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.02 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumanne,  
Tarehe 15 Februari, 2011 Saa Tatu Asubuhi)*